



TRI-COUNTY MWONGOZO WA MWANACHAMA WA 2023

SWAHILI
Januari 1, 2023
1-877-600-5472 (TTY 711)

[TrilliumOHP.com](https://www.TrilliumOHP.com)

Masasisho ya Mwongozo

Trillium Community Health Plan hutuma mwongozo wa mshirika kwa barua kwa washirika wapya walioandikishwa au walioandikishwa upya wakati ambapo Oregon Health Authority (OHA) hutuarifu kwamba umeandikishwa katika Oregon Health Plan (OHP), inavyohitajika na sheria ya shirikisho. Hapa ndipo unapoweza kupata mwongozo uliosasishwa zaidi

www.trilliumohp.com/members/oregon-health-plan/for-members/handbooks-forms.html.

Ikiwa unahitaji usaidizi au una maswali, pigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja simu kwa 877-600-5472; TTY: 877-600-5473.

VIDOKEZO MUHIMU:

- Rejelea sehemu ya mwisho ya mwongozo kwa ufafanuzi wa maneno yanayoweza kuwa muhimu kujua
- Kuwa na kadi zako za kitambulisho cha mshirika cha OHP na Trillium Community Health Plan wakati wote.
 - Kumbuka: Hizi zitatolewa kila moja kivyake, na utapokea kadi yako ya kitambulisho cha OHP kabla ya kadi yako ya kitambulisho cha mshirika cha Trillium Community Health Plan.
- Unaweza kupata Kadi yako ya Kitambulisho cha Trillium Community Health Plan ndani ya kifurushi cha makaribisho kilicho na mwongozo huu wa mshirika. Kadi yako ya kitambulisho ina maelezo yafuatayo:
 - Jina Lako
 - Nambari Yako ya Kitambulisho
 - Maelezo ya Mpango Wako
 - Jina na Maelezo ya Mtoa Huduma Wako wa Msingi
 - Nambari ya Simu ya Kitengo cha Huduma kwa Wateja
 - Nambari ya Simu ya Ufikiaji wa Lugha
- Mtoa Huduma Wangu wa Msingi ni _____
 - Nambari yake ni _____
- Daktari Wangu wa Meno wa Msingi ni _____
 - Nambari yake ni _____
- Watoa Huduma Wengine nilio nao ni _____
 - Nambari yao ni _____

Usaidizi wa bila malipo kwa lugha na miundo mingine.

Kila mtu ana haki ya kujua kuhusu mipango na huduma za Trillium Community Health Plan. Washirika wote wana haki ya kujua jinsi ya kutumia mipango na huduma zetu.

Tunatoa aina hizi za usaidizi wa bila malipo:

- Wakalimani wa lugha ya ishara
- Wakalimani wenye sifa zinazostahili na waliothibitishwa wa lugha ya kuzungumzwa wa lugha nyingine
- Nyenzo zilizoandikwa kwa lugha nyingine
- Breli
- Maandishi makubwa
- Sauti na miundo mingine

Unaweza kupata mwongozo huu wa mshirika kwenye tovuti yetu katika: www.trilliumohp.com/members/oregon-health-plan/for-members/handbooks-forms.html Ikiwa unahitaji usaidizi au una maswali, pigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja simu kwa 877-600-5472; TTY: 877-600-5473

Pata taarifa kwa lugha au muundo mwingine.

Wewe au mwakilishi wako anaweza kupata nyenzo za mshirika kama mwongozo huu au notisi za CCO kwa lugha nyingine, maandishi makubwa, Breli au muundo wowote unaopendelea. Utapata nyenzo ndani ya siku 5 baada ya ombi lako. Usaidizi huu ni wa bila malipo. Kila muundo una taarifa sawa. Mifano ya nyenzo za mshirika ni:

- Mwongozo huu
- Orodha ya dawa zinazolipiwa na bima
- Orodha ya watoa huduma
- Barua, kama notisi za lalamiko, kukataliwa na rufaa

Matumizi yako ya mafao, malalamiko, rufaa, au usikilizaji wa kesi hayakataliwa wala kuwekewa vikomo kulingana na hitaji lako la lugha au muundo mwingine.

Unaweza kuomba nyenzo kielektroniki. Jaza fomu salama ya mawasiliano kwenye tovuti yetu katika www.trilliumohp.com. Tafadhali tujulishe hati ambazo ungependa zitumwe kwako kwa barua pepe. Ukiomba nakala ya kielektroniki ya Mwongozo wetu wa Mshirika au hati nyingine zozote, kitengo cha huduma kwa wateja kitaomba ruhusa yako ili kukituma kwako kwa barua pepe. Anwani yako ya barua pepe itatumiwa tu kwa idhini yako. Pia unaweza kupigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja simu kwa 877-600-5472; TTY: 877-600-5473.

Unaweza kupata mkalimani.

Wewe, mwakilishi wako, wanafamilia na watunzaji wako wanaweza kuomba mkalimani aliyethibitishwa na mwenye sifa zinazostahili wa huduma za afya. Pia unaweza kuomba wakalimani wa maandishi au vifaa au huduma za usaidizi. Huduma hizi ni za bila malipo.

Iambie ofisi ya mtoa huduma wako ikiwa unahitaji mkalimani katika ziara yako. Waambie lugha au muundo unaohitaji. Pata habari zaidi kuhusu Wakalimani wa Huduma za Afya waliothibitishwa katika Oregon.gov/OHA/OEI.

Ikiwa unahitaji usaidizi, tafadhali tupigie simu kwa 877-600-5472; TTY: 877-600-5473 au pigia Kitengo cha Huduma za Wateja cha OHP simu kwa 800-273-0557 (TTY 711). Tazama ukurasa wa 92 kwa “Haki za lalamiko, rufaa na usikilizaji wa kesi.”

Ukikosa kupata usaidizi wa mkalimani unaohitaji, pigia mratibu wa Mpango wa Huduma za Ufikiaji wa Lugha wa jimbo kwa 844-882-7889, TTY 711 au utume barua pepe kwa: LanguageAccess.Info@odhsoha.oregon.gov.

English

You can get this letter in other languages, large print, Braille or a format you prefer. You can also ask for an interpreter. This help is free. Call 877-600-5472; or TTY: 877-600-5473. We accept relay calls.

-

You can get help from a certified and qualified health care interpreter.

Spanish

Puede obtener este documento en otros idiomas, en letra grande, braille o en un formato que usted prefiera. También puede recibir los servicios de un intérprete. Esta ayuda es gratuita. Llame al servicio de atención al cliente 877-600-5472 o TTY: 877-600-5473. Aceptamos todas las llamadas de retransmisión.

-

Usted puede obtener ayuda de un intérprete certificado y calificado en atención de salud.

Russian

Вы можете получить это письмо на другом языке, напечатанное крупным шрифтом, шрифтом Брайля или в предпочитаемом вами формате. Вы также можете запросить услуги переводчика. Эта помощь предоставляется бесплатно. Звоните по тел. 877-600-5472 или TTY: 877-600-5473. Мы принимаем звонки по линии трансляционной связи.

-

Вы можете получить помощь от аккредитованного и квалифицированного медицинского переводчика.

Vietnamese

Quý vị có thể nhận tài liệu này bằng một ngôn ngữ khác, theo định dạng chữ in lớn, chữ nổi Braille hoặc một định dạng khác theo ý muốn. Quý vị cũng có thể yêu cầu được thông dịch viên hỗ trợ. Sự trợ giúp này là miễn phí. Gọi 877-600-5472 hoặc TTY (Đường dây Dành cho Người Khiếm thính hoặc Khuyết tật về Phát âm): 877-600-5473. Chúng tôi chấp nhận các cuộc gọi chuyển tiếp.

-
Quý vị có thể nhận được sự giúp đỡ từ một thông dịch viên có chứng nhận và đủ tiêu chuẩn chuyên về chăm sóc sức khỏe.

Arabic

يمكنكم الحصول على هذا الخطاب بلغات أخرى، أو مطبوعة بخط كبير، أو مطبوعة على طريقة برايل أو حسب الصيغة المفضلة لديكم. كما يمكنكم طلب مترجم شفهي. إن هذه المساعدة مجانية. اتصلو على 877-600-5472 أو المبرقة الكاتبة 877-600-5473. نستقبل المكالمات المحولة.

-
يمكنكم الحصول على المساعدة من مترجم معتمد ومؤهل في مجال الرعاية الصحية.

Somali

Waxaad heli kartaa warqadan oo ku qoran luqaddo kale, far waaweyn, farta dadka indhaha aan qabin wax ku akhriyaan ee Braille ama qaabka aad doorbidayso. Waxaad sidoo kale codsan kartaa turjubaan.

Taageeradani waa lacag la'aan. Wac 877-600-5472 ama TTY: 877-600-5473. Waa aqbalnaa wicitaanada gudbinta.

-
Waxaad caawimaad ka heli kartaa turjubaanka daryeelka caafimaadka oo xirfad leh isla markaana la aqoonsan yahay.

Simplified Chinese

您可获取本文件的其他语言版、大字版、盲文版或您偏好的格式版本。您还可要求提供口译员服务。本帮助免费。致电 877-600-5472 或 TTY: 877-600-5473。我们会接听所有的转接来电。

-
您可以从经过认证且合格的医疗口语翻译人员那里获得帮助。

Traditional Chinese

您可獲得本信函的其他語言版本、大字版、盲文版或您偏好的格式。您也可申請口譯員。以上協助均為免費。請致電 877-600-5472 或聽障專線: 877-600-5473。我們接受所有傳譯電話。

-
您可透過經認證的合格醫療保健口譯員取得協助。

Korean

이 서신은 다른 언어, 큰 활자, 점자 또는 선호하는 형식으로 받아보실 수 있습니다. 통역사를 요청하실 수도 있습니다. 무료 지원해 드립니다. 877-600-5472 또는 TTY: 877-600-5473 에 전화하십시오. 저희는 중계 전화를 받습니다.

-
공인 및 자격을 갖춘 의료서비스 전문 통역사의 도움을 받으실 수 있습니다.

Hmong

Koj txais tau tsab ntawv no ua lwm yam lus, ua ntawv loj, ua lus Braille rau neeg dig muag los sis ua lwm yam uas koj nyiam. Koj kuj thov tau kom muaj ib tug neeg pab txhais lus. Txoj kev pab no yog ua pub dawb. Hu 877-600-5472 los sis TTY: 877-600-5473. Peb txais tej kev hu xov tooj rau neeg lag ntseg.

-
Koj yuav tau kev pab los ntawm ib tug kws txawj txhais lus rau tib neeg mob.

Marshallese

Kwomaroñ bōk leta in ilo kajin ko jet, kōn jeje ikkillep, ilo braille ak bar juon wāwein eo em̄man̄lok ippam̄. Kwomaroñ kajjitōk bwe juon ri ukōt en jipañ eok. Ejjeļok wōñāān jipañ in. Kaaltok 877-600-5472 ak TTY: 877-600-5473. Kwomaroñ kaaltok in relay.

-

Kwomaroñ bōk jipañ jān juon ri ukōt ekōmālim im keiie āinwōt ri ukōt in ājmour.

Chuukese

En mi tongeni angei ei taropwe non pwan ew fosun fenu, mese watte mak, Braille ika pwan ew format ke mwochen. En mi tongeni pwan tingor emon chon chiaku Ei aninis ese fokkun pwan kamo. Kokori 877-600-5472 ika TTY: 877-600-5473. Kich mi etiwa ekkewe keken relay.

-

En mi tongeni kopwe angei aninis seni emon mi certified ika qualified ren chon chiaku ren health care.

Tagalog

Makukuha mo ang liham na ito sa iba pang mga wika, malaking letra, Braille, o isang format na gusto mo. Maaari ka ring humingi ng tagapagsalin. Ang tulong na ito ay libre. Tawagan ang 877-600-5472 o TTY: 877-600-5473. Tumatanggap kami ng mga relay na tawag.

-

Makakakuha ka ng tulong mula sa isang sertipikado at kwalipikadong tagapagsalin ng pangangalaga sa kalusugan.

German

Sie können dieses Dokument in anderen Sprachen, in Großdruck, in Brailleschrift oder in einem von Ihnen bevorzugten Format erhalten. Sie können auch einen Dolmetscher anfordern. Diese Hilfe ist gratis. Wenden Sie sich an 877-600-5472 oder per Schreibtelefon an : 877-600-5473. Wir nehmen Relaisanrufe an.

-

Sie können die Hilfe eines zertifizierten und qualifizierten Dolmetschers für das Gesundheitswesen in Anspruch nehmen.

Portuguese

Esta carta está disponível em outros idiomas, letras grandes ou braile, se preferir. Também poderá solicitar serviços de interpretação. Essa ajuda é gratuita. Ligue para 877-600-5472 ou use o serviço TTY: 877-600-5473. Aceitamos encaminhamentos de chamadas.

-

Você poderá obter a ajuda de intérpretes credenciados e qualificados na área de saúde.

Japanese

この書類は、他の言語に翻訳されたもの、拡大文字版、点字版、その他ご希望の様式で入手可能です。また、通訳を依頼することも可能です。本サービスは無料をご利用いただけます。877-600-5472 または TTY: 877-600-5473 までお電話ください。電話リレーサービスでも構いません。

-

認定または有資格の医療通訳者から支援を受けられます。

Sera yetu ya kutobagua.

Trillium Community Health Plan sharti ifuate sheria za jimbo na shirikisho za haki za raia. Hatuwezi kuwashughulikia watu (washirika au washirika watarajiwa) bila haki katika mipango au shughuli zetu zozote kwa sababu ya:

- Umri
- Ulemavu
- Utambulisho wa kijinsia
- Hali ya ndoa
- Asili ya kitaifa
- Umbari
- Dini
- Rangi
- Jinsia
- Mwelekeo wa kimapenzi
- Hali ya afya na hitaji la huduma la mtu

Ikiwa unahisi hukutendewa haki kwa yoyote kati ya sababu zilizo hapo juu unaweza kutoa lalamiko au nung'uniko.

Toa (au wasilisha) lalamiko kwa Trillium Community Health Plan kwa yoyote kati ya njia hizi:

- Simu: 541-214-3948
- Pigia Mratibu wetu wa Manung'uniko Emily Farrell simu kwa 877-600-5472
TTY: 711
- Faksi: 844-805-3991
- Barua: Trillium Community Health Plan
PO Box 11740
Eugene, OR 97440-3940
- Barua pepe: Grievances@TrilliumCHP.com
- Wavuti: www.trilliumohp.com/members/oregon-health-plan/for-members/member-satisfaction.html

Je, unahitaji usaidizi wa kuwasilisha lalamiko? Pigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja, mtaalamu wa ustawi wa wenza, au mwelekezi wa binafsi wa afya. Pia una haki ya kuwasilisha lalamiko kwa lolote kati ya mashirika haya:

Oregon Health Authority (OHA) Civil Rights

- Simu: 844-882-7889, TTY 711
- Wavuti: www.oregon.gov/OHA/OEI
- Barua pepe: OHA.PublicCivilRights@odhsoha.oregon.gov
- Barua: Office of Equity and Inclusion Division
421 SW Oak St., Suite 750
Portland, OR 97204

Bureau of Labor and Industries Civil Rights Division

- Simu: 971-673-0764
- Wavuti: www.oregon.gov/boli/civil-rights
- Barua pepe: crdemail@boli.state.or.us
- Barua: Bureau of Labor and Industries Civil Rights Division
800 NE Oregon St., Suite 1045
Portland, OR 97232

U.S. Department of Health and Human Services Office for Civil Rights (OCR)

- Wavuti: <https://ocrportal.hhs.gov/ocr/smartscreen/main.jsf>
- Simu: 800-368-1019, TDD: 800-537-7697
- Barua pepe: OCRComplaint@hhs.gov
- Barua: Office for Civil Rights
200 Independence Ave. SW, Room 509F, HHH Bldg.
Washington, DC 20201

Tunaweka maelezo yako kwa faragha.

Tunashiriki tu rekodi zako na watu wanaohitaji kuziona. Hii inaweza kuwa kwa sababu za matibabu au malipo. Unaweza kuweka kikomo kwa anayeona rekodi zako. Tuambie kwa maandishi ikiwa hutaki mtu fulani aone rekodi zako **au** ikiwa unataka tushiriki rekodi zako na mtu fulani. Fomu hiyo inaweza kupatikana katika www.trilliumohp.com/members/oregon-health-plan/for-members/handbooks-forms.html na hutumwa kwa ProtectMyInfo@TrilliumCHP.com. Unaweza kutuomba orodha ya watu ambao tumeshiriki rekodi zako nao.

Sheria inayoitwa Health Insurance Portability and Accountability Act (Sheria ya Ubebekaji wa Bima ya Afya na Uwajibikaji, HIPAA) hulinda rekodi zako za matibabu na kuzifanya kuwa za faragha. Hili pia huitwa usiri. Tuna hati inayoitwa Notisi ya Utendaji wa Faragha inayoeleza jinsi tunavyotumia maelezo ya binafsi ya washirika wetu. Tutakutumia ukiomba. Pigia tu Kitengo cha Huduma kwa Wateja simu na uombe Notisi ya Utendaji wa Faragha. Pia unaweza kuitazama katika www.trilliumohp.com, kwa kutelezesha hadi sehemu ya chini ya ukurasa na kubofya “Notisi ya Utendaji wa Faragha”.

Rekodi za afya.

Rekodi ya afya ina matatizo yako ya afya na huduma ulizotumia. Pia inaonyesha rufaa ulizopewa.

Je, unaweza kufanyia nini rekodi za afya?

- Tuma rekodi yako kwa mtoa huduma mwingine inavyohitajika.
- Omba kurekebisha au kusahihisha rekodi zako.
- Pata nakala ya rekodi zako, ikiwa ni pamoja na, lakini si tu:
 - Rekodi za matibabu kutoka kwa mtoa huduma wako
 - Rekodi za huduma za meno kutoka kwa daktari wako wa meno
 - Rekodi kutoka kwa Trillium Community Health Plan

Kunaweza kuwa na nyakati ambapo sheria huweka kizuizi kwa ufikiaji wako. Unaweza kutozwa kiasi kinachokubalika kwa nakala ya rekodi zilizoombwa.

Rekodi fulani haziwezi kushirikiwa.

Mtoa huduma hawezi kushiriki rekodi za afya wakati, kwa maoni yake ya kitaalamu, kushiriki rekodi hizo kunaweza kusababisha hatari “dhahiri na ya mara moja” kwako, wengine, au kwa jamii. Mtoa huduma pia hawezi kushiriki rekodi zilizoandaliwa kwa kesi ya mahakamani.

Kilichomo katika mwongozo huu

Usaidizi wa bila malipo kwa lugha na miundo mingine.....	3
<i>Pata taarifa kwa lugha au muundo mwingine.....</i>	<i>3</i>
<i>Unaweza kupata mkalimani.....</i>	<i>4</i>
Sera yetu ya kutobagua.....	10
Tunaweka maelezo yako kwa faragha.....	11
Rekodi za afya.....	11
Karibu katika Trillium Community Health Plan!.....	15
Wasiliana nasi.....	16
<i>Nambari muhimu za simu.....</i>	<i>16</i>
<i>Wasiliana na Oregon Health Plan.....</i>	<i>17</i>
Haki na Majukumu Yako.....	18
<i>Haki zako kama mshirika wa OHP.....</i>	<i>18</i>
<i>Majukumu yako kama mshirika wa OHP.....</i>	<i>20</i>
Washirika ambao ni wajawazito.....	22
Washirika ambao ni Wamarekani wa Kihindi na Wazaliwa wa Alaska.....	22
Washirika wapya wanaohitaji huduma mara moja.....	23
Utafiti kuhusu afya yako.....	23
Mafao yako.....	25
<i>Jinsi Oregon huamua kile ambacho OHP italipia.....</i>	<i>25</i>
<i>Kupata idhini, kunakojulikana pia kama idhini ya awali (PA).....</i>	<i>25</i>
<i>Rufaa za mtoa huduma na rufaa za kujipatia mwenyewe.....</i>	<i>26</i>
<i>Mafao ya afya ya mwili.....</i>	<i>26</i>
<i>Mafao ya huduma za afya ya akili.....</i>	<i>32</i>
<i>Mafao ya matibabu ya matumizi ya dawa za kulevya.....</i>	<i>33</i>
<i>Mafao ya meno.....</i>	<i>34</i>
Ufikiaji kwa huduma unayohitaji.....	39
Inachukua muda gani kupata huduma.....	40
Watoa huduma wa msingi (PCPs).....	42
<i>Sajili ya watoa huduma.....</i>	<i>43</i>
<i>Panga miadi.....</i>	<i>43</i>
Pata usaidizi wa kupanga huduma zako kwa Uratibu wa Huduma.....	45
Uratibu wa Uangalizi Makini.....	47
Uchunguzi maalum na huduma za kuzuia magonjwa kwa washirika walio na umri wa chini ya miaka 21.....	49
Wafanyakazi wa Afya wa Kawaida (THW).....	51
Huduma za ziada.....	53
<i>Huduma Mbadala (ILOS).....</i>	<i>53</i>

<i>Huduma Mbadala (ILOS)</i>	53
<i>Huduma Zinazohusiana na Afya</i>	54
Usafiri wa bila malipo kwenda kupata huduma	58
Kupata huduma kwa video au simu.	62
Dawa zinazoagizwa na daktari.....	64
Huduma tusizolipia.....	66
Hospitali.	67
Huduma za matibabu ya haraka.	67
Huduma za matibabu ya dharura	71
<i>Dharura za mwili</i>	71
<i>Dharura za meno</i>	72
<i>Mgogoro na dharura za afya ya mwenendo</i>	73
<i>Huduma za ufuatiliaji baada ya dharura</i>	75
Huduma mbali na nyumbani.....	76
<i>Huduma zilizopangwa nje ya jimbo</i>	76
<i>Huduma za matibabu ya dharura mbali na nyumbani</i>	76
Bili za huduma.....	77
<i>Washirika wa OHP hawalipi bili za huduma zinazolipiwa na bima.</i>	77
<i>Kunaweza kuwa na huduma ambazo lazima ulipie.</i>	78
<i>Unaweza kuombwa kutia sahihi fomu ya Makubaliano ya Kulipa.</i>	79
<i>Vidokezo muhimu kuhusu kulipia huduma na bili.</i>	80
Wanachama walio na OHP na Medicare.	82
Kubadilisha CCOs na kuhamisha huduma.....	83
<i>Wakati ambapo unapoweza kubadilisha au kuondoka kwenye CCO.</i>	83
<i>Jinsi ya kubadilisha au kuondoka kwenye shirika lako la CCO</i>	84
<i>Trillium Community Health Plan inaweza kukuomba uondoke kwa sababu fulani.</i>	85
<i>Huduma huku ukibadilisha au kuondoka kwenye CCO</i>	86
Maamuzi ya mwisho wa maisha.....	87
<i>Maagizo ya mapema</i>	87
<i>Je, kuna tofauti gani kati ya POLST na agizo la mapema?</i>	89
<i>Tamko la Matibabu ya Afya ya Akili.</i>	90
Kuripoti Ulaghai, Ufujaji, na Matumizi Mabaya.	91
Malalamiko, Manung'uniko, Rufaa na Usikilizaji wa Haki wa Kesi	93
<i>Unaweza kutoa lalamiko</i>	93
<i>Unaweza kutuomba tubadilishe uamuzi tuliofanya.</i>	95
<i>Maswali na majibu kuhusu rufaa na usikilizaji wa kesi</i>	97
Maneno ya Kujua	100

Karibu katika Trillium Community Health Plan!

Tuna furaha kwamba wewe ni sehemu ya Trillium Community Health Plan. Trillium Community Health Plan ina furaha kusaidia kwa afya yako. Tungependa kukupatia huduma bora zaidi tunazoweza.

Ni muhimu kujua jinsi ya kutumia mpango wako. Mwongozo huu unakwambia kuhusu kampuni yetu, jinsi ya kupata huduma, na jinsi ya kunufaika zaidi kutoka kwa mafao yako.

Jinsi OHP na Trillium Community Health Plan hushirikiana

Oregon Health Plan (OHP) ni bima ya huduma za afya ya bila malipo ya Wanaoregon. OHP ni mpango wa Medicaid wa Oregon. Hulipia huduma za afya ya mwili, meno, na mwenendo (matibabu ya afya ya akili na ugonjwa wa matumizi ya dawa za kulevya). OHP pia itasaidia kwa dawa zinazoagizwa na daktari na usafiri kwenda kupata huduma.

OHP ina mipango ya afya ya maeneo husika ambayo hukusaidia kutumia mafao yako. Mipango hiyo inaitwa mashirika ya huduma zinazoratibiwa au CCOs. Trillium Community Health Plan ni CCO.

CCOs hupanga na kulipia huduma zako za afya. Tunawalipa madaktari au watoa huduma kwa njia tofauti ili kuimarisha jinsi unavyopata huduma. Hili husaidia kuhakikisha kwamba watoa huduma wanalenga kuimarisha afya yako ya jumla. Una haki ya kuuliza kuhusu jinsi tunavyowalipa watoa huduma. Malipo au marupurupu ya mtoa huduma hayatabadilisha huduma zako au jinsi unavyopata mafao. Kwa maelezo zaidi, pigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja simu kwa 877-600-5472.

Mashirika yote ya CCO hutoa mafao sawa ya OHP. Baadhi hutoa huduma za ziada kama bidhaa za mtoto mchanga aliyezaliwa tu na uanachama wa ukumbi wa mazoezi ya mwili. Pata habari zaidi kuhusu mafao ya Trillium Community Health Plan katika ukurasa wa 53.

Wasiliana nasi.

Ofisi ya Trillium Community Health Plan hufunguliwa Jumatatu hadi Ijumaa, kuanzia saa 8:00 asubuhi hadi saa 5:00 jioni.

Huwa tumefunga katika Sikukuu ya Mwaka Mpya, Sikukuu ya Martin Luther King Jr, Sikukuu ya Kumbukumbu, Sikukuu ya Uhuru, Sikukuu ya Wafanyakazi, Sikukuu ya Shukrani, Ijumaa baada ya Sikukuu ya Shukrani, Mkesha wa Krismasi, Krismasi, na Mkesha wa Mwaka Mpya.

Eneo la ofisi yetu ni:

Trillium Community Health Plan
13221 SW 68th Parkway, Ste 315
Tigard, OR 97223

Piga simu bila kutozwa ada: 877-600-5472, TTY 711, au ufikiaji wa lugha kwa 877-600-5472.
Faksi: 844-805-3991.

Mtandaoni: www.TrilliumOHP.com

Anwani ya barua: Trillium Community Health Plan
PO Box 11740
Eugene, OR 97440-3940

Nambari muhimu za simu.

- **Mafao ya matibabu na huduma**
Pigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja Simu: 877-600-5472. Watumiaji wa TTY, tafadhali piga simu kwa 711.
Saa: Jumatatu hadi Ijumaa, saa 8:00 asubuhi hadi saa 5:00 jioni.
Pata habari kuhusu mafao ya matibabu na huduma katika ukurasa wa 25.
- **Mafao ya famasia**
Kitengo cha Huduma kwa Wateja cha Famasia: 877-600-5472. Watumiaji wa TTY, piga simu kwa 711.
Saa: Jumatatu hadi Ijumaa, saa 8:00 asubuhi hadi saa 5:00 jioni.
Pata habari kuhusu mafao ya famasia katika ukurasa wa 63.
- **Mafao ya matibabu na huduma za afya ya mwenendo, dawa za kulevya, uraibu wa pombe, au ugonjwa wa matumizi ya dawa za kulevya.**
Kitengo cha Huduma kwa Wateja: 877-600-5472. Watumiaji wa TTY, tafadhali piga simu kwa 711.
Saa: Jumatatu hadi Ijumaa, saa 8:00 asubuhi hadi saa 5:00 jioni.
Pata habari kuhusu mafao ya afya ya mwenendo katika ukurasa wa 32.
- **Mafao na huduma za meno**

Advantage Dental Services

Kitengo cha Huduma kwa Wateja Bila kutozwa ada 1-866-268-9631 TTY: 711

Capitol Dental Care

Kitengo cha Huduma kwa Wateja 1-503-585-5205 au bila kutozwa ada 1-800-525-6800
TTY: 1-800-735-2900

Oregon Dental Service

Kitengo cha Huduma kwa Wateja 1-503-243-2987 au bila kutozwa ada 1-800-342-0526

- TTY: 1-503-243-3958 au 1-800-466-6313

- Usafiri wa bila malipo kwenda kupata huduma za tiba ya mwili, huduma za meno, au huduma za afya ya mwenendo

Unaweza kupata usafiri wa bila malipo kwenda kwa ziara za huduma za tiba ya mwili, huduma za meno, au huduma za afya ya mwenendo. Pigia 877-600-5472 simu ili kupanga usafiri. Watumiaji wa TTY, tafadhali pigia simu kwa 711.

Saa: Jumatatu hadi Ijumaa, saa 8:00 asubuhi hadi saa 5:00 jioni. Huwa tumefunga katika Sikukuu ya Mwaka Mpya, Sikukuu ya Martin Luther King Jr, Sikukuu ya Kumbukumbu, Sikukuu ya Uhuru, Sikukuu ya Wafanyakazi, Sikukuu ya Shukrani, Ijumaa baada ya Sikukuu ya Shukrani, Mkesha wa Krismasi, Krismasi, na Mkesha wa Mwaka Mpya.

Pata habari zaidi kuhusu usafiri kwenda kupata huduma katika ukurasa wa 58.

Wasiliana na Oregon Health Plan.

Kitengo cha Huduma kwa Wateja cha OHP kinaweza kusaidia:

- Kubadilisha anwani, nambari ya simu, hali ya familia au maelezo mengine
- Kubadilisha kadi iliyopotea ya kitambulisho cha Oregon Health
- Kupata usaidizi wa kuomba au kuwezesha mafao upya
- Kupata usaidizi ndani ya eneo husika kutoka kwa mshirika wa jamii

Jinsi ya kuwasiliana na Kitengo cha Huduma kwa Wateja cha OHP.

- Piga simu: 800-699-9075 bila kutozwa ada (TTY 711)
- Wavuti: www.OHP.Oregon.gov
- Barua pepe: Tumia tovuti salama ya barua pepe katika <https://secureemail.dhsoha.state.or.us/encrypt> kutuma barua pepe yako kwa Oregon.Benefits@odhsoha.oregon.gov.
 - Tuambie jina lako kamili, terehe ya kuzaliwa, nambari ya kitambulisho cha Oregon Health, anwani na nambari ya simu.

Haki na Majukumu Yako.

Kama mshirika wa Trillium Community Health Plan, una haki. Pia kuna majukumu au mambo ambayo unapaswa kufanya ukipata OHP. Ikiwa una maswali yoyote kuhusu haki na majukumu yaliyoorodheshwa hapa, pigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja simu kwa 877-600-5472.

Una haki ya kutumia haki zako za mshirika bila jibu baya au kubaguliwa. Unaweza kutoa lalamiko ikiwa unahisi kuwa haki zako hazijaheshimiwa. Pata habari zaidi kuhusu kutoa malalamiko katika ukurasa wa 92. Pia unaweza kupigia Mchunguzi wa Malalamiko ya Umma wa Oregon Health Authority simu kwa 877-642-0450 (TTY 711). Unaweza kumtumia barua pepe salama katika www.oregon.gov/oha/ERD/Pages/Ombuds-Program.aspx.

Kuna nyakati ambapo watu walio na umri wa chini ya miaka 18 (watoto) wanaweza kutaka au kuhitaji kupata huduma za afya wakiwa peke yao. Ili kupata habari zaidi, soma “Haki za Watoto: Ufikiaji na Idhini ya Huduma za Afya.” Kijitabu hiki hukwambia aina za huduma ambazo watoto wanaweza kupata wakiwa peke yao na jinsi rekodi zao za afya zinaweza kushirikiwa. Unaweza kukisoma katika www.OHP.Oregon.gov. Bofya katika “Haki za watoto na ufikiaji kwa huduma.” Au nenda kwenye: <https://sharedsystems.dhsoha.state.or.us/DHSForms/Served/le9541.pdf>

Haki zako kama mshirika wa OHP.

Una haki ya kushughulikiwa hivi

- Kushughulikiwa kwa hadhi, heshima na uzingatiaji wa faragha yako.
- Kushughulikiwa na watoa huduma kwa njia sawa kama watu wengine wanaotafuta huduma za afya.
- Kuwa na uhusiano thabiti na timu ya huduma inayowajibikia usimamizi wa huduma zako za jumla.
- Kutozuiliwa au kutengwa na watu kwa sababu itakuwa rahisi zaidi kukuhudumia, ili kukuadhibu, au kukufanya ufanye jambo ambalo hutaki kufanya.

Una haki ya kupata taarifa hii

- Nyenzo zinazoelezwa kwa njia na kwa lugha ambayo unaweza kuelewa. (tazama ukurasa wa 3)
- Nyenzo zinazokwambia kuhusu CCOs na jinsi ya kutumia mfumo wa huduma za afya. (Mwongozo wa Mshirika ni chanzo kizuri kwa hili)
- Nyenzo zilizoandikwa zinazokwambia haki zako, majukumu, mafao, jinsi ya kupata huduma, na unachopaswa kufanya katika dharura. (Mwongozo wa Mshirika ni chanzo kizuri kwa hili)
- Taarifa kuhusu maradhi yako, kinacholipiwa na bima, na kisicholipiwa na bima, ili uweze kufanya maamuzi mema kuhusu matibabu yako. Kupata taarifa hizi kwa lugha na muundo unaokufaa zaidi.

- Rekodi ya matibabu ambayo hufuatilia maradhi yako, huduma unazopata, na rufaa. (tazama ukurasa wa 11)
 - Kuwa na ufikiaji kwa rekodi zako za afya
 - Kushiriki rekodi zako za afya na mtoa huduma.
- Notisi iliyoandikwa ya kukataliwa au mabadiliko katika mafao kabla hilo kufanyika. Unaweza kukosa kupata notisi ikiwa hilo halihitajiki kwa kanuni za shirikisho au jimbo.
- Notisi iliyoandikwa kuhusu watoa huduma ambao si wa ndani ya mtandao tena.
- Kuambiwa kwa wakati unaofaa ikiwa miadi imebatilishwa.

Una haki ya kupata huduma hizi

- Matibabu na huduma zinazokupatia kipaumbele. Kupata huduma ambazo hukupatia uwezo wa kuchagua, uhuru na hadhi. Huduma hizi zitalingana na mahitaji yako ya afya na kutimiza viwango vya utendaji.
- Huduma ambazo huzingatia mahitaji yako ya kitamaduni na lugha na zilizo karibu na unakoishi. Ikiwa yanapatikana, unaweza kupata huduma katika mazingira yasiyo ya kawaida (Tazama ukurasa wa 51).
- Uratibu wa huduma, huduma katika jamii, na usaidizi wa mabadiliko ya huduma kwa njia inayofaa kwa utamaduni na lugha yako. Hili litasaidia kukufanya usilazwe hospitalini au katika katuo.
- Huduma zinazohitajika ili kujua tatizo la afya ulilo nalo.
- Usaidizi wa kutumia mfumo wa huduma za afya. Kupata usaidizi wa kitamaduni na lugha unaohitaji. (Tazama ukurasa wa 52). Hii inaweza kuwa:
 - Wakalimani waliothibitishwa au wenye sifa zinazostahili wa huduma za afya.
 - Wafanyakazi wa afya wa kawaida waliothibitishwa.
 - Wafanyakazi wa afya ya jamii.
 - Wataalamu wa ustawi wa wenza.
 - Wataalamu wa usaidizi wa wenza.
 - Doula.
 - Waelekezi wa binafsi wa afya.
- Usaidizi kutoka kwa wafanyakazi wa CCO ambao wamepokea mafunzo kamili kuhusu sera na taratibu za CCO.
- Huduma za kuzuia magonjwa zinazolipiwa na bima. (Tazama ukurasa wa 25).
- Huduma za haraka na dharura kwa saa 24 kwa siku, siku 7 kwa wiki bila idhini au rufaa. (tazama ukurasa wa 66).
- Rufaa kwa watoa huduma wataalamu kwa huduma zinazoratibiwa zinazolipiwa na bima ambazo zinahitajika kulingana na afya yako. (tazama ukurasa wa 25).

Una haki ya kufanya mambo haya

- Kuchagua watoa huduma wako na kubadilisha uteuzi huo. (tazama ukurasa wa 42)
- Kuandamana na rafiki, mwanafamilia au msaidizi kwenda kwenye miadi yako.
- Kuhusishwa kikamilifu katika kubuni mpango wako wa matibabu.
- Kukubali au kukataa huduma. Kujua kinachoweza kufanyika kulingana na uamuzi wako. Huduma iliyoagizwa na mahakama haiwezi kukataliwa.
- Kutafuta mwenyewe huduma za afya ya mwenendo au kupanga uzazi bila ruhusa kutoka kwa mtoa huduma.
- Kutoa taarifa ya matakwa yako ya matibabu. Hii inamaanisha matakwa yako ya kukubali au kukataa matibabu, tiba ya upasuaji, au matibabu ya afya ya mwenendo. Inamaanisha pia haki ya kutoa maagizo na kutoa mamlaka ya usimamizi wa huduma za afya, ambayo yameorodheshwa katika ORS 127. (Tazama ukurasa wa 86).
- Kutoa lalamiko au kuomba rufaa. Kupata jibu kutoka Trillium Community Health Plan unapofanya hivi. (tazama ukurasa wa 92)
 - Kuomba jimbo kufanya ukaguzi ikiwa hukubali uamuzi wa Trillium Community Health Plan. Huu unaitwa usikilizaji wa kesi.
- Kupata wakalimani waliothibitishwa au wenye sifa zinazostahili wa huduma za afya bila malipo kwa lugha zote zisizo Kiingereza na lugha ya ishara (tazama ukurasa wa 4).

Majukumu yako kama mshirika wa OHP.

Lazima uwafanyie wengine hivi

- Kuwatendea wafanyakazi wa Trillium Community Health Plan, watoa huduma na wengine kwa heshima.
- Kuwaambia watoa huduma wako ukweli ili waweze kukupatia huduma bora zaidi.

Lazima uiambie OHP taarifa hii

Pigia OHP simu kwa 800-699-9075 (TTY 711):

- Unapohama au kubadilisha anwani yako ya barua.
- Ikiwa mwanafamilia yeyote atahamia nyumbani kwako au kuhama kutoka nyumbani kwako.
- Unapobadilisha nambari yako ya simu.
- Unapokuwa mjamzito na unapojifungua.
- Unapokuwa na bima nyingine.

Lazima usaidie kwa huduma zako kwa njia hizi

- Chagua au usaidie kuchagua mtoa huduma wako wa msingi au kliniki.
- Pata uchunguzi wa kila mwaka, ziara za afya, na huduma za kuzuia magonjwa ili kukufanya uendelee kuwa na afya njema.
- Fika katika miadi kwa wakati unaofaa. Ikiwa utachelewa, piga simu mapema au batilisha miadi yako ikiwa huwezi kuhudhuria.
- Leta kadi zako za kitambulisho cha matibabu kwenye miadi. Iambie ofisi kwamba una OHP na bima nyingine yoyote ya afya. Wajulishe ikiwa uliumizwa kwenye ajali.
- Msaidie mtoa huduma wako kubuni mpango wako wa matibabu. Fuata mpango huo wa matibabu na ushiriki vikamilifu katika huduma zako.
- Fuata maagizo kutoka kwa watoa huduma wako au uombe chaguo jingine.
- Ikiwa huelewi, uliza maswali kuhusu maradhi, matibabu, na maswala mengine yanayohusiana na huduma.
- Tumia taarifa unayopata kutoka kwa watoa huduma na timu za huduma kukusaidia kufanya maamuzi ya busara kuhusu matibabu yako.
- Tumia mtoa huduma wako wa msingi kwa kipimo na mahitaji mengine ya huduma, isipokuwa ikiwa ni dharura.
- Tumia wataalamu wa ndani ya mtandao au ushirikiane na mtoa huduma wako kwa idhini ikiwa unataka au unahitaji kuhudumiwa na mtu asiyeshirikiana na Trillium Community Health Plan.
- Tumia huduma za haraka au za dharura kwa njia inayofaa. Mwambie mtoa huduma wako wa msingi ndani ya saa 72 ikiwa utatumia huduma hizi.
- Wasaidie watoa huduma kupata rekodi yako ya afya. Unaweza kulazimika kutia fomu sahihi kwa hili.
- Ambia Trillium Community Health Plan ikiwa una matatizo yoyote, malalamiko, au unahitaji usaidizi.
- Lipia huduma zisizolipiwa na OHP.
- Ukipata pesa kwa sababu ya jeraha, isaidie Trillium Community Health Plan kulipwa kwa huduma tulizokupatia kwa sababu ya jeraha hilo.

Washirika ambao ni wajawazito

Ikiwa wewe ni mjamzito, OHP hutoa huduma za ziada ili kusaidia kukufanya wewe na mtoto wako kuwa na afya njema. Wakati ambapo wewe ni mjamzito, Trillium Community Health Plan inaweza kukusaidia kupata huduma unazohitaji. Pia inaweza kulipia kujifungua kwako na huduma zako kwa mwaka mmoja baada ya ujauzito wako.

Hapa ni unachohitaji kufanya kabla ya kujifungua:

- Iambie OHP kwamba wewe ni mjamzito punde tu baada ya kujua.** Piga simu kwa 800-699-9075 (TTY 711) au uingie kwenye akaunti yako ya mtandaoni katika ONE.Oregon.gov.
- Iambie OHP tarehe yako ya kujifungua.** Si lazima ujue tarehe mahususi sasa hivi. Ikiwa uko tayari kujifungua, tupigie simu mara moja.
- Tuulize kuhusu mafao yako ya ujauzito.** Start Smart For Your Baby (SSFB®) ni mpango wa washirika wajawazito na wazazi wapya. Mpango huu hukusaidia kupata huduma unazohitaji kwa ujauzito wenye afya njema. Unaweza kupata tuzo kwa kuhudhuria miadi yako na kushirikiana na timu yako ya Usimamizi wa Huduma ya SSFB. Pia tunaweza kukuunganisha na Huduma za Doula za ndani ya mtandao. Tupigie simu kwa 877-600-5472 ili kupata habari zaidi.

Baada ya kujifungua:

- Pigia OHP simu au uombe hospitali kutuma taarifa ya mtoto aliyezaliwa kwa OHP.** OHP italipia huduma za mtoto wako kuanzia anapozaliwa. Mtoto wako pia atakuwa na Trillium Community Health Plan.

Washirika ambao ni Wamarekani wa Kihindi na Wazaliwa wa Alaska.

Wamarekani wa Kihindi na Wazaliwa wa Alaska wana haki ya kuchagua mahali wanakopata huduma. Wanaweza kutumia watoa huduma ambao si sehemu ya shirika letu la CCO, kama:

- Vituo vya afya vya kikabila.
- Kliniki za Indian Health Services (IHS).
- Native American Rehabilitation Association of the Northwest (NARA).

Wamarekani wa Kihindi na Wazaliwa wa Alaska hawahitaji rufaa au ruhusa ili kupata huduma kutoka kwa watoa huduma hawa. Watoa huduma hawa lazima watoze Trillium Community Health Plan bili. Tutalipia tu mafao yanayolipiwa na bima. Ikiwa huduma inahitaji idhini, mtoa huduma lazima aiombe kwanza.

Wamarekani wa Kihindi na Wazaliwa wa Alaska wana haki ya kuondoka kwenye Trillium Community Health Plan wakati wowote na huduma zao zilipiwe na OHP Fee-For-Service (FFS). Pata habari zaidi kuhusu kuondoka au kubadilisha shirika lako la CCO katika ukurasa wa 82.

Washirika wapya wanaohitaji huduma mara moja.

Washirika ambao ni wageni kwa OHP au Trillium Community Health Plan wanaweza kuhitaji dawa zilizoagizwa na daktari, vifaa au vitu au huduma nyingine haraka iwezekanavyo. Ikiwa huwezi kuhudumiwa na mtoa huduma wako wa msingi (PCP) ndani ya siku zako 30 za kwanza katika Trillium Community Health Plan:

- Pigia Kitengo cha Uratibu wa Huduma simu kwa 877-600-5472. Wanaweza kukusaidia kupata huduma unazohitaji. (Tazama ukurasa wa 45 kwa Uratibu wa Huduma)
- Panga miadi na PCP wako haraka uwezavyo. Unaweza kupata jina na nambari yake katika kadi yako ya kitambulisho cha Trillium Community Health Plan.
- Pigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja simu kwa 877-600-5472 ikiwa una maswali na unataka kupata habari kuhusu mafao yako. Wanaweza kukusaidia kwa unachohitaji.

Utafiti kuhusu afya yako.

Trillium Community Health Plan itajaribu kuwasiliana na washirika wapya kwa simu ili kupitia mafao yako na kufanya utafiti kuhusu afya yao ndani ya siku 90. Utafiti huu unaitwa Uchunguzi wa Hatari ya Afya.

Uchunguzi wa Hatari ya Afya ni utafiti ulio na maswali kuhusu afya yako ya jumla kwa lengo la kusaidia kupunguza hatari za afya, kudumisha afya, na kuzuia ugonjwa.

Utafiti huo huuliza kuhusu:

- Mazoea yako (kama mazoezi, mazoea ya kula, na ikiwa unavuta sigara au kunywa pombe).
- Jinsi unavyohisi (ili kuona ikiwa una mfadhaiko au unahitaji mtoa huduma wa afya ya akili).
- Ustawi wako wa jumla na historia ya matibabu.
- Lugha yako ya msingi.

Majibu yako hutusaidia kugundua:

- Ikiwa unahitaji tathmini zozote za afya, ikiwa ni pamoja na tathmini za macho au meno.
- Ikiwa una mahitaji ya kawaida au maalum ya huduma za afya.
- Maradhi yako sugu.
- Ikiwa unahitaji huduma na usaidizi wa matibabu ya muda mrefu.
- Matatizo ya usalama.
- Matatizo unayoweza kuwa nayo kuhusu kupata huduma.
- Ikiwa unahitaji usaidizi wa ziada kutoka kwa uratibu wa huduma au uratibu wa uangalizi makini. Tazama ukurasa wa 45 kwa uratibu wa huduma au uratibu wa uangalizi makini.

Mshirika wa timu ya Usimamizi wa Huduma (Muuguzi, Mfanyakazi wa Kijamii wa Tiba Aliye na Leseni, Mratibu wa Usaidizi wa Tiba, au Mfamasia) atapitia utafiti wako. Atakupigia simu ili kuzungumza kuhusu mahitaji yako na kukusaidia kuelewa mafao yako.

Utatumiwa utafiti mpya kila mwaka au ikiwa afya yako itabadilika.

Tukikosa kupata utafiti wako, tutawasiliana nawe ili kusaidia kuhakikisha kwamba umejazwa. Ikiwa unataka tukutumie utafiti unaweza kupigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja cha Trillium Community Health Plan simu kwa 877-600-5472, na tutakutumia.

Utafiti wako unaweza kushirikiwa na daktari wako au watoa huduma wengine. Trillium Community Health Plan itaomba ruhusa yako kabla ya kushiriki utafiti wako na watoa huduma.

Uzuiaji ni Muhimu

Tunataka kuzuia matatizo ya afya kabla hayajafanyika. Unaweza kufanya hili kuwa sehemu muhimu ya huduma zako. Tafadhali pata uchunguzi wa mara kwa mara wa afya na meno ili kujua kinachofanyikia afya yako.

Baadhi ya mifano ya huduma za kuzuia magonjwa:

- Chanjo za watoto na watu wazima
- Uchunguzi na usafishaji wa meno
- Mamogramu (eksirei za matiti) za wanawake
- Huduma za ujauzito na mtoto mchanga aliyezaliwa
- Tathmini za wanawake za kila mwaka
- Uchunguzi wa tezi kibofu kwa wanaume
- Uchunguzi wa kila mwaka
- Tathmini za ukuaji na maendeleo ya mtoto

Kinywa chenye afya njema pia hufanya moyo na mwili wako kuwa na afya njema zaidi.

Ikiwa una maswali yoyote, tafadhali tupigie simu kwa 877-600-5472, au TTY: 877-600-5473.

Mafao yako.

Jinsi Oregon huamua kile ambacho OHP italipia.

Huduma nyingi zinapatikana kwako kama mshirika wa OHP. Jinsi Oregon huamua huduma za kulipia hulingana na **Orodha Yenye Vipambebele ya Huduma za Afya**. Orodha hii inajumuisha maradhi tofauti (yanayoitwa matatizo ya afya yaliyotambuliwa) na aina za taratibu ambazo hutibu maradhi hayo. Kikundi cha wataalamu wa tiba na raia wa kawaida hushirikiana kuunda orodha hiyo. Kikundi hiki kinaitwa Tume ya Kukagua Ushahidi wa Afya ya Oregon (HERC). Huteuliwa na gavana.

Orodha hiyo ina michanganyiko ya maradhi yote na matibabu yake. Hii huitwa jozi za maradhi/matibabu.

Jozi za maradhi/matibabu hupangwa kwa madaraja katika orodha hiyo kulingana na ukali wa kila maradhi na jinsi kila matibabu yalivyo na ufanisi. Si jozi zote za maradhi na matibabu hulipiwa na OHP. Kuna sehemu ya kikomo kwenye orodha hiyo inayoitwa "mstari." Jozi zilizo juu ya mstari hulipiwa na bima na jozi zilizo chini ya mstari hazilipiwi na bima. Baadhi ya maradhi na matibabu yaliyo juu ya mstari yana kanuni fulani.

Pata habari zaidi kuhusu Orodha Yenye Vipambebele katika:

www.oregon.gov/oha/hsd/ohp/pages/prioritized-list.aspx

Kupata idhini, kunakojulikana pia kama idhini ya awali (PA).

Baadhi ya huduma huhitaji idhini kabla ya kupata huduma hiyo. Hii inajulikana kama "idhini ya awali (PA)" au "idhini ya mapema". Mtoa huduma wako hushirikiana na Trillium Community Health Plan kuomba idhini ya mapema ya huduma. Ikiwa una maswali yoyote kuhusu idhini ya mapema ya huduma, wasiliana na Kitengo cha Huduma kwa Wateja cha Trillium Community Health Plan kwa 877-600-5472.

Huenda usipate huduma hiyo ikiwa haijaidhinishwa. Tunapitia maombi ya PA haraka kadiri hali yako ya afya inavyohitaji. Maamuzi mengi hufanywa ndani ya siku 14. Wakati mwingine, uamuzi unaweza kuchukua hadi siku 28. Hili hufanyika tu wakati ambapo tunasubiri maelezo zaidi. Ikiwa wewe au mtoa huduma wako anahisi kufuata kipindi cha kawaida cha wakati kunaweka maisha yako, afya au uwezo wako wa kutenda shughuli hatarini, tunaweza kufanya uamuzi wa "uidhinishaji ulioharakishwa wa huduma". Maamuzi yaliyoharakishwa ya huduma kwa kawaida hufanywa ndani ya saa 72, lakini kunaweza kuwa na kurefushwa kwa muda kwa siku 14. Una haki ya kulalamika ikiwa hukubaliani na uamuzi wa kurefusha muda. Tazama ukurasa wa 92 ili kupata habari kuhusu jinsi ya kuwasilisha lalamiko.

Huhitaji idhini kwa huduma za dharura au za haraka au huduma za matibabu ya baada ya dharura. Tazama ukurasa wa 70 ili kupata habari kuhusu huduma za dharura.

Rufaa za mtoa huduma na rufaa za kujipatia mwenyewe.

Ili kupata baadhi ya huduma, utahitaji kuwa na rufaa kutoka kwa mtoa huduma wako wa msingi (PCP). **Rufaa** ni agizo lililoandikwa kutoka kwa mtoa huduma wako linaloeleza hitaji la huduma.

Ikiwa PCP wako hawezi kukupatia huduma unazohitaji, anaweza kukupatia rufaa kwa mtaalamu. Ikiwa hakuna mtaalamu karibu na unakoishi au anayeshirikiana na Trillium Community Health Plan (anayejulikana pia kama wa ndani ya mtandao), anaweza kulazimika kushirikiana na timu ya Uratibu wa Huduma ili kukutafutia huduma nje ya mtandao. Hakuna gharama ya ziada ikiwa hili litafanyika.

Wakati mwingi PCP wako anaweza kutoa huduma unazohitaji. Ikiwa unafikiri unaweza kuhitaji rufaa kwa mtaalamu wa huduma za afya, muulize PCP wako. Huhitaji rufaa ikiwa unakumbwa na dharura na huwezi kuwasiliana na PCP wako. Baadhi ya huduma hazihitaji rufaa kutoka kwa mtoa huduma wako. Hii inaitwa kujipatia rufaa mwenyewe. **Kujipatia rufaa mwenyewe** kunamaanisha unaweza kutazama sajili ya watoa huduma ili kutafuta aina ya mtoa huduma ambaye ungependa kutembelea. Unaweza kumpigia mtoa huduma huyo simu ili kupanga ziara bila rufaa kutoka kwa mtoa huduma wako. Pata habari zaidi kuhusu Sajili ya Watoa Huduma katika ukurasa wa 42.

Iwe unaweza kujipatia rufaa mwenyewe au unahitaji rufaa ili kutembelea mtaalamu, bado unaweza kuhitaji idhini ya mapema kwa huduma hiyo. Zungumza na PCP wako au uwasiliane na Kitengo cha Huduma kwa Wateja ikiwa una maswali kuhusu ikiwa unahitaji idhini ya mapema ili kupata huduma.

Ufikiaji wa Moja kwa Moja.

Una “ufikiaji wa moja kwa moja” kwa watoa huduma wakati ambapo huhitaji rufaa au idhini ya mapema kwa huduma. Daima una ufikiaji wa moja kwa moja kwa huduma za dharura na za haraka. Tazama chati zilizo hapa chini kwa huduma ambazo ni za ufikiaji wa moja kwa moja na zisizohitaji rufaa au idhini ya mapema.

Mafao ya afya ya mwili.

Tazama hapa chini kwa orodha ya mafao ya matibabu yanayopatikana kwako bila gharama. Tazama safuwima ya “Kiasi, muda na upeo” ili kuona ni mara ngapi unaweza kupata kila huduma bila malipo. Trillium Community Health Plan itaratibu huduma bila malipo ikiwa unahitaji usaidizi.

Huduma	Kiasi, muda, na upeo wa mafao	Je, rufaa au idhini ya mapema inahitajika?
Tiba vitobo	Ziara 8 kwa kila mwaka wa kalenda bila uidhinishaji.	Uidhinishaji unahitajika baada ya ziara 8. Rufaa haihitajiki.
Huduma za Uratibu wa Huduma	Hakuna kikomo wakati inahitajika kimatibabu	Haihitajiki

Huduma	Kiasi, muda, na upeo wa mafao	Je, rufaa au idhini ya mapema inahitajika?
Huduma za Usimamizi wa Kesi	Hakuna kikomo wakati inahitajika kimatibabu	Haihitajiki
Tabibu maungo	Ziara 8 kwa kila mwaka wa kalenda bila uidhinishaji.	Udhinishaji unahitajika baada ya ziara 8. Rufaa haihitajiki.
Huduma za Kutuliza Maumivu na za Wagonjwa Mahututi	Hakuna kikomo wakati inahitajika kimatibabu	Haihitajiki
Vifaa vya Kudumu vya Tiba Baadhi ya mifano ni: Vifaa vya tiba (ikiwa ni pamoja na vifaa vya kisukari), vyombo vya tiba, viungo bandia na vifaa vya orthotiki	Hakuna kikomo wakati inahitajika kimatibabu	Udhinishaji unahitajika. Rufaa haihitajiki.
Huduma za Uchunguzi wa Mapema na Mara kwa Mara, Utambuzi wa Magonjwa na Matibabu (EPSDT).	Hakuna kikomo wakati inahitajika kimatibabu	Rufaa inahitajika
Usafirishaji wa matibabu ya dharura	Hakuna kikomo wakati inahitajika kimatibabu	Haihitajiki
Huduma za Dharura	Hakuna kikomo wakati inahitajika kimatibabu	Ufikiaji wa moja kwa moja (Hakuna rufaa au idhini inayohitajika)
Huduma za Kupanga Uzazi Baadhi ya mifano ni: kingamimba na tathmini za kila mwaka.	Hakuna Kikomo	Ufikiaji wa moja kwa moja (Hakuna rufaa au idhini inayohitajika).
Uchunguzi wa Hatari ya Afya kwa Uratibu wa Uangalizi Makini	Hakuna Kikomo	Hakuna rufaa inahitajika. Inaweza kuhitaji idhini ya mapema.
Huduma za Masikio Baadhi ya mifano ni: Tiba ya Uwezo wa Kusikia na Vifaa vya Usaidizi wa Kusikia	Vikomo kulingana na miongozo ya OHP. Pigia Trillium simu kwa maelezo.	Udhinishaji unahitajika
Huduma za Afya ya Nyumbani	Vikomo kulingana na miongozo ya OHP. Pigia Trillium simu kwa maelezo.	Udhinishaji unahitajika

Huduma	Kiasi, muda, na upeo wa mafao	Je, rufaa au idhini ya mapema inahitajika?
Huduma za Kulazwa Hospitalini	Hakuna kikomo wakati inahitajika kimatibabu	Hakuna rufaa inahitajika. Inaweza kuhitaji idhini ya mapema.
Huduma za Uratibu wa Uangalizi Makini (ICC)	Hakuna kikomo	Ufikiaji wa moja kwa moja (Hakuna rufaa au idhini inayohitajika).
Huduma za Mkalimani	Hakuna kikomo. Tazama Ukurasa wa 4 kwa maelezo zaidi	Haihitajiki
Huduma za Maabara:		
Kutolewa damu	Hakuna kikomo	Rufaa inahitajika. Uidhinishaji hauhitajiki
Eksirei	Hakuna kikomo	Rufaa inahitajika. Uidhinishaji hauhitajiki
Picha za viungo vya ndani za CT	Hakuna kikomo	Uidhinishaji unahitajika. Rufaa haihitajiki
Picha za viungo vya ndani za MRI	Hakuna kikomo	Uidhinishaji unahitajika. Rufaa haihitajiki
Huduma za Uzazi:		
Ziara za kabla ya kujifungua kwa mtoa huduma wako	Hakuna kikomo	Haihitajiki
Huduma za Baada ya Kujifungua (huduma unazopata baada ya mtoto wako kuzaliwa)	Hakuna kikomo	Haihitajiki
Huduma za macho za mara kwa mara	Zinapatikana kwa washirika wajawazito na watoto walio na umri wa miaka 20 na michache	Haihitajiki
Usaidizi wa kunyonyesha, ikiwa ni pamoja na pampu za matiti	Wasiliana na Trillium kwa maelezo zaidi	Haihitajiki
Uchungu wa Uzazi na Kujifungua	Tafadhali ijulishe Trillium na Oregon Health Authority	Haihitajiki

Huduma	Kiasi, muda, na upeo wa mafao	Je, rufaa au idhini ya mapema inahitajika?
	unapokuwa mjamzito au mimba yako ikiharibika. Utahitaji kutuma ombi la OHP kwa ajili ya mtoto wako. Kujifungua ukiwa nyumbani hakulipiwi na Trillium lakini hulipiwa na OHA.	
Usafiri kwenda kupata huduma. Pia unaoitwa huduma za Usafirishaji wa Matibabu Yasiyo ya Dharura (NEMT)	Hakuna kikomo wakati inahitajika kimatibabu	Haihitajiki
Huduma za Hospitali Bila Kulazwa Baadhi ya mifano ni: Tibakemikali, Tibamiali, na Udhibiti wa Maumivu	Hakuna kikomo wakati inahitajika kimatibabu	Haihitajiki
Huduma za Dawa (Dawa Zinazoagizwa na Daktari)	Dawa nyingi japo si zote zinapatikana unapokuwa na agizo la mtoa huduma. Orodha kamili inaweza kupatikana katika orodha yetu ya dawa zinazopendelewa ya Oregon Health Plan.	Hakuna gharama kwa dawa zinazolipiwa na bima. Dawa za afya ya akili husimamiwa na jimbo. Malipo ya mshiriki ya dawa hizo hutofautiana. Baadhi ya dawa zinaweza kuhitaji uidhinishaji pamoja na agizo la daktari
Wataalamu wa Afya ya Mwili kwa wale walio na mahitaji maalum ya huduma za afya wanaopokea huduma za ICC na LTSS.	Idhini kulingana na miongozo ya OHP. Pigia Trillium simu kwa maelezo	Ufikiaji wa moja kwa moja (Hakuna rufaa au idhini inayohitajika).
Tiba ya Mwili Tiba ya Kazi Tiba ya Matatizo ya Kunena	Ziara 30 kwa kila mwaka wa bila Uidhinishaji	Rufaa inahitajika. Uidhinishaji unahitajika baada ya ziara 30.
Dawa Zinazoagizwa na Daktari	Dawa nyingi japo si zote zinapatikana unapokuwa na agizo la mtoa huduma. Orodha	Hakuna gharama kwa dawa zinazolipiwa na bima. Dawa za afya ya akili husimamiwa na

Huduma	Kiasi, muda, na upeo wa mafao	Je, rufaa au idhini ya mapema inahitajika?
	kamili inaweza kupatikana katika orodha yetu ya dawa zinazopendelewa ya Oregon Health Plan.	jimbo. Malipo ya mshiriki ya dawa hizo hutofautiana. Baadhi ya dawa zinaweza kuhitaji uidhinishaji pamoja na agizo la daktari
Huduma za kuzuia magonjwa. Baadhi ya mifano ni: tathmini za mwili, uchunguzi wa ukuaji na maendeleo ya mtoto, chanjo, afya ya wanawake (mamogramu, tathmini ya kijinakolojia, nk.), uchunguzi (saratani, nk.), uzuiaji wa kisukari, ushauri wa lishe, huduma za kuacha kutumia tumbaku, nk.	Kama inavyopendekezwa	Haihitajiki
Ziara za Mtoa Huduma wa Msingi	Hakuna kikomo wakati inahitajika kimatibabu	Ufikiaji wa moja kwa moja (Hakuna rufaa au idhini inayohitajika).
Tathmini za Unyanyasaji wa Kingono	Hakuna kikomo wakati inahitajika kimatibabu	Ufikiaji wa moja kwa moja (Hakuna rufaa au idhini inayohitajika).
Huduma za Mtaalamu	Kama inavyopendekezwa	Kwa wale walio na mahitaji maalum ya huduma za afya wanaopokea ICC au LTSS: Hakuna rufaa inayohitajika. Inaweza kuhitaji idhini ya mapema.
Taratibu za upasuaji	Hakuna kikomo wakati inahitajika kimatibabu	Uidhinishaji unahitajika
Huduma za Afya kwa Vifaa vya Mawasiliano Baadhi ya mifano ni: Huduma za tiba kwa vifaa vya mawasiliano, Ziara za mtandaoni, na Ziara za barua pepe	Hakuna kikomo wakati inahitajika kimatibabu	Haihitajiki

Huduma	Kiasi, muda, na upeo wa mafao	Je, rufaa au idhini ya mapema inahitajika?
Huduma za Mfanyakazi wa Afya wa Kawaida (THW)	Hakuna kikomo	Hakuna rufaa inayohitajika. Inaweza kuhitaji idhini ya mapema.
Huduma za Tiba ya Haraka	Hakuna kikomo wakati inahitajika kimatibabu	Ufikiaji wa moja kwa moja (Hakuna rufaa au idhini inayohitajika)
Huduma za Macho:		
Tathmini za macho	Zinapatikana kwa washirika wajawazito na watoto walio na umri wa miaka 20 na michache	Rufaa inahitajika. Uidhinishaji hauhitajiki.
Miwani	Zinapatikana kwa washirika wajawazito na watoto walio na umri wa miaka 20 na michache	Rufaa inahitajika. Uidhinishaji hauhitajiki.
Tathmini ya macho ya kimatibabu	Idadi ya ziara kulingana na idhini ya mpango	Rufaa inahitajika. Uidhinishaji hauhitajiki.
Huduma za Afya ya Wanawake (pamoja na PCP) kwa huduma za kawaida na za kuzuia magonjwa.	Kama inavyopendekezwa	Ufikiaji wa moja kwa moja (Hakuna rufaa au idhini inayohitajika)
Huduma Zilizobinafsishwa za Mtoto na Familia Yake	Kama inavyopendekezwa	Ufikiaji wa moja kwa moja (Hakuna rufaa au idhini inayohitajika)

Jedwali lililo hapa juu si orodha kamili ya huduma zinazohitaji idhini ya mapema. Ikiwa una maswali kuhusu idhini za mapema, tafadhali pigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja cha Trillium Community Health Plan simu kwa 877-600-5472.

Mafao ya huduma za afya ya akili.

Tazama hapa chini kwa orodha ya mafao ya afya ya mwenendo yanayopatikana kwako bila malipo. Tazama safuwima ya “Kiasi, muda na upeo” ili kuona ni mara ngapi unaweza kupata kila huduma bila malipo. Trillium Community Health Plan itaratibu huduma bila malipo ikiwa unahitaji usaidizi.

Huduma	Kiasi, muda, na upeo wa mafao	Je, rufaa au idhini ya mapema inahitajika?
Matibabu Thabiti ya Jamii (ACT)	Hakuna kikomo	Rufaa inahitajika. Uidhinishaji hauhitajiki.
Matibabu ya Uangalizi Makini ya Nyumbani ya Afya ya Mwenendo (IIBHT)	Hakuna Kikomo	Rufaa inahitajika. Uidhinishaji hauhitajiki.
Huduma za Ukadiriaji na Tathmini ya Afya ya Mwenendo	Hakuna kikomo	Rufaa inahitajika. Uidhinishaji hauhitajiki.
Huduma za Matibabu ya Afya ya Mwenendo Katika Makazi ya Tiba ya Magonjwa ya Akili (PRTS)	Vikomo kulingana na miongozo ya OHP. Pigia Trillium simu kwa maelezo	Uidhinishaji unahitajika. Rufaa haihitajiki.
Huduma za afya ya mwenendo zisizo za kulazwa hospitalini na zinazotolewa na wenza kutoka kwa mtoa huduma wa ndani ya mtandao	Hakuna kikomo	Ufikiaji wa moja kwa moja (Hakuna rufaa au idhini inayohitajika)
Dawa Zinazoagizwa na Daktari (Mahususi kwa Afya ya Mwenendo)	Hakuna kikomo	Hakuna gharama kwa dawa zinazolipiwa na bima. Dawa za afya ya akili husimamiwa na jimbo. Malipo ya mshiriki ya dawa hizo hutofautiana.
Huduma za Mtaalamu	Vikomo kulingana na miongozo ya OHP. Pigia Trillium simu kwa maelezo	Kwa wale walio na mahitaji maalum ya huduma za afya wanaopokea ICC au LTSS: Hakuna rufaa inayohitajika. Inaweza kuhitaji idhini ya mapema.

Jedwali lililo hapa juu si orodha kamili ya huduma zinazohitaji idhini ya mapema. Ikiwa una maswali kuhusu idhini za mapema, tafadhali pigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja cha Trillium Community Health Plan simu kwa 877-600-5472.

Mafao ya matibabu ya matumizi ya dawa za kulevya.

Tazama hapa chini kwa orodha ya mafao ya matibabu ya matumizi ya dawa za kulevya yanayopatikana kwako bila malipo. Tazama safuwima ya “Kiasi, muda na upeo” ili kuona ni mara ngapi unaweza kupata kila huduma bila malipo. Trillium Community Health Plan itaratibu huduma bila malipo ikiwa unahitaji usaidizi.

Huduma	Kiasi, muda, na upeo wa mafao	Je, rufaa au idhini ya mapema inahitajika?
Thabiti za Matibabu ya Jamii	Hakuna kikomo	Rufaa inahitajika. Hakuna Uidhinishaji unaohitajika.
Huduma za Kulazwa Katika Makazi ya Tiba kwa Ugonjwa wa Matumizi ya Dawa za Kulevya na Kuacha Kutumia Dawa za Kulevya	Vikomo kulingana na miongozo ya OHP. Pigia Trillium simu kwa maelezo	Uidhinishaji unahitajika. Hakuna rufaa inahitajika.
Matibabu Yanayosaidiwa na Dawa (MAT) ya Ugonjwa wa Matumizi ya Dawa za Kulevya (SUD)	Idhini ya awali inahitajika baada ya siku 30 za kwanza	Hakuna idhini ya mapema inayohitajika kwa siku 30 za kwanza za matibabu. Zinaweza kuhitaji rufaa.
Huduma za Kutolazwa Hospitalini za Ugonjwa wa Matumizi ya Dawa za Kulevya (SUD)	Hakuna kikomo	Ufikiaji wa moja kwa moja (Hakuna rufaa au idhini inayohitajika)

Jedwali lililo hapa juu si orodha kamili ya huduma zinazohitaji idhini ya mapema. Ikiwa una maswali kuhusu idhini za mapema, tafadhali pigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja cha Trillium Community Health Plan simu kwa 877-600-5472.

Mafao ya meno.

Washirika wote wa Oregon Health Plan wana bima ya meno. OHP hulipia usafishaji wa kila mwaka, eksirei, vijazo, na huduma nyingine zinazofanya meno yako kuwa na afya njema.

Meno yenye afya njema ni muhimu kwa umri wowote. Hapa ni baadhi ya ukweli muhimu kuhusu huduma za meno:

- Meno yenye afya njema hufanya moyo na mwili wako kuwa na afya njema, pia.
- Unapaswa kutembelea daktari wako wa meno mara moja kwa mwaka.
- Wakati ambapo wewe ni mjamzito, kudumisha afya njema ya meno na fizi zako kunaweza kulinda afya ya mtoto wako.
- Kurekebisha matatizo ya meno kunaweza kukusaidia kudhibiti kiwango chako cha sukari kwenye damu.
- Watoto wanapaswa kufanyiwa uchunguzi wao wa kwanza wa meno kufikia umri wa mwaka 1.

Tafadhali tazama jedwali lililo hapa chini kwa huduma za meno zinazolipiwa na bima.

Huduma zote zinazolipiwa na bima ni za bila malipo. Hizi hulipiwa na bima mradi mtoa huduma wako anasema unahitaji huduma hizo. Tazama safuwima ya “Kiasi, muda na upeo” ili kuona ni mara ngapi unaweza kupata kila huduma bila malipo.

Wakati mwingine unaweza kuhitaji kutembelea mtaalamu. Huduma za kawaida za meno ambazo zinahitaji kupewa rufaa kwa mtaalamu ni:

- Upasuaji wa Kinywa
- Hospitali au kituo cha upasuaji
- Mizizi ya meno
- Matatizo ya ufizi wa meno
- Kupewa nusukaputi ofisini

Huduma Zinazolipiwa na Bima	Kiasi, muda, na upeo wa mafao (huonyesha mfano wa mafao yanayolipiwa na bima)	Je, Rufaa au Idhini ya Mapema inahitajika? (huonyesha mfano wa mafao yanayolipiwa na bima)
Huduma za Matibabu ya Dharura na ya Haraka ya Meno (maumivu makali mno au maambukizi, Kutokwa na damu au kuvimba, majeraha ya meno au fizi)	Hakuna vikomo	Hakuna rufaa au idhini inayohitajika

Mafao ya Washirika Wajawazito na wale walio na umri wa chini ya miaka 21

Tathmini za Meno	Mara Mbili kwa Mwaka	Hakuna idhini ya mapema inayohitajika. Rufaa inahitajika ikiwa si PCD wako.
Usafishaji wa Kinywa	Mara Mbili kwa Mwaka	
Matibabu ya floraidi	Mara Mbili kwa Mwaka	
Eksirei za Kinywa	Mara Moja kwa Mwaka	
Tiba ya Kufunika Meno	Chini ya Umri wa Miaka 16. Katika Meno ya Nyuma ya Watu Wazima Mara Moja kwa Kila Miaka 5	
Vijazo	Inavyohitajika	
Meno bandia ya kisehemu	Mara Moja kwa Kila Miaka 5	Idhini ya mapema inaweza kuhitajika. Rufaa inahitajika ikiwa si PCD wako.
Meno bandia kamili	Mara Moja kwa Kila Miaka 10	Idhini ya mapema inaweza kuhitajika. Rufaa inahitajika ikiwa si PCD wako.
Vizibo	Baadhi ya Meno ya Juu na ya Chini ya Mbele. Vizibo 4 kwa Kila Miaka 7.	Idhini ya mapema inaweza kuhitajika. Rufaa inahitajika ikiwa si PCD wako.
Kuondolewa Meno	Inavyohitajika	Idhini ya mapema inaweza kuhitajika. Rufaa inahitajika ikiwa si PCD wako.
Tiba ya Mizizi ya Meno	Hailipiwi na Bima kwa Magego ya Tatu (Magego ya Mwisho). Washirika Wajawazito Hulipiwa na Bima kwa Magego ya Kwanza.	Hakuna idhini ya mapema inayohitajika kwa Meno ya Mbele na ya Kabla ya Magego Madogo. Idhini ya mapema inaweza kuhitajika kwa Magego. Rufaa inahitajika ikiwa si PCD wako.

Mafao ya Watu Wazima (Ambao si Wajawazito, walio na umri wa zaidi ya miaka 21)		
Tathmini za Meno	Mara Moja kwa Mwaka	Hakuna idhini ya mapema inayohitajika. Rufaa inahitajika ikiwa si PCD wako.
Usafishaji wa Kinywa	Mara Moja kwa Mwaka	
Matibabu ya floraidi	Mara Moja kwa Mwaka	
Eksirei za Kinywa	Mara Moja kwa Mwaka	
Tiba ya Kufunika Meno	Hailipiwi	
Vijazo	Inavyohitajika	
Meno bandia ya kisehemu	Mara Moja kwa Kila Miaka 5	Idhini ya mapema inaweza kuhitajika. Rufaa inahitajika ikiwa si PCD wako.
Meno bandia kamili	Mara Moja kwa Kila Miaka 10	Hakuna idhini ya mapema inayohitajika. Rufaa inahitajika ikiwa si PCD wako.
Vizibo	Hailipiwi	
Kuondolewa Meno	Inavyohitajika	Hakuna idhini ya mapema inayohitajika. Rufaa inahitajika ikiwa si PCD wako.
Tiba ya Mizizi ya Meno	Katika Meno ya Mbele na ya Kabla ya Magego Madogo tu.	Hakuna idhini ya mapema inayohitajika. Rufaa inahitajika ikiwa si PCD wako.

Jedwali lililo hapa juu si orodha kamili ya huduma zinazohitaji idhini ya mapema. Ikiwa una maswali kuhusu idhini za mapema, tafadhali pigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja simu kwa 877-600-5472.

Huduma ambazo OHP hulipia.

Trillium Community Health Plan hulipia huduma zako, lakini kuna huduma fulani tusizolipia. Hizi bado zinalipwa na bima na zitalipwa na mpango wa Oregon Health Plan wa Fee-For-Service. CCOs wakati mwingine huita huduma hizi mafao “yasiyolipwa na bima”. Kuna aina mbili za huduma ambazo OHP hulipia moja kwa moja:

1. Huduma ambapo unapata uratibu wa huduma kutoka kwa Trillium Community Health Plan.
2. Huduma ambapo unapata uratibu wa huduma kutoka kwa OHP.

Huduma zenye uratibu wa huduma wa Trillium Community Health Plan.

Trillium Community Health Plan bado hukupatia uratibu wa huduma kwa huduma fulani. Uratibu wa huduma unamaanisha utapata usafiri wa bila malipo kutoka kwa MTM (Usimamizi wa Usafirishaji wa Kimatibabu) kwa huduma zinazolipiwa na bima, shughuli za usaidizi na nyenzo zozote zilizoidhinishwa unazohitaji kwa huduma zisizolipiwa na bima.

Trillium Community Health Plan itaratibu huduma zako kwa huduma zinazofuata:

- Huduma za Planned Community Birth (Kujifungua Katika Jamii Zilizopangwa, PCB) zinajumuisha huduma za kabla ya kujifungua na baada ya kujifungua kwa watu walio na ujauzito wenye hatari ya chini kama inavyobainishwa na Kitengo cha Mifumo ya Afya cha OHA. OHA inawajibikia kutoa na kulipia huduma za msingi za PCB ikijumuisha angalau, kwa washirika ambao wameidhinishwa kwa PCB, tathmini ya kwanza ya mtoto mchanga aliyezaliwa, kipimo cha uchunguzi wa damu cha mtoto mchanga, ikijumuisha seti ya vifaa vya uchunguzi, huduma za uchungu wa uzazi na kujifungua, ziara za kabla ya kujifungua na huduma za baada ya kujifungua.
- Huduma na usaidizi wa muda mrefu (LTSS) haulipiwi na Trillium Community Health Plan
- Huduma za Family Connects Oregon
- Kuwasaidia washirika kupata ufikiaji kwa huduma za afya ya mwenendo. Mifano ya huduma hizi ni:
 - Dawa fulani za baadhi ya maradhi ya afya ya mwenendo
 - Malipo ya kituo cha tiba ya kikundi kwa washirika walio na umri wa chini ya miaka 21
 - Huduma za muda mrefu za magonjwa ya akili (afya ya mwenendo) kwa washirika wenye umri wa miaka 18 na zaidi
 - Huduma za binafsi katika makao ya ulezi ya watu wazima kwa washirika walio na umri wa miaka 18 na zaidi
 - Kulazwa Hospitalini na kuwekwa katika Makazi ya Tiba kwa magonjwa ya akili kwa vijana walio na miaka 17 na michache
- Na huduma nyingine

Kwa maelezo zaidi au kwa orodha kamili kuhusu huduma hizi, pigia Kitengo cha Usimamizi wa Huduma simu kwa 877-600-5472 au Kitengo cha Huduma kwa Wateja kwa 877-600-5472.

Huduma ambazo OHP hulipia na kutoa uratibu wa huduma.

OHP itaratibu huduma zako kwa huduma zinazofuata:

- Kujitoka uhai ukisaidiwa na daktari chini ya Sheria ya Kufa kwa Heshima ya Oregon.
- Huduma za kutuliza maumivu (za wagonjwa mahututi) kwa washirika wanaoishi katika vituo vya uuguzi stadi
- Huduma za shuleni zinazotolewa chini ya Sheria ya Elimu ya Watu Wenye Ulemavu (IDEA). Kwa watoto wanaopata huduma za matibabu shuleni, kama vile tiba ya matatizo ya kunena.
- Tathmini ya kimatibabu ili kubainisha ikiwa unastahili kwa mpango wa usaidizi au kupanga shughuli za kesi
- Huduma zinazotolewa kwa washirika wa Citizen Waived Medical au CWM Plus-CHIP Prenatal Coverage kwa CWM

- Utaratibu wa kuharibu mimba
- Na huduma nyingine

Wasiliana na timu ya Uratibu wa Huduma ya KEPRO ya OHP kwa 800-562-4620 kwa maelezo zaidi na usaidizi wa huduma hizi.

Bado unaweza kupata usafiri wa bila malipo kutoka kwa MTM (Usimamizi wa Usafirishaji wa Kimatibabu) kwa yoyote kati ya huduma hizi. Tazama ukurasa wa 54 kwa maelezo zaidi. Pigia MTM (Usimamizi wa Usafirishaji wa Kimatibabu) simu kwa 877-583-1552, ili kupanga usafiri. Watumiaji wa TTY, tafadhali piga simu kwa 711.

Washirika wa Veterans and Compact of Free Association (COFA) Dental Program.

Ikiwa wewe ni mshirika wa Veterans Dental Program au COFA Dental Program, Trillium Community Health Plan **hutoa tu** mafao ya meno na usafiri wa bila malipo kwenda kwenye miadi ya meno.

OHP na Trillium Community Health Plan hazitoi ufikiaji kwa huduma za afya ya mwili au afya ya mwenendo au usafiri wa bila malipo kwa huduma hizi, ambazo ni huduma zisizolipiwa na bima zisizo na uratibu wa huduma.

Ikiwa una maswali kuhusu kinacholipiwa na bima na ni mafao yapi yanapatikana, wasiliana na Kitengo cha Huduma kwa Wateja kwa 877-600-5472.

Makatazo ya Kimaadili au Kidini.

Trillium Community Health Plan haiweki vikomo kwa huduma kutokana na makatazo ya kimaadili au kidini.

Ufikiaji kwa huduma unayohitaji.

Ufikiaji unamaanisha kwamba unaweza kupata huduma unayohitaji. Unaweza kupata ufikiaji kwa huduma kwa njia inayotimiza mahitaji yako ya kitamaduni na lugha. Ikiwa Trillium Community Health Plan haishirikiani na mtoa huduma anayetimiza mahitaji yako ya ufikiaji, unaweza kupata huduma hizi nje ya mtandao. Trillium Community Health Plan huhakikisha kwamba huduma ziko karibu na unakoishi au karibu na unakotaka kupata huduma. Hii inamaanisha kwamba kuna watoa huduma wa kutosha katika eneo hilo na kuna aina tofauti za watoa huduma wa kuchagua.

Huwa tunafuatilia mtandao wetu wa watoa huduma ili kuhakikisha tuna huduma za msingi na huduma za mtaalamu unazohitaji. Pia tunahakikisha kwamba una ufikiaji kwa huduma zote zinazolipiwa na bima katika eneo lako.

- **Eneo la mjini:** Ufikiaji kwa watoa huduma ndani ya maili 30, au dakika 30 kutoka unakoishi. Eneo la mjini linamaanisha unaishi katika au karibu na jiji.
- **Eneo la kijijini:** Ufikiaji kwa watoa huduma ndani ya maili 60, au dakika 60 kutoka unakoishi. Eneo la kijijini linamaanisha huishi katika au karibu na jiji.

Watoa huduma wetu pia watahakikisha kwamba utakuwa na ufikiaji kwa eneo halisi, marekebisho yanayofaa na vifaa vinavyoweza kufikiwa ikiwa una ulemavu wa mwili na/au kiakili. Wasiliana na Trillium Community Health Plan kwa 877-600-5472 ili kuomba marekebisho. Watoa huduma pia huhakikisha saa za ofisi ni sawa kwa washirika wa OHP na watu wengine wote.

Usafiri kwenda kupata huduma.

Unaweza kupata usafiri wa bila malipo kwenda kwenye miadi inayolipiwa na bima. Tazama ukurasa wa 58 ili kupata habari kuhusu jinsi unavyoweza kupata usafiri wa bila malipo. Pigia MTM (Usimamizi wa Usafirishaji wa Kimatibabu) simu kwa 877-583-1552, ili kupanga usafiri. Watumiaji wa TTY, tafadhali piga simu kwa 711

Chagua mtoa huduma.

Una haki ya kuchagua mtoa huduma wako na mahali unakopata huduma zako za afya. Unaweza kuchagua kutoka kwa orodha ya watoa huduma wanaoshirikiana na Trillium Community Health Plan. Orodha hiyo ya watoa huduma inaitwa Sajili ya Watoa Huduma ya Trillium Community Health Plan. Pata habari zaidi kuhusu sajili hiyo katika ukurasa wa 43.

Usaidizi wa kupanga huduma zako.

Uratibu wa huduma unamaanisha utapata usaidizi wa kuratibu ziara zako, kupata usaidizi na nyenzo. Pata habari zaidi kuhusu uratibu wa huduma katika ukurasa wa 45 au pigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja simu kwa 877-600-5472.

Inachukua muda gani kupata huduma.

Tunashirikiana na watoa huduma ili kuhakikisha kwamba utahudumiwa, kutibiwa au kupewa rufaa ndani ya nyakati zilizoordheshwa hapa chini:

Aina ya huduma	Kipindi cha wakati
Afya ya mwili	
Miadi ya kawaida	Ndani ya wiki 4
Huduma za Matibabu ya Haraka	Ndani ya saa 72 au ilivyoonyeshwa katika uchunguzi wa kwanza.
Huduma za Matibabu ya Dharura	Mara moja au hupewa rufaa kwa idara ya dharura kulingana na hali yako.
Huduma za kinywa na meno kwa watoto na watu ambao si wajawazito	
Miadi ya kawaida ya afya ya kinywa	Ndani ya wiki 8 isipokuwa ikiwa kuna sababu ya kimatibabu ya kusubiri zaidi.
Huduma za matibabu ya haraka ya kinywa	Ndani ya wiki 2.
Huduma za Matibabu ya Dharura ya meno	Huhudumiwa au kutibiwa ndani ya saa 24
Huduma za kinywa na meno kwa watu ambao ni wajawazito	
Huduma za kawaida za kinywa	Ndani ya wiki 4 isipokuwa ikiwa kuna sababu ya kimatibabu ya kusubiri zaidi.
Huduma za matibabu ya haraka ya meno	Ndani ya wiki 1
Huduma za matibabu ya dharura ya meno	Huhudumiwa au kutibiwa ndani ya saa 24
Afya ya mwenendo	
Huduma za afya ya mwenendo za kawaida kwa watu ambao si wa kipaumbele	Tathmini ndani ya siku 7 baada ya ombi, huku miadi ya pili ikiratibiwa inavyofaa kimatibabu.
Huduma za afya ya mwenendo za haraka kwa watu wote	Ndani ya saa 24
Huduma maalum za afya ya mwenendo kwa watu waliopewa kipaumbele	
Wanawake wajawazito, wanajeshi wa zamani na familia zao, wanawake walio na watoto, watunzaji wasiolipwa, familia, na watoto wenye umri wa miaka 0-5, washirika walio na VVU/UKIMWI au kifua kikuu, washirika walio katika hatari ya kichaa cha tukio la kwanza na watu wenye I/DD	Tathmini ya mara moja na kuingia. Ikiwa huduma za muda zinahitajika kwa sababu hakuna watoa huduma walio na ziara, matibabu katika kiwango kinachofaa cha huduma lazima yafanyike ndani ya siku 120 kuanzia wakati ambapo mgonjwa anawekwa katika orodha ya kusubiri.
Ugonjwa wa matumizi ya opiodi	Tathmini na kuingizwa ndani ya saa 72
Matibabu yanayosaidiwa na dawa	Haraka iwezekanavyo, lakini si zaidi ya saa 72 baada ya tathmini na kuingia.

Kwa huduma maalum za afya ya mwenendo ikiwa hakuna chumba au nafasi inayopatikana:

- Utawekwa katika orodha ya kusubiri.
- Utapewa huduma nyingine ndani ya saa 72.
- Huduma hizi zitakuwa za muda hadi kutakapokuwa na chumba au nafasi inayopatikana.

Ikiwa una maswali yoyote kuhusu ufikiaji kwa huduma, pigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja simu kwa 877-600-5472.

Maoni ya mtaalamu mwingine.

Una haki ya kupata maoni ya mtaalamu mwingine kuhusu maradhi au matibabu yako. Maoni ya mtaalamu mwingine ni ya bila malipo. Ikiwa unataka maoni ya mtaalamu mwingine, pigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja cha Trillium Community Health Plan simu na utwambie kwamba unataka kutembelea mtoa huduma mwingine.

Ikiwa hakuna mtoa huduma aliye na sifa zinazostahili ndani ya mtandao wetu na unataka kutembelea mtoa huduma nje ya mtandao wetu kwa maoni ya mtaalamu mwingine, wasiliana na kitengo cha huduma kwa wateja cha Trillium Community Health Plan kwa usaidizi. Tutapanga maoni ya mtaalamu mwingine bila malipo.

Watoa huduma wa msingi (PCPs).

Mtoa huduma wa msingi ni utakayemtembelea kwa ziara, dawa zinazoagizwa na daktari na huduma za mara kwa mara. Unaweza kuchagua mmoja, au tunaweza kukusaidia kuchagua mmoja.

Watoa huduma wa msingi (PCPs) wanaweza kuwa madaktari, wauguzi wataalamu na zaidi. Una haki ya kuchagua PCP ndani ya mtandao wa Trillium Community Health Plan. Ukikosa kuchagua mtoa huduma ndani ya siku 30, Trillium Community Health Plan itakukabidhi kliniki au ikuchagulie PCP. Trillium Community Health Plan itakutumia barua iliyo na maelezo ya mtoa huduma wako.

Watoa huduma wa ndani ya mtandao

Trillium Community Health Plan hushirikiana na baadhi ya watoa huduma, lakini si wote. Watoa huduma tunaoshirikiana nao huitwa watoa huduma wa ndani ya mtandao au wanaoshiriki. Watoa huduma tusioshirikiana nao huitwa watoa huduma wa nje ya mtandao. Huenda ukaweza kutembelea watoa huduma wa nje ya mtandao ikiwa inahitajika, lakini lazima washirikiane na Oregon Health Plan.

PCP wako atashirikiana nawe ili kukusaidia uendeleo kuwa na afya njema iwezekanavyo. Hufuatilia mahitaji yako yote ya huduma za msingi na za utaalamu. PCP wako:

- Atakujua na kujua historia yako ya matibabu.
- Atatoa huduma zako za matibabu.
- Atasasisha rekodi zako za matibabu na kuzihifadhi katika sehemu moja.

PCP wako atakupatia rufaa kwa mtaalamu au kukulaza hospitalini ikiwa inahitajika.

Kila mwanafamilia wako anayetumia OHP lazima achague PCP. Kila mtu anaweza kuwa na PCP tofauti.

Ukikosa kuchagua PCP, tutakuchagulia mmoja, tafadhali pigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja simu ikiwa ungependa kubadilisha PCP wako. Unaweza kuanza kutembelea PCP wako mpya siku ambayo mabadiliko haya yatafanywa.

Usisahau kuuliza Trillium Community Health Plan kuhusu daktari wa meno, mtoa huduma wa afya ya akili, na famasia.

Unaweza kuchagua Daktari wa Meno wa Msingi (PCD) kutoka kwa Trillium Find a Dentist kwenye tovuti yetu: www.trilliumohp.com/members/oregon-health-plan/for-members/benefit-information.html.html au pigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja simu kwa 877-600-5472, TTY:877-600-5473.

Unaweza kuchagua mtoa huduma wa afya ya akili kutoka kwa Trillium Find a Provider kwenye tovuti yetu:

www.trilliumohp.com/members/oregon-health-plan/for-members/benefit-information.html.html Ikiwa unahitaji usaidizi wa kuchagua mtoa huduma wa afya ya akili, pigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja simu kwa 877-600-5472, TTY: 877-600-5473.

Kila mwanafamilia wako lazima awe na daktari wa meno ambaye atakuwa daktari wake wa meno wa msingi (PCD). Utaenda kwa PCD wako kwa mahitaji yako mengi ya huduma za meno. PCD wako atakutuma kwa mtaalamu ikiwa unahitaji kwenda kwa mmoja.

PCD wako ni muhimu kwa sababu:

- Ndiye mwasiliani wako wa kwanza unapohitaji huduma za meno.
- Husimamia huduma zako na matibabu ya afya ya meno.
- Hupanga huduma zako za kitaalamu.

Mabadiliko ya PCP wako

Ikiwa kuna mabadiliko na PCP wako hana kandarasi na Trillium Community Health Plan tena, tutakutumia barua siku 30 kabla ya mabadiliko hayo kufanyika. Ikiwa mabadiliko haya yamefanywa tayari, tutakutumia barua ndani ya siku 15 baada ya mabadiliko hayo.

Sajili ya watoa huduma.

Unaweza kuchagua PCP wako kutoka kwa sajili ya watoa huduma katika:

www.trilliumohp.com/find-a-provider.html. Pia unaweza kupigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja simu kwa usaidizi, au ili kuomba nakala ya karatasi ya sajili ya watoa huduma.

Hapa ni mifano ya maelezo unayoweza kupata katika Sajili ya Watoa Huduma:

- Ikiwa mtoa huduma anakubali wagonjwa wapya.
- Aina ya mtoa huduma (wa tiba, wa meno, afya ya mwenendo, famasia, nk.).
- Jinsi ya kuwasiliana naye.
- Machaguo ya huduma kwa video na simu (huduma ya afya kwa vifaa vya mawasiliano).
- Usaidizi wa lugha (ikiwa ni pamoja na tafsiri na wakalimani).
- Marekebisho kwa watu walio na ulemavu wa mwili.

Unaweza kupata nakala ya karatasi. Unaweza kuipata kwa muundo mwingine (kama vile lugha nyingine, maandishi makubwa, au Breli) bila malipo. Pigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja simu kwa 877-600-5472.

Panga miadi.

Unaweza kupanga miadi na mtoa huduma wako punde tu baada ya kuchagua mmoja.

PCP wako anapaswa kuwa mtu wa kwanza unayempigia simu wakati unahitaji huduma. Atapanga miadi au kukusaidia kuamua aina ya huduma unayohitaji. PCP wako pia anaweza kukupatia rufaa kwa huduma au nyenzo nyingine zinazolipiwa na bima. Mpigie simu moja kwa moja ili kupanga miadi.

Ikiwa wewe ni mgeni kwa PCP wako, panga miadi ya uchunguzi. Hivi anaweza kukujua na historia yako ya matibabu kabla ya kukabiliwa na suala au tatizo. Hili litakusaidia kuepuka kuchelewa kwokwote wakati wa kwanza unapohitaji kutumia mafao yako.

Kabla ya miadi yako, andika:

- Maswali uliyo nayo kwa PCP wako au watoa huduma wengine.
- Historia ya matatizo ya afya ya familia.
- Dawa zilizoagizwa na daktari, dawa zilizoununuliwa bila agizo la daktari, vitamini au vijalizo unavyotumia.

Piga simu kwa miadi wakati wa saa za ofisi na uwaambie:

- Wewe ni mshirika wa Trillium Community Health Plan.
- Jina lako na nambari yako ya kitambulisho cha Trillium Community Health Plan.
- Aina ya miadi unayohitaji.
- Ikiwa unahitaji mkalimani na lugha unayohitaji.

Wajulishe ikiwa wewe ni mgonjwa na unahitaji kuhudumiwa na mtu siku hiyo.

Unaweza kupata usafiri wa bila malipo kwenda kwenye miadi yako. Pata habari zaidi kuhusu usafiri wa bila malipo katika ukurasa wa 58.

Miadi ambayo haikuhudhuriwa.

Jaribu kutokosa kuhudhuria miadi. Ikiwa unahitaji kutohudhuria miadi, pigia PCP wako simu na ubatilishe mara moja. Atakupangia ziara nyingine. Ukikosa kuiambia ofisi ya mtoa huduma wako mapema, wanaweza kutokubali kukuhudumia tena.

Kila mtoa huduma ana kanuni zake mwenyewe kuhusu miadi ambayo haikuhudhuriwa. Muulize kuhusu kanuni zake.

Pata usaidizi wa kupanga huduma zako kwa Uratibu wa Huduma.

Unaweza kupata uratibu wa huduma kutoka kwa kituo cha huduma za msingi zinazolenga mgonjwa (PCPCH), mtoa huduma wa msingi, au timu nyingine ya huduma za msingi. Unaweza kuzungumza na mtoa huduma wako au Kitengo cha Huduma kwa Wateja cha Trillium Community Health Plan ili kuomba mratibu wa huduma.

Madhumuni ya huduma hii ni kufanya afya yako ya jumla kuwa bora. Tutasaidia kubainisha mahitaji yako ya huduma za afya na kukusaidia kudhibiti afya na ustawi wako.

Unaweza kutuomba mratibu wa huduma. Mwakilishi wako anaweza kukuomba pia. Pigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja simu kwa 877-600-5472 Jumatatu hadi Ijumaa, saa 8:00 asubuhi hadi saa 5:00 jioni TTY: 877-600-5473

Kushirikiana kwa huduma zako.

Timu ya mratibu wako wa huduma itashirikiana nawe na mtoa huduma wako kwa karibu. Watakuunganisha na nyenzo za jamii na usaidizi wa jamii zinazoweza kukusaidia. Wataunda mpango ili kuhakikisha kwamba timu yako ya huduma inashirikiana kutoa huduma zako, na ili kufuatilia baada ya huduma zako.

Tungependa kusaidia kuhakikisha kwamba mtu yeyote anayekupatia huduma anaweza kulenga kukusaidia kuwa mzima na kuimarisha afya yako. Timu yako ya huduma itashirikiana ili kusimamia na kupanga huduma zako. Hili litasaidia kuhakikisha kwamba unapata huduma bora zaidi kwa mahitaji yako.

Wauguzi na wasimamizi wa kesi wa timu ya huduma wana mafunzo maalum kwa matatizo mengi ya afya. Wanaweza kukusaidia kwa:

- Kisukari.
- Ugonjwa wa moyo.
- Pumu.
- Mfadhaiko.
- Shinikizo la juu la damu.
- Na maradhi mengine.

Timu hii ya huduma pia iko tayari kukusaidia kwa idhini zako na mahitaji mengine. Wanaweza:

- Kukusaidia kuelewa mafao yako na jinsi yanavyofanya kazi.
- Kukusaidia kuchagua mtoa huduma wa msingi (PCP).
- Kutoa huduma na ushauri ambao ni rahisi kufuata.
- Kukusaidia kuelewa mfumo wa huduma za afya zinazoratibiwa.
- Kukusaidia kupata huduma za afya ya mwenendo.
- Kusaidia kuhakikisha kwamba watoa huduma wako wanazungumza miongoni mwao kuhusu mahitaji yako ya huduma za afya.

Timu yako ya huduma inaweza kusaidia kupata nyenzo nyingine katika jamii yako, kama usaidizi kwa mahitaji yasiyo ya tiba. Baadhi ya mifano ni:

- Makazi salama.
- Chakula bora.
- Usafiri.
- Mafunzo na madarasa.
- Usaidizi wa familia, au
- Huduma za kijamii.

Washirika walio na Medicare.

Pia unaweza kupata usaidizi wa mafao yako ya OHP na Medicare. Mratibu wa huduma hushirikiana nawe, watoa huduma wako, mpango wako wa Medicare Advantage na/au mtunzaji wako. Tunashirikiana na watu hawa ili kukupatia huduma za kijamii na usaidizi, kama huduma za jamii ambazo ni mahususi kwa utamaduni.

Wawakilishi wa Kuunganisha Washirika (MCRs)

Wawakilishi wa Kuunganisha Washirika (MCRs) ni Wafanyakazi wa Afya ya Jamii ambao wamethibitishwa katika Jimbo la Oregon na wanaofanyia Trillium kazi.

MCRs wanaweza kusaidia kuunganisha washirika na huduma zinazohitajika. MCRs wanaweza kukusaidia kufikia mafao yako na kupanga miadi ya matibabu. Pia wanaweza kuratibu mahitaji ya kijamii kama makazi na chakula. Wanaweza kukuunganisha na rasilimali za jamii.

MCRs hushirikiana kwa karibu na kituo chako cha matibabu ya msingi na timu ya ndani ya Trillium. Wanaweza kukutana nawe kupitia kwa simu, video au nyumbani kwako. Wanaweza kusaidia kwa mambo kama jinsi ya kukumbuka kutumia dawa zako kwa wakati unaofaa. Pia wanaweza kukusaidia kwa maombi ya usaidizi wa makazi au kupasha nyumba joto. Pia wanaweza kukusaidia kupata vitu kupitia mifumo ya kijamii. MCR wanaweza kutoa mafunzo ya afya kuhusu kisukari na pumu.

MCR wana uwezo mkubwa wa kutatua matatizo na wanajua jamii zao. Ikiwa ungependa kushirikiana na MCR, tafadhali piga simu kwa 877-600-5472 na uombe Mwakilishi wa Miunganisho ya Washirika.

Uratibu wa Uangalizi Makini

Unaweza kupata huduma za Uratibu wa Uangalizi Makini (ICC) ikiwa unahitaji usaidizi zaidi. Huduma za ICC hutoa usaidizi wa ziada kwa wale wanaohitaji.

Baadhi ya watu wanaostahili kwa huduma za ICC wanaweza kuwa:

- Watu wazima wenye umri mkubwa, wale walio na matatizo ya kusikia, viziwi, vipofu au walio na ulemavu mwingine.
- Wale walio na mahitaji ya juu ya huduma za afya, maradhi sugu mengi, au maradhi mabaya na yanayoendelea ya akili (SPMI).
- Watu wanaopokea huduma za matibabu na usaidizi wa muda mrefu (LTSS) zinazofadhiliwa na Medicaid.
- Wale wanaopokea matibabu yanayosaidiwa na dawa (MAT) kwa Ugonjwa wa Matumizi ya Dawa za Kulevya (SUD).
- Watu ambao wamebainishwa kuwa na ujauzito wenye hatari ya juu.
- Watumiaji wa dawa za kulevya za kudungwa kwa IV.
- Wale walio na SUD wanaohitaji uhibitaji wa matatizo yanayotokana na kuacha kutumia dawa za kulevya.
- Mtu aliye na VVU/UKIMWI au aliye na kifua kikuu.
- Wanajeshi wa zamani na familia zao.
- Wale walio na hatari ya juu ya kichaa cha tukio la kwanza.
- Wale walio ndani ya jamii ya ulemavu wa kiakili na maendeleo (IDD).
- Na wengine.

Uratibu wa Uangalizi Makini unaweza pia kuwasaidia watoto:

- Wenye umri wa miaka 0-5 ambao wanaonyesha dalili za mapema za matatizo ya kijamii/kihisia au mwenendo au ambao wamebainishwa kuwa na Ugonjwa Mbaya wa Kihisia (SED).
- Walio na ugonjwa wa mtoto mchanga aliyezaliwa kutengwa na dawa za kulevya zilizotiwa mwilini mwake kabla ya kuzaliwa.
- Walio katika Child Welfare.

Wewe na mratibu wako wa ICC mtaunda mpango unaoitwa mpango wa Uratibu wa Uangalizi Makini (ICCP). Mpango huu utauandwa ndani ya siku 10 baada ya kuanza mpango wa ICC. Utakusaidia kutimiza mahitaji yako. Pia utakusaidia kuweka malengo yako ya afya ya binafsi na usalama.

Mpango wako wa huduma utaorodhesha usaidizi na huduma zinazohitajika ili kukusaidia kutimiza malengo yako. Mpango huo wa huduma utasasishwa kila siku 90, au mapema zaidi ikiwa mahitaji yako ya huduma za afya yatabadilika. Unaweza kupata nakala ya mpango wako.

Utakuwa na timu ya ICC ya kukusaidia. Timu hii itajumuisha watu tofauti ambao wataashirikiana ili kutimiza mahitaji yako, kama vile watoa huduma na wataalamu unaoshirikiana nao. Mpango huu hushughulikia mahitaji ya kimatibabu, kijamii, kitamaduni, kimaendeleo, kitabia, kielimu, kiroho na kifedha ili upate matokeo chanya ya afya na ustawi. Kazi ya timu yako ya huduma ni kuhakikisha kwamba watu wanaofaa ni sehemu ya mpango wako wa huduma ili kukusaidia kutimiza malengo yako. Sote tutashirikiana ili kukusaidia.

Mratibu wako wa huduma pia anaweza:

- Kufikia nyenzo ili kuhakikisha unajihisi sawa, salama na unayejaliwa.
- Kutumia mipango ya huduma ili kukusaidia kudhibiti matatizo sugu ya afya.
- Kusaidia kwa matatizo ya afya kama vile kisukari, ugonjwa wa moyo na pumu.
- Kusaidia kwa matatizo ya afya ya mwenendo ikiwa ni pamoja na mfadhaiko na ugonjwa wa matumizi ya dawa za kulevya.
- Kuunda mpango wa matibabu pamoja nawe.

Pigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja cha Trillium Community Health Plan simu kwa 877-600-5472 ili kupata mratibu wa huduma wa ICC. Trillium Community Health Plan itahakikisha kwamba wewe au mwakilishi wako anapata jina na nambari ya simu ya mratibu wako wa huduma wa ICC.

Huduma za uratibu wa uangalizi makini zinapatikana Jumatatu hadi Ijumaa, saa 8:00 asubuhi hadi saa 5:00 jioni. Ikiwa huwezi kupata huduma za ICC wakati wa saa za kawaida za kazi, Trillium Community Health Plan itakupatia machaguo mengine.

Uchunguzi maalum na huduma za kuzuia magonjwa kwa washirika walio na umri wa chini ya miaka 21.

Huduma za Uchunguzi wa Mapema na Mara kwa Mara, Utambuzi wa Magonjwa na Matibabu (EPSDT) ni pana na huduma za afya za kuzuia magonjwa kwa watoto kuanzia kuzaliwa hadi umri wa miaka 21. Mafao haya yanakupatia huduma zinazoweza kuzuia na kugundua ikiwa kuna maradhi au matatizo ya afya yaliyo katika hatua za mapema. Yanaweza kupunguza hatari ya ugonjwa, ulemavu au huduma nyingine za kimatibabu/afya ya akili zinazoweza kuhitajika.

Mpango wa EPSDT hutoa:

- Tathmini za kimatibabu za ukuaji na maendeleo ya mtoto, uchunguzi, na huduma za kutambua magonjwa ili kubainisha ikiwa kuna matatizo yoyote ya mwili, meno, maendeleo, na afya ya akili kwa washirika wenye umri wa miaka 0 hadi 21.
- Pia hulipia huduma za afya, matibabu na hatua nyingine za kurekebisha au kusaidia kwa maradhi yoyote yaliyogunduliwa.

Kwa washirika wanaostahiki kwa EPSDT wanaoomba, Trillium Community Health Plan lazima itoe:

- Uchunguzi na tathmini zinazoratibiwa mara kwa mara za afya ya jumla ya mwili na akili, hali ya ukuaji, maendeleo, na lishe ya watoto wachanga, watoto, na vijana walio na umri wa chini ya miaka 21.

Ikiwa wewe au mwanafamilia wako anahitaji huduma za EPSDT, shirikiana na mtoa huduma wako wa msingi (PCP). Atakusaidia kupata huduma unazohitaji. Ikiwa huduma zozote zinahitaji idhini, ataishughulikia. Shirikiana na daktari wako wa meno wa msingi kwa huduma zozote za meno za EPSDT. Huduma zote za EPSDT ni za bila malipo kwa washirika hadi umri wa miaka 21.

Unaweza kupata huduma za EPSDT kutoka kwa tabibu (MD au DO), wauguzi wataalamu, wasaidizi wa tabibu wenye leseni, na wataalamu wengine wa afya wenye leseni (watoa huduma wa huduma zinazoendelea). Watoa huduma hawa pia wanaweza kukupatia rufaa ya moja kwa moja kwa daktari wa meno wa kutoa huduma za meno. Nyakati na aina za huduma za meno zinaweza kupatikana hapa: www.oregon.gov/oha/HSD/OHP/Tools/OHP-Recommended-Dental-Periodicity-Schedule.pdf

Usaidizi wa kupata huduma za EPSDT.

- Pigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja simu kwa 877-600-5472.
- Pigia Mtoa Huduma wa Meno simu ili kupanga huduma za meno au kwa maelezo zaidi:

Advantage Dental Services

Kitengo cha Huduma kwa Wateja Bila kutozwa ada 1-866-268-9631 TTY: 711

Capitol Dental Care

Kitengo cha Huduma kwa Wateja 1-503-585-5205 au bila kutozwa ada 1-800-525-6800
TTY: 1-800-735-2900

Oregon Dental Service

Kitengo cha Huduma kwa Wateja 1-503-243-2987 au bila kutozwa ada 1-800-342-0526

TTY: 1-503-243-3958 au 1-800-466-6313

- Unaweza kupata usafiri wa bila malipo kuelekea na kutoka kwa ziara za mtoa huduma wa EPSDT zinazolipiwa na bima. Pigia 877-600-5472 ili kupanga usafiri au kwa maelezo zaidi.
- Pia unaweza kupata maelezo haya katika tovuti yetu katika:
www.trilliumohp.com/members/oregon-health-plan/Benefits-and-Services/transportation.html

Uchunguzi.

OHP hulipia ziara za uchunguzi za EPSDT kwa nyakati zinazofaa kwa umri. Pindi baada ya kuomba uchunguzi, matibabu kwa kawaida yataanza ndani ya miezi 6. OHP hufuata miongozo ya American Academy of Pediatrics na Bright Futures. Bright Futures inaweza kupatikana katika: <https://brightfutures.aap.org/Pages/default.aspx>.

Miongozo ya Bright Futures hutoa mwongozo wa uchunguzi wote wa huduma za kuzuia magonjwa na ziara za uchunguzi wa ukuaji na maendeleo ya mtoto.

Ziara za uchunguzi lazima ziwe:

- Uchunguzi wa maendeleo.
- Kipimo cha sumu ya risasi:
 - Watoto lazima wafanyiwe vipimo vya uchunguzi wa sumu ya risasi kwenye damu katika umri wa miezi 12 na miezi 24. Mtoto yeyote mwenye umri wa kati ya miezi 24 na 72 asiye na rekodi ya kipimo cha awali cha uchunguzi wa sumu ya risasi kwenye damu lazima afanyiwe kipimo hicho.
 - Kukamilisha hojaji ya tathmini ya hatari hakutimizi sharti la uchunguzi wa sumu ya risasi kwa watoto walio katika OHP. Watoto wote walio na sumu ya risasi mwilini wanaweza kupata huduma za ufuatiliaji za usimamizi wa kesi.
- Vipimo vingine vya maabara vinavyohitajika (kama vile kipimo cha anemia, kipimo cha selimundu, na vingine) kulingana na umri na hatari ya mteja.
- Tathmini ya hali ya lishe.
- Tathmini ya jumla ya mwili bila kuvaa mavazi inayojumuisha uchunguzi wa meno na fizi.
- Historia kamili ya afya na maendeleo (ikiwa ni pamoja na ukaguzi wa maendeleo ya mwili na afya akili).
- Chanjo (sindano za chanjo) zinazotimiza viwango vya tiba:
 - Ratiba ya Kuchanjwa ya Mtoto (tangu kuzaliwa hadi miaka 18):
www.cdc.gov/vaccines/schedules/hcp/imz/child-adolescent.html
 - Ratiba ya Kuchanjwa ya Mtu Mzima (19+):
www.cdc.gov/vaccines/schedules/hcp/imz/adult.html
- Maelekezo na elimu ya afya kwa wazazi na watoto.
- Rufaa kwa matibabu yanayohitajika kimatibabu ya mwili na afya ya akili.
- Vipimo vinavyohitajika vya masikio na macho.

- Huduma na uchunguzi unaopendekezwa kwa umri fulani, hadi umri wa miaka 21. Tazama ratiba ya Bright Futures hapa: https://downloads.aap.org/AAP/PDF/periodicity_schedule.pdf
- Na nyingine.

Ziara za EPSDT pia zinajumuisha uchunguzi au tathmini ambazo hazijaratibiwa ambazo zinaweza kufanyika wakati wowote kwa sababu ya ugonjwa au mabadiliko ya afya.

Rufaa ya EPSDT, uchunguzi wa kutambua ugonjwa na matibabu.

Mtoa huduma wako wa msingi anaweza kukupatia rufaa akigundua maradhi ya mwili, afya ya akili, matumizi ya dawa za kulevya, au meno. Mtoa huduma mwingine atakusaidia kwa uchunguzi zaidi wa kutambua ugonjwa na/au matibabu.

Mtoa huduma anayefanya uchunguzi ataeleza hitaji la rufaa kwa mtoto na mzazi au mlezi. Ikiwa unakubali rufaa hiyo, mtoa huduma huyo atashughulikia hati zinazohusika.

Trillium Community Health Plan au OHP pia itasaidia kwa uratibu wa huduma, inavyohitajika.

Uchunguzi unaweza kubainisha hitaji la huduma zinazofuata:

- Uchunguzi wa kutambua ugonjwa na matibabu ya kasoro za kuona na kusikia, ikiwa ni pamoja na miwani na vifaa vya usaidizi wa kusikia.
- Huduma za meno, kwa umri mdogo zaidi inavyowezekana, zinazohitajika ili kutuliza maumivu na maambukizi, kurejesha afya ya meno na matengenezo ya afya ya meno.
- Chanjo. (Ikiwa itabainishwa wakati wa uchunguzi kwamba chanjo inahitajika na inafaa kutolewa wakati wa uchunguzi, basi matibabu ya chanjo lazima yatolewe kwa wakati huo.)

Huduma hizi lazima zitolewe kwa wanaostahiki kwa EDPST wanaozihitaji.

Trillium Community Health Plan itatoa usaidizi wa rufaa kwa washirika au wawakilishi wao kwa huduma za kijamii, mipango ya elimu, mipango ya usaidizi wa lishe, na huduma nyingine.

Wafanyakazi wa Afya wa Kawaida (THW).

Wafanyakazi wa Afya wa Kawaida (THW) husaidia kwa maswali uliyo nayo kuhusu huduma zako za afya na mahitaji ya kijamii. Husaidia kwa mawasiliano kati ya watoa huduma wako wa afya na watu wengine wanaohusika katika huduma zako. Pia huunganisha na watu na huduma katika jamii zinazoweza kukusaidia.

Kuna aina chache tofauti za wafanyakazi wa afya wa Kawaida.

- **Doula wa Uzazi:** Doula (wa Uzazi) ni mtu anayetoa huduma za uzazi ambaye hutoa usaidizi wa binafsi, usio wa tiba kwa watu wajawazito na familia wakati wa ujauzito, kujifungua, na baada ya kujifungua.

- **Mfanyakazi wa Afya ya Jamii:** Mfanyakazi wa afya ya jamii anaelewa watu na jamii unakoishi. Hukusaidia kufikia huduma za afya na jamii. Mfanyakazi wa afya ya jamii hukusaidia kuanza mwenendo mwema. Kwa kawaida hushiriki kabila lako, lugha au uzoefu wa matukio ya maisha.
- **Mwelekezi wa Binafsi wa Afya:** Mtu ambaye hutoa taarifa, zana, na usaidizi ili kukusaidia kufanya maamuzi bora zaidi kuhusu afya na ustawi wako, kulingana na hali yako.
- **Mtaalamu wa Usaidizi wa Wenza:** Mtu ambaye ana uzoefu wa matukio ya maisha wa afya ya akili, uraibu na kupona. Au huenda alikuwa mzazi wa mtoto anayepata matibabu ya afya ya akili au uraibu. Hutoa auni, kutia motisha, na usaidizi kwa wale wanaokabiliwa na matatizo ya uraibu na afya ya akili. Anaweza kukusaidia unapokumbana na mambo sawa.
- **Mtaalamu wa Ustawi wa Wenza:** Mtu ambaye hufanya kazi kama sehemu ya timu ya afya ya nyumbani na kukutetea wewe na mahitaji yako. Hutoa usaidizi kwa afya ya jumla ya watu katika jamii yake na anaweza kukusaidia kupata nufuu dhidi ya matatizo ya uraibu, afya ya akili, au ya mwili.
- **Wafanyakazi wa Afya wa Kawaida wa Kikabila:** Mtu ambaye husaidia jamii za kikabila au mjini za Wahindi kuboresha afya yao ya jumla. Hutoa elimu, ushauri, na usaidizi ambao unaweza kuwa mahususi kwa desturi za kikabila.

THW anaweza kukusaidia kwa mambo mengi, kama:

- Kupata mtoa huduma mpya.
- Kupokea huduma unazohitaji.
- Kuelewa mafao yako.
- Kutoa taarifa kuhusu huduma na usaidizi wa afya ya mwenendo.
- Kutoa ushauri kuhusu nyenzo za jamii unazoweza kutumia.
- Mtu wa kuzungumza naye kutoka kwa jamii yako.

Pigia mshirika wetu wa THW simu ili kupata habari zaidi kuhusu THWs na jinsi ya kutumia huduma zao.

Maelezo ya Mawasiliano ya Mshirika wa THW:

Kristinia Rogers
 krogers@trilliumchp.com
 877-600-5472

Ikiwa tutabadilisha maelezo ya mawasiliano ya mshirika wa THW, unaweza kupata maelezo yaliyosasishwa kwenye tovuti yetu katika: www.trilliumohp.com/members/oregon-health-plan/wellness/traditional-health-workers.html.

Huduma za ziada

Huduma Mbadala (ILOS)

Huduma Mbadala (ILOS)

Trillium Community Health Plan hutoa huduma au mazingira ambayo ni mbadala unaofaa kimatibabu kwa huduma zinazolipiwa na OHP. Hizi huitwa “huduma mbadala” (ILOS). Hutolewa kama machaguo ya usaidizi kwa washirika wakati ambapo mazingira au huduma za kawaida hazitimizi mahitaji ya Washirika wetu. Trillium Community Health Plan hutoa ILOS zinazofuata:

Huduma za Usaidizi wa Kupata Nafuu Kutoka kwa Mwenza na Mshirika Mwenye Sifa Zinazostahili wa Afya ya Akili zinazotolewa katika Mazingira Mbadala kama mbadala wa huduma za tiba ya afya ya mwenendo. ILOS hii pia inaweza kufaa kwa washirika walio na maradhi ya afya ya mwenendo wanaohitaji huduma za kuwezesha kuishi maisha ya kawaida za kisaikolojia na kijamii.

- Huduma za Usaidizi wa Kupata Nafuu Kutoka kwa Mwenza na Mshirika Mwenye Sifa Zinazostahili wa Afya ya Akili zinazotolewa katika mazingira mbadala zinaweza kujumuisha mipango ya kwenda kituoni, utoaji wa huduma katika jamii, na vituo vya huduma vya jamii mbali na mazingira ya kawaida ya ofisi au kliniki.
- Mfano wa ILOS: Huduma za uhamasishaji na ushirikishaji zinazotolewa na Wataalamu wa Usaidizi wa Wenza ambao wamethibitishwa, Wataalamu wa Ustawi wa Wenza, au Washirika wa Afya ya Akili Wenye Sifa Zinazostahili, ili kuwashirikisha washirika katika huduma zao na kutoa usaidizi unaoendelea wa kuimarisha usimamizi wa ustawi, ujuzi wa kukabiliana na hali, ujuzi wa maisha ya kujitegemea, na usaidizi wa kupata nafuu. Huduma zinaweza kutolewa ama kabla ya au baada ya tathmini na utambuzi wa ugonjwa, katika mazingira ya kimatibabu au jamii, katika vikao vya binafsi au kikundi, na zinaweza kujumuisha huduma za kwenda kituoni, huduma za mabadiliko ya huduma, huduma mahususi kwa utamaduni, na huduma zinazolenga jamii mahususi za OHP.

Huduma za Mfanyakazi wa Afya ya Jamii kama mbadala wa huduma sawa katika mazingira ya kawaida. ILOS hii inaweza kufaa kwa washirika wanaohitaji ushauri wa tiba wa kuzuia magonjwa na/au upunguzaji wa sababu ya hatari, mafunzo na ukuzaji wa ujuzi, au huduma pana za usaidizi wa jamii.

- Huduma za Mfanyakazi wa Afya ya Jamii zinazotolewa katika mazingira mbadala au kwa kutumia mpangilio usio wa kawaida wa kutoza bili.
- Mfano wa ILOS: Uratibu wa mifumo ya huduma kwa ajili ya washirika kutoka kwa Wafanyakazi wa Afya ya Jamii (CHW) katika mazingira ya jamii, kama vile makazi au Huduma Zinazofaa kwa Utamaduni na Lugha kutoka kwa mashirika ya huduma za kijamii ambayo yanaweza au kutoweza kutoza bili yenyewe kwa huduma. Huduma zinazotolewa kuwasaidia Washirika kufikia sehemu tofauti za mfumo wa huduma za afya, kuwezesha kuhudhuria kwa Mshirika katika miadi ya matibabu na mingine, kuchangia kwa timu ya huduma/upangaji wa huduma, kueleza maelezo ya afya na huduma za afya, na kusaidia kuelewa mahitaji na kupata huduma.

Mpango wa Kitaifa wa Kuzuia Kisukari kama mbadala wa Huduma za Mpango wa Kitaifa wa Kuzuia Kisukari. ILOS hii inaweza kufaa kwa Washirika walio katika hatari ya kupata aina ya 2 ya kisukari.

- Mpango wa Kitaifa wa Kuzuia Kisukari unaotolewa katika mazingira ya jamii, kama vile ukumbi wa mazoezi ya mwili wa jamii au maktaba ya jamii pamoja na mazingira ya kliniki ya afya unaotoa huduma za ana kwa ana au za mtandaoni.
- Mfano wa ILOS: Utoaji wa Mpango wa Kitaifa wa Kuzuia Kisukari (National DPP) kutoka kwa shirika la uwasilishaji wa mpango linalotambuliwa na Centers for Disease Control and Prevention (CDC). *ILOS hii huwezesha utoaji wa National DPP kutoka kwa mashirika ya jamii ambayo hayana miundombinu ya kutoza bili lakini vinginevyo yanayostahiki kuwa watoaji wa DPP.*

Ushauri wa Kunyonyesha kama mbadala wa ushauri wa kawaida wa kunyonyesha ambao hautimizi mahitaji ya washirika. ILOS hii inaweza kufaa kwa watu ambao wamejifungua na mtoto wao mchanga wanaohitaji ushauri wa kunyonyesha ambao kwa kawaida hutolewa ofisini au katika mazingira mengine yasiyohusisha kulazwa hospitalini.

- Ushauri wa Kunyonyesha unaotolewa katika mazingira mbadala au kwa kutumia mpangilio wa kutoza bili usio wa kawaida.
- Mfano wa ILOS: Ushauri unaotolewa na muuguzi aliyesajiliwa, Mfanyakazi wa Afya wa Kawaida, au Doula aliye na mafunzo ya kunyonyesha (kama vile mshauri aliyethibitishwa wa elimu ya kunyonyesha, au mafunzo ya mtaalamu wa kunyonyesha aliyethibitishwa), katika mazingira ya jamii ambaye anaweza au kutoweza kutoza bili mwenyewe kwa huduma hizo.

Kuamua ikiwa ILOS inakufaa ni juhudi ya timu. Tunashirikiana na timu yako ya huduma ili kufanya uchaguzi bora. Uchaguzi, hata hivyo, ni wako. Si lazima ushiriki katika yoyote kati ya mipango hii. Washirika watajulishwa mapema kwa siku 30 ikiwa ILOS wanayopokea itakomeshwa. Notisi hii itajumuisha maelezo ya nung'uniko na rufaa kwa huduma zinazolipiwa na bima ambazo zimekataliwa zote au kwa sehemu (tazama ukurasa wa 81 kwa maelezo zaidi kuhusu manung'uniko na rufaa). Ikiwa una maswali yoyote kuhusu mafao au huduma zozote zilizo hapo juu, piga simu kwa 877-600-5472 (TTY: 877-600-5473).

Huduma Zinazohusiana na Afya

Huduma Zinazohusiana na Afya (HRS) ni huduma za ziada ambazo Trillium Community Health Plan hutoa. HRS husaidia kuimarisha afya na ustawi wa jumla wa mshirika na jamii. HRS ni huduma zinazobadilika kulingana na hali za washirika na mipango ya manufaa ya jamii kwa ajili ya washirika na jamii ya jumla. Mpango wa HRS wa Trillium Community Health Plan husaidia katika matumizi bora zaidi ya fedha ili kushughulikia sababu za hatari za kijamii, kama mahali unakoishi, ili kuimarisha ustawi wa jamii. Pata habari zaidi kuhusu huduma zinazohusiana na afya katika www.oregon.gov/oha/HPA/dsi-tc/Pages/Health-Related-Services.aspx.

Huduma Zinazobadilika Kulingana na Hali

Huduma zinazobadilika kulingana na hali ni usaidizi wa bidhaa au huduma za kuwasaidia washirika kuwa na afya njema au kuendelea kuwa na afya njema. Trillium Community Health Plan hutoa huduma hizi zinazobadilika kulingana na hali:

- Usaidizi wa chakula, kama vile uwasilishaji wa mboga na matunda, vocha za chakula, au milo iliyopangwa kulingana na mahitaji ya tiba.
- Usaidizi wa muda mfupi wa makazi, kama vile amana za kodi ya nyumba ili kusaidia kwa gharama za kuhama, usaidizi wa kodi ya nyumba kwa kipindi kifupi cha wakati, au ada za kuweka huduma za matumizi ya nyumbani
- Makazi au hifadhi ya muda huku ukipata nafuu kutokana na kulazwa hospitalini
- Bidhaa zinazoweza mwenendo mwema, kama vile viatu au mavazi ya michezo ya riadha
- Simu za mkononi au vifaa vya kufikia huduma ya afya kwa vifaa vya mawasiliano au programu za afya
- Bidhaa nyingine zinazokufanya uendeleo kuwa na afya njema, kama vile kiyoyozi au kichujio cha kusafisha hewa

Mfano wa Huduma nyingine Zinazobadilika Kulingana na Hali:

- Mipango/Huduma za Afya na Mazoezi ya Mwili
- Huduma za Usafirishaji au Mafuta/Matengenezo ya Gari
- Vyombo Saidizi, Vifaa vya Usaidizi, Vipengele vya Ufikiaji

Pata habari zaidi kuhusu huduma zinazobadilika kulingana na hali za Trillium Community Health Plan katika www.trilliumohp.com/members/oregon-health-plan/Benefits-and-Services/Flexible-Services.html

Mipango ya Manufaa ya Jamii

Mipango ya manufaa ya jamii ni huduma na usaidizi kwa washirika na jamii ya jumla ili kuimarisha afya na ustawi wa jamii.

Katika Trillium, usawa wa afya ni muhimu kwetu. Tunaamini kwamba kila mtu anapaswa kuwa na ufikiaji kwa huduma kamili za afya. Tunawasikiliza washirika wa jamii zetu za ndani.

Tunabainisha wanachohitaji. Tunakuza ushirikiano na mashirika ya jamii (CBOs) ili kusaidia kutimiza mahitaji haya. Hili linaweza kuwa kuwaunganisha watu kwa huduma za afya ya mwili. Pia linaweza kuwa kuwaunganisha watu kwa nyenzo za chakula, makazi na usafirishaji (magari ya usafiri). Baadhi ya mipango yetu ya manufaa ya jamii ni:

- Kufadhili stoo za chakula na ufikiaji kwa vyakula maalum vya kitamaduni
- Kuunda maeneo salama zaidi ya kujifunza
- Kuwekeza katika miradi ya kampeni ya mitaji ili kujenga upya vituo vya jamii vya ndani
- Kupanua timu ya Wafanyakazi wa Afya wa Kawaida (THW), Wafanyakazi wa Afya ya Jamii (CHW) na Doula

Mifano ya mipango mingine ya manufaa ya jamii ni:

- Madarasa ya elimu ya wazazi na usaidizi wa familia
- Mipango ya jamii ambayo husaidia familia kufikia matunda na mboga bora kupitia masoko ya wakulima
- Maboresho halisi ya usafirishaji, kama vile leni salama za baiskeli na njia za watembea kwa miguu.
- Mipango ya shuleni ambayo huwezesha mazingira ya kuelimisha ili kuimarisha afya ya jamii na kihisia na mafunzo ya kielimu ya wanafunzi
- Mafunzo ya walimu na mashirika ya jamii ambayo ni maalum kwa watoto kuhusu desturi zinazoelewa kiwewe

Jinsi ya kupata huduma zinazohusiana na afya kwa ajili yako au mwanafamilia

Unaweza kushirikiana na mtoa huduma wako kuomba Huduma Zinazohusiana na Afya. Pia unaweza kupigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja simu kwa 877-600-5472. Waombe wakutumie fomu ya ombi kwa lugha au muundo unaofaa kwa mahitaji yako.

Maamuzi ya kuidhinisha au kukataa maombi ya huduma zinazobadilika kulingana na hali hufanywa kwa msingi wa kila kesi. Ikiwa ombi lako la huduma inayobadilika kulingana na hali litakataliwa, utapata barua. Huwezi kukata rufaa kwa huduma inayobadilika kulingana na hali iliyokataliwa, lakini una haki ya kutoa lalamiko. Pata habari zaidi kuhusu rufaa na malalamiko katika ukurasa wa 92.

Ikiwa una OHP na unatatizika kupata huduma, tafadhali wasiliana na Mpango wa Wachunguzi wa Malalamiko ya Umma wa OHA. Wachunguzi wa Malalamiko ya Umma ni watetezi wa washirika wa OHP na watafanya kadiri wawezavyo ili kukusaidia. Tafadhali tuma barua pepe kwa OHA.OmbudsOffice@odhsoha.oregon.gov au uache ujumbe katika 877-642-0450.

Nyenzo nyingine ya usaidizi na huduma katika jamii yako ni 211 Info. Piga simu kwa 2-1-1 au uende katika tovuti ya [211 Info](#) kwa usaidizi.

Huduma za Jamii za Afya ya Kinywa

Tunajivunia kuwasaidia washirika wanaopata huduma za afya ya kinywa katika mazingira ya jamii. Mipango ya Meno inaweza kutuma wataalamu wa usafi wa meno wenye kibali maalum shuleni, Women Infants Children (WIC), Head Start, Ofisi za matibabu, vituo vya huduma za muda mrefu na maeneo mengine ya jamii kufanya tathmini za afya ya kinywa. Pia hutoa baadhi ya huduma za kuzuia magonjwa wakiwa huko, kama floridi, vanishi na tiba ya kufunika meno kwa watoto walio na umri wa kwenda shuleni na kuwasaidia watu kuelewa jinsi ya kutunza meno yao.

Katika maeneo ambapo hatuna mtaalamu wa usafi wa kufanya hivi, tunashirikiana na mashirika mengine. Huduma unazopata katika jamii zinapaswa kuwa za bila malipo kwako ikiwa zinalipiwa na bima katika mpango wako. Ikiwa huna uhakika, unaweza kumuuliza mtu anayetoa huduma hizo, au unaweza kupigia Kitengo cha Huduma kwa Washirika simu.

Maeneo ya Ufikiaji Huru

Katika maeneo mengi ndani ya Oregon, tuna mikataba maalum na Vituo vya Afya Vinavyofadhiliwa na Shirikisho (FQHC), Vituo vya Afya vya Jamii vya Kijijini (RCHC), Watoa Huduma wa Huduma za Afya za Kihindi (IHCP) na kliniki za Huduma za Afya za Kihindi (IHS). Mikataba hii maalum huruhusu washirika wetu kuhudumiwa na aina hizi za vituo bila kukabidhiwa kwa kituo hicho na bila rufaa.

Ikiwa ungependa kupokea huduma zako za afya ya kinywa katika mojawapo ya aina hizi za vituo, unaweza kupigia kituo hicho simu na uulize ikiwa wanashirikiana na Trillium Community Health Plan kama “Eneo la Ufikiaji Huru”. Pia unaweza kupigia Kitengo cha Huduma kwa Washirika simu na uombe orodha ya sasa ya Maeneo ya Ufikiaji Huru katika eneo lako.

Usafiri wa bila malipo kwenda kupata huduma

Usafiri wa bila malipo kwenda kwenye miadi kwa washirika wote wa Trillium Community Health Plan.

Ikiwa unahitaji usaidizi wa kufika kwenye miadi, pigia MTM (Usimamizi wa Usafirishaji wa Kimatibabu) simu kwa usafiri wa bila malipo. Unaweza kupata usafiri wa bila malipo kwenda kwa ziara yoyote ya afya ya mwili, meno, famasia, au afya ya mwenendo inayolipiwa na Trillium Community Health Plan.

Wewe au mwakilishi wako anaweza kuomba usafiri. Tunaweza kukupatia tikiti ya basi, pesa za teksi, au kutuma dereva akuchukue. Tunaweza kulipa pesa za gesi kwako, mwanafamilia, au rafiki ili akupeleke kwa gari. Hakuna gharama kwako kwa huduma hii. Trillium Community Health Plan haitakutoza kamwe bili kwa usafiri kuelekea na kutoka kwa huduma zinazolipiwa na bima.

Ratibu usafiri.

Pigia MTM (Usimamizi wa Usafirishaji wa Kimatibabu) simu kwa 877-583-1552 Watumiaji wa TTY, tafadhali piga simu kwa 711

Saa: Jumatatu hadi Jumapili, saa 8:00 asubuhi hadi saa 5:00 jioni. Kufungwa katika sikukuu: Sikukuu ya Mwaka Mpya, Sikukuu ya Kumbukumbu, Sikukuu ya Uhuru, Sikukuu ya Wafanyakazi, Sikukuu ya Shukrani na Sikukuu ya Krismasi.

Tafadhali piga simu angalau siku 2 za kazi kabla ya miadi ili kuratibu usafiri. Hili litasaidia kuhakikisha kwamba tunaweza kutimiza mahitaji yako ya usafiri.

Iwapo usafiri utambwa chini ya siku mbili (2) kabla ya muda ulioratibiwa wa kuchukuliwa, Mkandarasi au udalali wake wa NEMT wenye kandarasi ndogo utampatia Mshirika nambari ya simu ya udalali huo na unaweza, lakini si lazima, kumpatia Mshirika jina na nambari ya simu ya dereva wa NEMT au Mtoa Huduma wa NEMT.

Unaweza kupata usafiri katika siku sawa au inayofuata. Tafadhali pigia MTM (Usimamizi wa Usafirishaji wa Kimatibabu) simu.

Wewe au mtu unayemjua anaweza kupanga zaidi ya usafiri mmoja kwa wakati kwa miadi mingi. Unaweza kuratibu usafiri wa miadi ya siku zijazo mapema kwa hadi siku 90.

Cha kutarajia unapopiga simu.

MTM (Usimamizi wa Usafirishaji wa Kimatibabu) ina wafanyakazi wa kituo cha simu za usaidizi wanaoweza kukusaidia kwa lugha unayopendelea na kwa njia unayoweza kuelewa. Usaidizi huu ni wa bila malipo.

Wakati wa kwanza utakapopiga simu tutakwambia kuhusu mpango na kuzungumza kuhusu mahitaji yako ya usafiri. Tutauliza kuhusu uwezo wako wa kimwili na ikiwa utahitaji mtu wa kusafiri nawe.

Unapopiga simu kuratibu usafiri, tutaomba:

- Jina lako kamili.
- Anwani yako na nambari yako ya simu.

- Tarehe yako ya kuzaliwa.
- Jina la daktari au kliniki unayohitaji kutembelea.
- Tarehe ya miadi.
- Wakati wa miadi.
- Wakati wa kuchukuliwa baada ya miadi.
- Ikiwa unahitaji m hudumu wa kukusaidia.
- Mahitaji mengine yoyote maalum (kama kiti cha magurudumu au mnyama wa usaidizi).

Tutakagua ili kuona ikiwa unatumia Trillium Community Health Plan na ikiwa miadi yako ni ya huduma inayolipiwa na bima. Utapata maelezo zaidi kuhusu usafiri wako ndani ya saa 24. Utapata maelezo kuhusu ombi lako la usafiri kwa njia unayochagua (kupigiwa simu, barua pepe, faksi).

Kuchukuliwa na kufikishwa.

Utapata jina na nambari ya kampuni ya usafiri au dereva kabla ya miadi yako. Dereva wako atawasiliana nawe angalau siku 2 kabla ya usafiri wako ili kuthibitisha maelezo. Atakuchukua katika wakati wako ulioratibiwa. Tafadhali fika kwa wakati unaofaa. Ukichelewa, atasubiri kwa dakika 15 baada ya wakati wako ulioratibiwa. Hilo linamaanisha ikiwa usafiri wako umeratibiwa kufanyika saa 10 asubuhi, atakusubiri hadi saa 10:15 asubuhi.

Tutakufikisha kwa miadi yako angalau dakika 15 kabla ya kuanza.

- **Miadi ya kwanza ya siku:** Tutakufikisha si zaidi ya dakika 15 kabla ya ofisi kufunguliwa.
- **Miadi ya mwisho ya siku:** Tutakuchukua si zaidi ya dakika 15 baada ya ofisi kufungwa isipokuwa ikiwa miadi haitarajiwi kuisha ndani ya dakika 15 baada ya kufunga.
- **Kuomba wakati zaidi:** Lazima uombe kuchukuliwa mapema au kufikishwa baadaye kuliko nyakati hizi. Mwakilishi, mzazi au mlezi wako pia anaweza kutuomba.
- **Piga simu ikiwa huna wakati wa kuchukuliwa:** Ikiwa hakuna wakati ulioratibiwa wa kuchukuliwa kwa safari yako ya kurudi, tupigie simu wakati uko tayari. Dereva wako atafika ndani ya saa 1 baada ya simu yako.

MTM (Usimamizi wa Usafirishaji wa Kimatibabu) ni mpango wa kusafiri pamoja na watu wengine. Abiria wengine wanaweza kuchukuliwa na kushushwa njiani. Ikiwa una miadi kadhaa, unaweza kuombwa kuratibu katika siku sawa. Hili litatusaidia kufanya safari chache zaidi.

Unaweza kuomba kusafirishwa na rafiki au mwanafamilia kwa gari kwenda kwenye miadi. Anaweza kurejeshewa gharama zilizotumika (kulipwa) kwa maili anazoendesha gari.

Una haki na majukumu kama msafiri:

Una haki ya:

- Kupata usafiri salama na wa kutegemeka unaotimiza mahitaji yako.
- Kutendewa kwa heshima.
- Kuomba huduma za ukalimani unapozungumza na kitengo cha huduma kwa wateja.
- Kupata nyenzo kwa lugha au muundo unaotimiza mahitaji yako.
- Kupata notisi iliyoandikwa usafiri unapokataliwa.
- Kuwasilisha lalamiko kuhusu uzoefu wako wa usafiri.
- Kuomba rufaa, kuomba usikilizaji wa kesi, au kuomba vyote viwili ikiwa unahisi umenyimwa huduma ya usafiri bila haki.

Majukumu yako ni:

- Kuwatendea madereva na abiria wengine kwa heshima.
- Kutupigia simu mapema iwezekanavyo ili kuratibu, kubadilisha, au kubatilisha usafiri.
- Kutumia mikanda ya usalama na vifaa vingine vya usalama inavyohitajika kisheria (mfano: viti vya gari).
- Kuomba kukatiza safari katika sehemu za ziada, kama famasia, mapema.

Batilisha au ubadilishe usafiri wako.

Pigia MTM (Usimamizi wa Usafirishaji wa Kimatibabu) simu unapojua kwamba unahitaji kubatilisha au kuratibu upya usafiri wako, angalau saa 2 kabla ya wakati wa kuchukuliwa.

Unaweza kupigia MTM (Usimamizi wa Usafirishaji wa Kimatibabu) simu [Jumatatu hadi Jumapili, saa 8:00 asubuhi hadi saa 5:00 jioni. Acha ujumbe ikiwa huwezi kupiga simu wakati wa saa za kazi. Pigia MTM (Usimamizi wa Usafirishaji wa Kimatibabu) simu ikiwa una maswali au mabadiliko yoyote ya usafiri.

Unapokosa kufika.

“Kukosa kufika” ni wakati ambapo hauko tayari kuchukuliwa kwa wakati unaofaa. Dereva wako atasubiri kwa angalau dakika 15 baada ya wakati ulioratibiwa wa kuchukuliwa kabla ya kuondoka. Tunaweza kuweka vizuizi kwa usafiri wako wa siku zijazo ikiwa utakosa kufika mara nyingi sana.

Kuwa na kizuizi kunamaanisha tunaweza kuweka kikomo kwa idadi ya safari unazoweza kufanya, kukuwekea kikomo kwa dereva mmoja, au kuhitaji simu kabla ya kila usafiri.

Ikiwa usafiri wako utakataliwa.

Utapokea simu ya kukujulisha kwamba usafiri wako umekataliwa. Kukataliwa kwote hukaguliwa na wafanyakazi wawili kabla ya kutumwa kwako. Ikiwa usafiri wako utakataliwa, tutakutumia barua ya kukataliwa ndani ya saa 72 baada ya uamuzi huo. Notisi hiyo hueleza kanuni na sababu ya kukataliwa huko.

Unaweza kuomba rufaa kwa Trillium Community Health Plan ikiwa hukubaliani na kukataliwa huko. Una siku 60 kuanzia tarehe ya notisi ya kukataliwa kuomba rufaa. Baada ya rufaa, ikiwa kukataliwa huko kutadumishwa pia una haki ya kuomba Usikilizaji wa kesi wa jimbo.

Tutamtumia mtoa huduma wako barua pia ikiwa mtoa huduma huyo ni sehemu ya mtandao wetu wa watoa huduma na aliomba usafirishaji huo kwa niaba yako.

Una haki ya kutoa lalamiko au nung'uniko wakati wowote. Baadhi ya mifano ya lalamiko au nung'uniko ni:

- Wasiwasi kuhusu usalama wa gari
- Ubora wa huduma
- Miingiliano na madereva na watoa huduma (kama vile ufidhuli)
- Huduma ya usafiri iliyoombwa haikutolewa ilivyopangwa
- Haki za mtumiaji

Pata habari zaidi kuhusu malalamiko, manung'uniko, rufaa na usikilizaji wa kesi katika ukurasa wa 92.

Mwongozo wa Msafiri

Pata Mwongozo wa Msafiri wa MTM (Usimamizi wa Usafirishaji wa Kimatibabu) katika:

www.trilliumohp.com/members/oregon-health-plan/Benefits-and-Services/transportation.html.

Wewe au mwakilishi wako pia anaweza kupigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja simu kwa 877-600-5472 ili kuomba nakala ya karatasi ya bila malipo. Itatumwa ndani ya siku 5 za kazi. Nakala hiyo ya karatasi inaweza kuwa kwa lugha na muundo unaopendelea.

Mwongozo huo una maelezo zaidi, kama:

- Usaidizi wa viti vya magurudumu na uwezo wa kwenda.
- Usalama wa gari.
- Majukumu na kanuni za dereva.
- Cha kufanya katika dharura au ikiwa kuna hali mbaya ya hewa.
- Miadi ya umbali mrefu.
- Kurejeshwa kwa gharama za chakula na malazi.

Kupata huduma kwa video au simu.

Huduma ya afya kwa vifaa vya mawasiliano (inayojulikana pia kama tiba kwa vifaa vya mawasiliano au matibabu ya meno kwa vifaa vya mawasiliano) ni njia ya kupata huduma bila kwenda kwenye kliniki au ofisi. Huduma ya afya kwa vifaa vya mawasiliano inamaanisha unaweza kufanya miadi yako kwa simu au simu ya video. Trillium Community Health Plan italipia ziara za huduma ya afya kwa vifaa vya mawasiliano. Huduma ya afya kwa vifaa vya mawasiliano hukuruhusu kutembelea mtoa huduma wako kwa kutumia:


- Simu (sauti)
- Simu janja (sauti/video)
- Simu kibao (sauti/video)
- Kompyuta (sauti/video)

Hizi zote ni za bila malipo. Ikiwa huna ufikiaji kwa mtandao au video, zungumza na mtoa huduma wako kuhusu kitakachokufaa.

Jinsi ya kupata watoa huduma wa afya kwa vifaa vya mawasiliano.

Si watoa huduma wote wana machaguo ya huduma ya afya kwa vifaa vya mawasiliano. Unapaswa kuuliza kuhusu huduma ya afya kwa vifaa vya mawasiliano unapopiga simu ili kupanga miadi yako. Pia unaweza kuangalia zana yetu ya utafutaji ya Find a Provider katika www.TrilliumOHP.com

Chagua sanduku la mtoa huduma wa huduma ya afya kwa vifaa vya mawasiliano ambalo limeonyeshwa katika picha iliyo hapa chini. Orodha hii haijakamilika hivyo unaweza pia kumpigia mtoa huduma wako simu ili kuuliza ikiwa anatoa huduma ya afya kwa vifaa vya mawasiliano.



What medical provider or facility are you looking for?
Search by name, specialty or location.

Name of provider or clinic

Name of [Appointments for medical care that can be done on the phone, text, and/or video are available.]

Include []

Telehealth provider *i*

Ikiwa una matatizo yoyote ya sauti au video katika ziara yako ya huduma ya afya kwa vifaa vya mawasiliano, tafadhali hakikisha unashirikiana na mtoa huduma wako.

Wakati wa kutumia huduma ya afya kwa vifaa vya mawasiliano:

Washirika wa Trillium Community Health Plan wanaotumia huduma ya afya ya vifaa vya mawasiliano wana haki ya kupata huduma za afya ya mwili, meno, na mwenendo wanazohitaji. Baadhi ya mifano ya wakati unapoweza kutumia huduma ya afya kwa vifaa vya mawasiliano ni:

- Wakati mtoa huduma wako anataka kufanya ziara nawe kabla ya kuchukua dawa iliyoagizwa na daktari.
- Huduma za ushauri.

- Ufuatiliaji kutoka kwa ziara ya ana kwa ana.
- Wakati una maswali ya kawaida ya matibabu.
- Ikiwa uko karantini au unakaa mbali na watu kutokana na ugonjwa.
- Ikiwa huna uhakika ikiwa unahitaji kwenda kwa kliniki au ofisi.

Huduma ya afya kwa vifaa vya mawasiliano haipendekezwi kwa dharura. Ikiwa unahisi kuwa maisha yako yamo hatarini, tafadhali pigia 911 au nenda kwenye chumba cha dharura kilicho karibu nawe zaidi. Tazama ukurasa wa 66 kwa orodha ya hospitali zilizo na vyumba vya dharura.

Ikiwa hujui mtoa huduma wako ana huduma au machaguo yapi ya huduma ya afya kwa vifaa vya mawasiliano, mpigie simu na uulize.

Ziara za huduma ya afya kwa vifaa vya mawasiliano ni za faragha.

Huduma za afya kwa vifaa vya mawasiliano zinazotolewa na mtoa huduma wako ni salama. Kila mtoa huduma atakuwa na mfumo wake mwenyewe wa ziara za huduma ya afya kwa vifaa vya mawasiliano, lakini kila mfumo lazima ufuate sheria.

Pata habari zaidi kuhusu faragha na Health Insurance Portability and Accountability Act (HIPAA) (HIPAA) katika ukurasa wa 11.

Hakikisha unapokea simu yako katika chumba cha faragha au mahali ambapo hakuna mtu anayeweza kusikiliza miadi yako na mtoa huduma wako.

Una haki ya:

- Kupata huduma za afya kwa vifaa vya mawasiliano kwa lugha unayohitaji.
- Kuwa na mtoa huduma anayeheshimu mahitaji yako ya utamaduni na lugha.
- Kupata huduma za ukalimani kutoka kwa mkalimani aliye na sifa zinazostahili na aliyethibitishwa. Pata habari zaidi katika ukurasa wa 4].
- Kupata ziara za ana kwa ana, si ziara za huduma ya afya kwa vifaa vya mawasiliano tu.
- Kupata usaidizi na kuwa na zana zinazohitajika kwa huduma ya afya kwa vifaa vya mawasiliano.

Kuzungumza na mtoa huduma wako kuhusu huduma ya afya kwa vifaa vya mawasiliano. Pia unaweza kupigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja simu kupitia 877-600-5472 (TTY 877-600-5473). Tunapatikana Jumatatu hadi Ijumaa, saa 8:00 asubuhi hadi saa 5:00 jioni.

Dawa zinazoagizwa na daktari.

Ikiwa unahitaji kuchukua dawa iliyoagizwa na daktari, unaweza kwenda kwa famasia yoyote iliyo katika mtandao wa Trillium Community Health Plan. Orodha ya famasia tunazoshirikiana nazo inaweza kupatikana katika sajili yetu ya watoa huduma katika: www.trilliumohp.com/find-a-provider.html.

Peleka kadi yako ya kitambulisho cha Trillium Community Health Plan na kadi yako ya kitambulisho cha Oregon Health kwenye famasia hiyo. Huenda usiweze kuchukua dawa iliyoagizwa na daktari bila kuwa nazo.

Dawazinazoagizwa na daktari ambazo zinalipiwa na bima.

Orodha ya dawa zinazoagizwa na daktari zinazolipiwa na Trillium Community Health Plan inapatikana katika:

www.trilliumohp.com/content/dam/centene/trillium/medicaid/pdfs/Trillium_OHP%20Formulary_Medicaid.pdf. Ikiwa huna uhakika ikiwa dawa yako ipo katika orodha yetu, tupigie simu ili tukusaidie kuangalia.

Ikiwa unahitaji idhini ya mapema kwa dawa iliyoagizwa na daktari, tutafanya uamuzi ndani ya saa 24. Ikiwa tunahitaji maelezo zaidi ili kufanya uamuzi, inaweza kuchukua saa 72.

Baadhi ya dawa ambazo mtoa huduma wako ameagiza zinaweza kutokuwa katika orodha yetu. Unaweza kutuomba kuilipia ondoleo la kipekee la masharti ya kawaida. Ikiwa unataka ondoleo la kipekee la masharti ya kawaida, mwambie mtoa huduma wako. Madaktari na wafamasia wetu wa Trillium Community Health Plan watakagua ondoleo hilo la kipekee la masharti ya kawaida kwa ajili ya uidhinishaji.

Ombi linapokataliwa, utapata barua kutoka kwa Trillium Community Health Plan. Barua hiyo itakuwa na haki za kukata rufaa na fomu ya ombi la rufaa unayoweza kutumia ikiwa hukubaliani na uamuzi wetu.

Pigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja cha Famasia cha Trillium Community Health Plan simu kwa 877-600-5472 (TTY: 844-600-5473) ikiwa una maswali.

Dawa zinazouzwa bila agizo la daktari (OTC).

Baadhi ya wawa zinazouzwa bila agizo la daktari (OTC) hulipiwa na Trillium Community Health Plan. Dawa za OTC ni zile unazoweza kununua katika duka au famasia yoyote bila agizo la daktari, kama vile aspirini. Ili Trillium Community Health Plan ilipie dawa hizi, utahitaji agizo la daktari kutoka kwa mtoa huduma wako. Leta agizo la daktari, pamoja na kadi ya kitambulisho cha Trillium Community Health Plan na kadi ya kitambulisho cha Oregon Health kwenye famasia wakati unachukua dawa ya OTC.

Famasia ya agizo la posta

Baadhi ya dawa zinaweza kutumwa kwa posta hadi kwa anwani yako ya nyumbani. Hii inaitwa famasia ya agizo la posta. Ikiwa unapata shida kwenda kwa famasia kuchukua dawa zako zilizoagizwa na daktari, hili linaweza kuwa chaguo zuri kwako. Washirika wa Trillium Community Health Plan wanaweza kutumia Agizo la Dawa la Posta kwa famasia ya agizo la posta kwa 1-800-552-6694. Ili kupata habari zaidi na kupanga famasia ya agizo la posta, pigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja cha Famasia cha Trillium Community Health Plan kwa 877-600-5472 (TTY: 877-600-5473).

OHP hulipia dawa za afya ya mwenendo.

Dawa nyingi zinazotumiwa kutibu maradhi ya afya ya mwenendo hulipiwa na OHP, si Trillium Community Health Plan. Famasia hutuma bili yako ya dawa iliyoagizwa na daktari moja kwa moja kwa OHP. Trillium Community Health Plan na mtoa huduma wako watakusaidia kupata dawa za afya ya mwenendo unazohitaji. Zungumza na mtoa huduma wako ikiwa una maswali. Pia unaweza kupigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja cha Trillium Community Health Plan kwa 877-600-5472.

Bima ya dawa kwa washirika walio na Medicare.

Trillium Community Health Plan na OHP hazilipii dawa ambazo hulipiwa na Medicare Part D.

Ikiwa unastahili kwa Medicare Part D lakini uchague kutojiandikisha, utalazimika kulipia dawa hizi. Ikiwa una Part D, onyesha kadi yako ya kitambulisho cha Medicare na kadi yako ya kitambulisho cha Trillium Community Health Plan katika famasia.

Ikiwa dawa yako hailipiwi na Medicare Part D, famasia yako inaweza kutoza Trillium Community Health Plan bili ili kuona ikiwa dawa hiyo inalipiwa chini ya OHP. Trillium Community Health Plan italipia huduma nyingine zote zinazolipiwa na bima.

Pata habari zaidi kuhusu mafao ya Medicare katika ukurasa wa 81.

Huduma tusizolipia.

Si huduma zote za matibabu zinalipwa na OHP au Trillium Community Health Plan. Unapohitaji huduma, zungumza na mtoa huduma wako wa msingi kuhusu machaguo. Ukichagua kupata huduma isiyolipwa na bima, unaweza kulazimika kulipa bili. Ofisi ya mtoa huduma inapaswa kukwambia ikiwa matibabu au huduma hailipwi na bima. Watakwambia inagharimu pesa ngapi.

Unalipa tu ukitia fomu sahihi kabla ya kupata huduma hiyo inayosema kwamba unakubali kuilipia. Fomu hiyo lazima itaje au kueleza huduma hiyo, kuorodhesha gharama iliyokadiriwa, na kujumuisha taarifa kwamba OHP hailipii huduma hiyo. Pata habari zaidi kuhusu bili katika ukurasa wa 76.

Daima wasiliana na Kitengo cha Huduma kwa Wateja cha Trillium Community Health Plan kwanza ili kujadili kinacholipwa na bima. Ikiwa utapata bili, tafadhali wasiliana na Kitengo cha Huduma kwa Wateja cha Trillium Community Health Plan mara moja.

Mifano ya baadhi ya huduma zisizolipwa na bima:

- Baadhi ya matibabu, kama dawa zinazouzwa bila agizo la daktari, kwa maradhi ambayo unaweza kutibu nyumbani au ambayo huona peke yake (homa, mafua yasiyo makali, sagamba, sugu, nk.)
- Upasuaji au matibabu ya kubadilisha sura ya mwonekano tu.
- Huduma za kukusaidia kupata ujauzito.
- Matibabu ambayo hayana ufanisi kwa ujumla.
- Orthodontiki, isipokuwa ili kutibu kaakaa lililopasuka miongoni mwa watoto.

Ikiwa una maswali kuhusu huduma zinazolipwa au zisizolipwa na bima, tafadhali wasiliana na Kitengo cha Huduma kwa Wateja cha Trillium Community Health Plan kwa 877-600-5472 (TTY 711).

Hospitali.

Tunashirikiana na hospitali zilizo hapa chini kwa huduma za kawaida za hospitali. Unaweza kupata huduma za matibabu ya dharura katika hospitali yoyote.

Hillsboro

Tuality Community Hospital

335 South East Eighth Avenue, Hillsboro, OR 97123
(503) 681-1111, Bila Kutozwa Ada: hakuna, TTY: hakuna
<https://tuality.org>

Portland

Oregon Health and Sciences University

3181 SW Sam Jackson Park Road, Portland, OR 97239
(503) 494-8311, TTY/TDD: 503-494-0550
www.ohsu.edu

Portland

OHSU Center for Health & Healing

3303 S Bond Avenue, Portland, OR 97239
(503) 494-4779, Bila Kutozwa Ada: hakuna, TTY: hakuna
www.ohsu.edu/visit/south-waterfront-campus

Portland

Portland Adventist Medical Center

10123 Southeast Market Street, Portland, OR 97216
(855) 691-9890, TTY: (503) 261-6610
www.adventisthealth.org/portland

Portland

Cedar Hills Hospital

10300 Southwest Eastridge Street, Portland, OR 97225
(503) 944-5000, Bila Kutozwa Ada: 877-703-8880
<https://cedarhillshospital.com>

Huduma za matibabu ya haraka.

Tatizo la haraka ni baya vya kutosha kutibiwa mara moja, lakini si baya vya kutosha kwa matibabu ya papo hapo katika chumba cha dharura. Matatizo haya ya haraka yanaweza kuwa ya mwili, mwenendo au meno.

Unaweza kupata huduma za matibabu ya haraka saa 24 kwa siku, siku 7 kwa wiki bila idhini ya mapema.

Huhitaji rufaa kwa huduma za matibabu ya haraka au ya dharura. Kwa orodha ya vituo vya matibabu ya haraka na kliniki za kwenda bila miadi tazama hapa chini.

Huduma za matibabu ya haraka ya mwili.

Baadhi ya mifano ya huduma za matibabu ya haraka ya mwili ni:

- Mikwaruzo ya ngozi isiyo na damu nyingi lakini inayoweza kuhitaji kushonwa.
- Mifupa iliyovunjika kidogo tu na kuvunjia katika vidole vya mikono na miguu.
- Kutenguka au kuteguka.

Ikiwa una tatizo la haraka, pigia mtoa huduma wako wa msingi (PCP) simu.

Unaweza kupiga simu wakati wowote, mchana au usiku, katika wikendi au sikukuu. Iambie ofisi ya PCP kwamba wewe ni mshirika wa Trillium Community Health Plan. Utapigiwa simu ndani ya dakika 30. Utapata ushauri au rufaa. Ikiwa huwezi kuwasiliana na PCP wako kuhusu tatizo la haraka au ikiwa PCP wako hawezi kukuhudumia mapema inavyofaa, nenda kwenye kituo cha huduma za matibabu ya haraka au kliniki ya kwenda bila miadi. Huhitaji miadi. Tazama orodha iliyo hapa chini ya kliniki za huduma za matibabu ya haraka na za kwenda bila miadi.

Ikiwa unahitaji usaidizi, pigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja cha Trillium Community Health Plan kwa 877-600-5472 (TTY: 877-600-5473).

Ikiwa hujui kama tatizo lako ni la haraka, piga simu kwenye ofisi ya mtoa huduma wako bado, hata kama imefungwa.

Unaweza kupata huduma ya kujibu ujumbe. Acha ujumbe na useme kwamba wewe ni mshirika wa Trillium Community Health Plan. Utapigiwa simu ndani ya dakika 60 ili kutathmini asili ya simu yako. Unaweza kupata ushauri au rufaa ya mahali pengine pa kupiga simu.

Pia unaweza kufikia Simu ya Ushauri wa Wauguzi ya Saa 24 kwa usaidizi kwa 844-647-9667.

Kwa ushauri na miadi isiyo ya haraka, tafadhali piga simu katika saa za kazi.

Vituo vya huduma za matibabu ya haraka na kliniki za kwenda bila miadi zilizo katika eneo la Trillium Community Health Plan ni:

Forest Grove

OHSU Tuality Healthcare Urgent Care Forest Grove

1809 Maple St. Forest Grove, OR 97116

(503) 369-6180, Bila Kutozwa Ada: hakuna, TTY: hakuna

Gresham

Adventist Health Urgent Care Gresham Station

831 NW Council Dr. Gresham, OR 97030

(503) 665-8176, Bila Kutozwa Ada: hakuna, TTY: hakuna

Hillsboro

Rose City Urgent Care and Family Practice

6110 B N Lombard Hillsboro, OR 97123

(503) 894-9005, Bila Kutozwa Ada: hakuna, TTY: hakuna

Hillsboro**Rose City Urgent Care and Family Practice**

9975 SW Frewing St. Hillsboro, OR 97123
(503) 894-9005, Bila Kutozwa Ada: hakuna, TTY: hakuna

Hillsboro**Tuality Urgent Care**

7545 SE Tualatin Valley Hwy Hillsboro, OR 97123]
(503) 681-4223, Bila Kutozwa Ada: hakuna, TTY: hakuna

Lake Oswego**AFC Urgent Care**

17437 Boones Ferry Rd. Lake Oswego, OR 97305
(503) 305-6262, Bila Kutozwa Ada: hakuna, TTY: hakuna

Molalla**Molalla Urgent Care**

861 W. Main St., Molalla, OR 97038
(503) 829-7344, Bila Kutozwa Ada: hakuna, TTY: hakuna

Portland**Adventist Health Urgent Care Parkrose**

1350 NE 122nd Ave. Portland, OR 97230
(503) 408-7008, Bila Kutozwa Ada: hakuna, TTY: hakuna

Portland**Adventist Health Urgent Care Rockwood**

18750 SE Stark St. Portland, OR 97233
(503) 408-7008 Bila Kutozwa Ada: hakuna, TTY: hakuna

Portland**AFC Urgent Care NE Portland**

7033 NE Sandy Blvd. Portland, OR 97213
(503) 305-6262, Bila Kutozwa Ada: hakuna, TTY: hakuna

Portland**Pacific Crest Children's Urgent Care**

6924 NE Sandy Blvd. Portland, OR 97213
(503) 963-7963, Bila Kutozwa Ada: hakuna, TTY: hakuna

Portland**Portland Urgent**

4160 NE Sandy Blvd. Portland, OR 97212
(503) 249-9000, Bila Kutozwa Ada: hakuna, TTY: hakuna

Portland**Rose City Urgent Care and Family Practice Gateway**

135 NE 102nd Ave. Hillsboro, OR 97123
(503) 894-9005, Bila Kutozwa Ada: hakuna, TTY: hakuna

Sandy

Adventist Health Urgent Care Sandy

17055 Ruben Ln. Sandy, OR 97055

(503) 668-8002, Bila Kutozwa Ada: hakuna, TTY: hakuna

Huduma za matibabu ya haraka ya meno:

Baadhi ya mifano ya huduma za matibabu ya haraka ya meno ni pamoja na:

- Maumivu ya meno.
- Jino lililobambuka au kuvunjika.
- Kizibo au kijalizi cha jino kilichopotea.

Ikiwa una tatizo la haraka la meno, pigia daktari wako wa meno wa msingi (PCD) simu.

Ikiwa huwezi kuwasiliana na PCD wako au huna mmoja, pigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja cha Meno simu katika:

Advantage Dental Services

Kitengo cha Huduma kwa Wateja Bila kutozwa ada 1-866-268-9631 TTY: 711

Capitol Dental Care

Kitengo cha Huduma kwa Wateja 1-503-585-5205 au bila kutozwa ada 1-800-525-6800

TTY: 1-800-735-2900

Oregon Dental Service

Kitengo cha Huduma kwa Wateja 1-503-243-2987 au bila kutozwa ada 1-800-342-0526

TTY: 1-503-243-3958 au 1-800-466-6313

Watakusaidia kupata huduma za matibabu ya haraka ya meno, kulingana na hali yako.

Unapaswa kupata miadi ndani ya wiki 2, au wiki 1 ikiwa wewe ni mjamzito, kwa maradhi ya haraka ya meno.

Huduma za matibabu ya dharura

Pigia 911 ikiwa unahitaji gari la wagonjwa au nenda kwa chumba cha dharura ikiwa unafikiri uko hatarini. Dharura inahitaji huduma ya mara moja na huweka maisha yako hatarini. Inaweza kuwa jeraha la ghafla au ugonjwa wa ghafla. Dharura pia zinaweza kusababisha madhara kwa mwili wako. Ikiwa wewe ni mjamzito, dharura pia inaweza kusababisha madhara kwa mtoto wako.

Unaweza kupata huduma za matibabu ya haraka na ya dharura saa 24 kwa siku, siku 7 kwa wiki bila idhini ya mapema. Huhitaji rufaa.

Dharura za mwili

Huduma za matibabu ya dharura ya mwili ni wakati ambapo unahitaji huduma ya mara moja, na maisha yako yamo hatarini.

Baadhi ya mifano ya dharura za matibabu ni pamoja na:

- Mifupa iliyovunjika.
- Kutokwa na damu kusikokoma.
- Mshtuko wa moyo unaowezekana.
- Kupoteza fahamu.
- Matukutiko ya maungo.
- Maumivu makali.
- Kushindwa kupumua.
- Athari za mzio.

Maelezo zaidi kuhusu huduma za matibabu ya dharura:

- Pigia PCP wako simu au Kitengo cha Huduma kwa Wateja cha Trillium Community Health Plan ndani ya siku 3 baada ya kupokea huduma za matibabu ya dharura.
- Una haki ya kutumia hospitali yoyote au mazingira mengine, ndani ya Marekani.
- Dharura hulipiwa na bima ndani ya Marekani. Hailipiwi na bima ndani ya Meksiko au Kanada.
- Huduma za matibabu ya dharura hutoa huduma za baada ya hali kuimarika (huduma za baadaye). Huduma za baadaye ni huduma zinazolipiwa na bima zinazohusiana na maradhi ya dharura. Huduma hizi hutolewa kwako baada ya hali yako kuimarika. Husaidia kudumisha hali yako iliyoimarika. Husaidia kuboresha au kuponya tatizo lako la afya.

Tazama orodha ya hospitali zilizo na vyumba vya dharura katika ukurasa wa 66.

Dharura za meno

Dharura ya meno ni wakati ambapo unahitaji huduma za meno ndani ya siku sawa. Huduma hizi zinapatikana saa 24 kwa siku na siku 7 kwa wiki. Dharura ya meno inaweza kuhitaji matibabu ya mara moja. Baadhi ya mifano ni:

- Jino ambalo limeng'ooka.
- Una uvimbe au maambukizi mabaya kinywani.
- Una maumivu makali ya meno. Hii inamaanisha maumivu ambayo yanakuzuia kulala au yasiyokoma unapotumia dawa inayouzwa bila agizo la daktari kama aspirini au Tylenol.

Kwa dharura ya meno, tafadhali pigia daktari wako wa meno wa msingi (PCD) simu. Utahudumiwa ndani ya saa 24. Baadhi ya ofisi zina nyakati za kwenda kituoni kwa dharura bila miadi. Ikiwa huwezi kuwasiliana na PCD wako au huna mmoja, pigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja simu kwa 877-600-5472. Watakusaidia kupata huduma za matibabu ya dharura ya meno.

Ikiwa hakuna lolote kati ya machaguo haya linalokufaa, pigia 911 au utembelee Chumba cha Dharura. **Ikiwa unahitaji usafiri wa gari la wagonjwa, tafadhali pigia 911.** Tazama orodha ya hospitali zilizo na vyumba vya dharura katika ukurasa wa 66.

Mgogoro na dharura za afya ya mwenendo

Dharura ya afya ya mwenendo ni wakati ambapo unahitaji usaidizi mara moja ili kuhisi au kuwa salama. Ni wakati ambapo wewe au watu wengine wako hatarini. Mfano ni kuhisi huwezi kujidhibiti. Unaweza kuhisi kwamba usalama wako uko hatarini au kuwa na mawazo ya kujiumiza au kuwaumiza wengine.

Pigia 911 au uende kwenye chumba cha dharura ikiwa uko hatarini.

- Huduma za dharura za afya ya mwenendo hazihitaji rufaa au idhini ya mapema. Trillium Community Health Plan huwapatia washirika usaidizi na huduma za mgogoro baada ya dharura.
- Mtoa huduma wa afya ya mwenendo anaweza kukusaidia kupata huduma za kuboresha na kuimarisha afya ya akili. Tutajaribu kukuauni na kukusaidia baada ya mgogoro.

Nambari za ndani na saa 24 za mgogoro, vituo vya mgogoro vya kwenda bila miadi au kupeleka mtu

Unaweza kupiga simu, kutuma ujumbe au kupiga gumzo na 988. 988 ni simu ya usaidizi Unapotamani Kujitoa Uhai na wakati wa Mgogoro unakoweza kupata usaidizi unaokujali na wa huruma kutoka kwa washauri waliofunzwa wa mgogoro saa 24 kwa siku, siku 7 kwa wiki.

Wasiliani wa Mgogoro:

David Romprey Oregon Warmline
800-698-2392

Teen Line Warmline
800-852-8336

Senior Loneliness Line
800-282-7035

Kaunti ya Clackamas:

Crisis Line & Mental Health Urgent Walk-In
11211 SE 82nd Ave, Suite O
Happy Valley, Oregon 97086
503-655-8585

Clackamas Adult Protective Services
971-673-6655

Kaunti ya Multnomah

Crisis Line & Mental Health Urgent Walk-In
4212 SE Division St. Suite 100
Portland Oregon, 97206
800-716-9769
Foster Care Crisis Response and Coordination
503-575-3767

Multnomah Adult Protective Services
503-988-4450

Kaunti ya Washington

Crisis Line
503-291-9111

Washington Adult Protective Services
971-673-5200

Nyenzo za Jamii za Afya ya Akili

NAMI-Kaunti ya Clackamas *Kihispania kinapatikana
503-344-5050

NAMI-Kaunti ya Multnomah
503-228-5692

NAMI-Kaunti ya Washington
503-356-6835

Mgogoro wa afya ya mwenendo ni wakati unahitaji usaidizi haraka. Ukikosa kutibiwa, hali hiyo inaweza kuwa dharura. Tafadhali piga simu kwa mojawapo ya simu za ndani za saa 24 za mgogoro zilizo hapo juu au pigia 988 ikiwa unakabiliwa na lolote kati ya yafuatayo au huna uhakika ikiwa ni mgogoro. Tungependa kukuauni na kukusaidia kuzuia dharura.

Mifano ya mambo ya kuangalia ikiwa wewe au mwanafamilia anakabiliwa na dharura au mgogoro wa afya ya mwenendo:

- Kuzingatia kujitoa uhai.
- Kusikia sauti zinazokwambia ujumize au umuumize mtu mwingine.
- Kuumiza watu wengine, wanyama au kudhuru mali.
- Tabia hatari au zinazosumbua sana shuleni, kazini, au na marafiki au familia.

Hapa pana baadhi ya mambo ambayo Trillium Community Health Plan inaweza kufanya ili kuwezesha kuimarika katika jamii:

- Simu ya usaidizi wa mgogoro ya kupigia wakati mshirika anahitaji usaidizi
- Timu ya mgogoro inayoweza kwenda sehemu tofauti ambayo itaenda kwa mshirika anayehitaji usaidizi.
- Vituo vya mgogoro vya kwenda bila miadi au kupeleka mtu (tazama hapa chini)
- Huduma za kumtunza mtu anayekabiliwa na mgogoro ili mtunzaji wake wa kawaida apumzike (huduma za muda mfupi)
- Maeneo ya kuishi kwa muda mfupi ili kuimarika
- Huduma za baada ya kuimarika na huduma za matibabu ya haraka. Huduma hizi zinapatikana saa 24 kwa siku na siku 7 kwa wiki. Huduma za Baada ya Kuimarika ni huduma zinazolipiwa na bima, zinazohusiana na dharura ya matibabu au afya ya mwenendo, ambazo hutolewa baada ya dharura kuimarika na ili kudumisha kuimarika kwa hali au kuponya tatizo hilo la afya.
- Huduma za kushughulikia mgogoro kwa washirika wanaopokea matibabu ya uangalizi makini ya nyumbani kwa afya ya mwenendo saa 24 kwa siku.

Tazama maelezo zaidi kuhusu huduma za afya ya mwenendo zinazotolewa katika ukurasa wa 32.

Uzuiaji wa kujitoa uhai

Ikiwa una ugonjwa wa akili na ukose kuutibu, unaweza kuhatarisha kujitoa uhai. Kwa matibabu sahihi, maisha yako yanaweza kuboreka.

Ishara za kawaida za onyo la kujitoa uhai

Pata usaidizi ikiwa utagundua ishara zozote kwamba wewe au mtu unayemjua anafikiri kuhusu kujitoa uhai. Angalau 80% ya watu wanaofikiri kuhusu kujitoa uhai wanataka usaidizi. Unahitaji kuchukulia ishara za onyo kwa uzito.

Hapa pana baadhi ya ishara za onyo la kujitoa uhai:

- Kuzungumza kuhusu kutaka kufa au kujiua.
- Kupanga njia ya kujiua, kama vile kununua bunduki.
- Kuhisi huna tumaini au kutokuwa na sababu ya kuishi.
- Kuhisi umenaswa au unahisi uchungu usioweza kuvumilika.
- Kuzungumza kuhusu kuwa mzigo kwa wengine.
- Kupatia watu mali ya thamani.
- Kufikiri na kuzungumza sana kuhusu kifo.
- Kutumia pombe au mihadarati zaidi.
- Kuwa na mahangaiko au mwenye wasiwasi.
- Kufanya mambo bila hadhari.
- Kujitenga na watu au kuhisi umetengwa.
- Kuwa na mabadiliko makubwa mno ya hali ya kihisia.

Usiwahi kufanya mawazo wala mazungumzo kuhusu kujitoa uhai kuwa siri!

Pia unaweza kupata usaidizi kwa:

- Kubonyeza 988 – ni nambari ya simu ya tarakimu tatu ya taifa zima ya kuunganisha moja kwa moja kwa 988 Suicide and Crisis Lifeline. Kwa kupiga simu au kutuma ujumbe kwa 988, utaungana na wataalamu wa afya ya akili ambao wanaweza kukusaidia.
- Kutafuta nambari ya mgogoro wa afya ya akili ya kaunti yako mtandaoni. Wanaweza kufanya uchunguzi na kukusaidia kupata huduma unazohitaji. Kwa orodha ya simu za ziada za usaidizi wa mgogoro tazama ukurasa wa 72 au nenda kwenye www.TrilliumOHP.com.

Huduma za ufuatiliaji baada ya dharura

Baada ya dharura, unaweza kuhitaji huduma za ufuatiliaji. Hii ni pamoja na kitu chochote unachohitaji baada ya kuondoka kwenye chumba cha dharura. Huduma za ufuatiliaji si dharura. OHP hailipii huduma za ufuatiliaji wakati ambapo hupo jimboni. Pigia ofisi ya mtoa huduma wako wa msingi au daktari wa meno simu ili kupanga huduma zozote za ufuatiliaji.

- Lazima upate huduma za ufuatiliaji kutoka kwa mtoa huduma wako wa kawaida au daktari wako wa kawaida wa meno. Unaweza kumwomba daktari wa dharura ampigie mtoa huduma wako simu ili kupanga huduma za ufuatiliaji.

- Pigia mtoa huduma wako au daktari wako wa meno simu haraka iwezekanavyo baada ya kupata huduma za matibabu ya haraka au ya dharura. Mwambie mtoa huduma wako au daktari wako wa meno ulikotibiwa na sababu.
- Mtoa huduma wako au daktari wako wa meno atasimamia huduma zako za ufuatiliaji na kuratibu miadi ikiwa unahitaji miadi.

Huduma mbali na nyumbani

Huduma zilizopangwa nje ya jimbo

Trillium Community Health Plan itakusaidia kutafuta mtoa huduma wa nje ya jimbo na kulipia huduma inayolipiwa na bima wakati:

- Unahitaji huduma ambayo haipatikani ndani ya Oregon
- Au ikiwa huduma hiyo ni ya bei nafuu

Huduma za matibabu ya dharura mbali na nyumbani

Unaweza kuhitaji huduma za matibabu ya dharura wakati uko mbali na nyumbani au nje ya eneo la huduma la Trillium Community Health Plan. **Pigia 911 au nenda kwa chumba chochote cha dharura.** Huhitaji idhini ya mapema kwa huduma za dharura. Huduma za matibabu ya dharura hulipiwa na bima Marekani kote, hii ni pamoja na maradhi ya afya ya mwenendo na ya dharura ya meno. Hatulipii huduma nje ya Marekani, ikiwa ni pamoja na ndani ya Kanada na Meksiko.

Usilipie huduma za matibabu ya dharura. Ukilipa bili ya chumba cha dharura, Trillium Community Health Plan hairuhusiwi kukurejeshea malipo hayo. Tazama ukurasa wa 76 kwa unachopaswa kufanya ikiwa utatozwa bili.

Tafadhali fuata hatua zilizo hapa chini ikiwa unahitaji huduma za matibabu ya dharura mbali na nyumbani

1. Hakikisha kwamba una Kadi yako ya Kitambulisho cha Oregon Health na kadi yako ya Kitambulisho cha Trillium Community Health Plan unaposafiri nje ya jimbo.
2. Waonyeshe Kadi yako ya Kitambulisho cha Trillium Community Health Plan na uwaombe kutoza Trillium Community Health Plan bili.
3. Usitie hati zozote sahihi hadi utakapojua kwamba mtoa huduma huyo atatoza Trillium Community Health Plan bili.
4. Unaweza kuomba kwamba ofisi ya kutoza bili ya Chumba cha Dharura au mtoa huduma iwasiliane na Trillium Community Health Plan ikiwa wanataka kuthibitisha bima yako au wana maswali yoyote.
5. Tafadhali pigia PCP wako simu ikiwa unahitaji huduma zisizo za dharura mbali na nyumbani.

Wakati wa dharura, hatua zilizo hapo juu haziwezekani kila wakati. Kuwa umejiandaa na kujua ni hatua zipi za kuchukua kwa huduma za matibabu ya dharura nje ya jimbo kunaweza kutatua

matatizo ya utozaji wa bili wakati uko mbali. Hatua hizi zinaweza kusaidia kukuzuia kutozwa bili kwa huduma ambazo Trillium Community Health Plan inaweza kulipia. Trillium Community Health Plan haiwezi kulipia huduma ikiwa mtoa huduma hajatutumia bili.

Bili za huduma

Washirika wa OHP hawalipi bili za huduma zinazolipiwa na bima.

Unapopanga ziara yako ya kwanza kwa mtoa huduma, iambie ofisi hiyo kuwa unatumia Trillium Community Health Plan. Wajulishe ikiwa una bima nyingine, pia. Hili litamsaidia mtoa huduma kujua wa kutoza bili. Peleka kadi yako ya kitambulisho kwenye ziara zote za matibabu.

Hakuna mtoa huduma wa ndani ya mtandao wa Trillium Community Health Plan au mtu anayemfanyia kazi anaweza kumtoza mshirika bili, kutuma bili ya mshirika kwa shirika la kukusanya madeni, au kufungua dai la kiraia dhidi ya mshirika ili kupata pesa zozote ambazo Trillium Community Health Plan inadaiwa kwa huduma usizowajibikia kwa mtoa huduma aliyepewa kandarasi.

Washirika hawawezi kutozwa bili kwa miadi ambayo haikuhudhuriwa au makosa.

- Miadi ambayo haikuhudhuriwa si huduma ya OHP (Medicaid) na haitozwi bili kwa mshirika au OHP.
- Ikiwa mtoa huduma wako atakosa kutuma hati sahihi au kukosa kupata idhini, huwezi kupata bili kwa hilo. Hili linaitwa kosa la mtoa huduma.

Washirika hawawezi kutozwa bili ya salio au bili isiyotarajiwa.

Mtoa huduma anapotoza bili kwa kiasi kinachosalia cha bili, hilo linaitwa kutoza bili ya salio. Pia linaitwa bili isiyotarajiwa. Kiasi hicho ni salio kati ya kiasi halisi kilichotozwa kwa bili na kiasi ambacho Trillium Community Health Plan hulipa. Hili hufanyika mara nyingi unapotembelea mtoa huduma wa nje ya mtandao. Washirika hawawajibikii gharama hizi.

Ikiwa una maswali, pigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja simu kwa 877-600-5472. Kwa maelezo zaidi kuhusu kutozwa bili isiyotarajiwa nenda kwenye

<https://dfr.oregon.gov/Documents/Surprise-billing-consumers.pdf>.

Ikiwa mtoa huduma wako atakutumia bili, usiilipe.

Pigia Trillium Community Health Plan simu kwa usaidizi mara moja kwa 877-600-5472, (TTY 711).

Pia unaweza kupiga simu kwa ofisi ya kutoza bili ya mtoa huduma wako na uhakikishe wanajua kwamba una OHP.

Kunaweza kuwa na huduma ambazo lazima ulipie.

Kwa kawaida, ukiwa na Trillium Community Health Plan, hutalazimika kulipa bili zozote za matibabu. Wakati mwingine, hata hivyo, unalazimika kulipa.

Lazima umlipe mtoa huduma ikiwa:

- **Utapata huduma za kawaida nje ya Oregon.** Utapata huduma nje ya Oregon ambazo si za matibabu ya haraka au ya dharura.
- **Utakosa kumwambia mtoa huduma kwamba una OHP.** Hukumwambia mtoa huduma kuwa una Trillium Community Health Plan, bima nyingine au ulitoa jina ambalo halikulingana na lile lililo kwenye Kitambulisho cha Trillium Community Health Plan wakati wa au baada ya huduma kutolewa, hivyo mtoa huduma hakuweza kutoza Trillium Community Health Plan bili. Lazima watoa huduma wathibitisha ustahiki wako wa Trillium Community Health Plan wakati wa huduma na kabla ya kutoza bili au kuchukua malipo. Lazima wajaribu kupata maelezo ya bima kabla ya kukutoza bili.
- **Utaendelea kupata huduma iliyokataliwa.** Wewe au mwakilishi wako aliomba kuendelezwa kwa mafao wakati wa mchakato wa rufaa na usikilizaji wa kwa kesi ya pingamizi, na uamuzi wa mwisho haukukuunga mkono. Utalazimika kulipa ada zozote zitakazotowazwa kwa huduma zilizokataliwa mnamo au baada ya tarehe ya kutekelezwa iliyo katika notisi ya hatua au notisi ya uamuzi wa rufaa.
- **Utapata pesa kwa huduma kutoka kwa ajali.** Ikiwa mlipaji wa mhusika mwingine, kama vile bima ya gari, alikutumia hundi kwa huduma ulizopata kutoka kwa mtoa huduma wako na hukutumia hundi hizi kumlipa mtoa huduma huyo.
- **Hatushirikiani na mtoa huduma huyo.** Unapochagua kutembelea mtoa huduma ambaye hayuko ndani ya mtandao wa Trillium Community Health Plan unaweza kulazimika kulipia huduma zako. Kabla ya kutembelea mtoa huduma ambaye hayuko ndani ya mtandao wa Trillium Community Health Plan, unapaswa kupigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja simu au ushirikiane PCP wako, idhini ya awali inaweza kuhitajika au kunaweza kuwa na mtoa huduma ndani ya mtandao anayeweza kutosheleza mahitaji yako.
- **Utachagua kupata huduma zisizolipiwa na bima.** Lazima ulipe unapochagua kupata huduma ambazo mtoa huduma anakwambia hazilipiwi na Trillium Community Health Plan. Katika hali hii:
 - Huduma ni kitu ambacho mpango wako haulipii.
 - Kabla ya kupata huduma hiyo, unatia sahihi fomu halali ya Makubaliano ya Kulipa. Pata habari zaidi kuhusu fomu hiyo hapa chini.

Unaweza kuombwa kutia sahihi fomu ya Makubaliano ya Kulipa.

Fomu ya makubaliano ya kulipa hutumiwa wakati ambapo unataka huduma ambayo hailipiwi na Trillium Community Health Plan au OHP. Fomu hiyo pia inaitwa ondoleo. Unaweza kutazama nakala ya fomu hiyo katika <https://bit.ly/OHPwaiver>.

Yafuatayo lazima yawe ukweli kwa fomu hiyo ya Makubaliano ya Kulipa kuwa halali:

- Fomu hiyo lazima iwe na gharama iliyokadiriwa ya huduma hiyo. Hii lazima iwe sawa na iliyo katika bili.
- Huduma hiyo imeratibiwa ndani ya siku 30 kuanzia tarehe uliyotia fomu sahihi.
- Fomu hiyo inasema kwamba OHP hailipii huduma hiyo.
- Fomu hiyo inasema unakubali kulipa bili hiyo mwenyewe.
- Uliomba kulipia binafsi huduma inayolipiwa na bima. Ukichagua kufanya hivi, mtoa huduma anaweza kukutoza bili ikiwa atakwambia yafuatayo mapema:
 - Huduma hiyo inalipiwa na bima na Trillium Community Health Plan itamlipa vikamilifu kwa huduma inayolipiwa na bima.
 - Gharama iliyokadiriwa, ikiwa ni pamoja na ada zote zinazohusiana, kiasi ambacho Trillium Community Health Plan ingelipa kwa huduma hiyo. Mtoa huduma hawezi kukutoza kiasi kinachozidi kile ambacho Trillium Community Health Plan ingelipa; na,
 - Kwa kujua na hiari unakubali kulipia huduma inayolipiwa na bima.
- Mtoa huduma atarekodi kwa maandishi, yaliyotiwa sahihi nawe au mwakilishi wako, kwamba alikupatia taarifa iliyo hapa juu, na:
 - Alikupatia nafasi ya kuuliza maswali, kupata taarifa zaidi, na kushauriana na mfanyakazi wako wa kesi au mwakilishi wako.
 - Unakubali kulipa binafsi. Wewe au mwakilishi wako ametia sahihi makubaliano ambayo yana taarifa zote za malipo ya binafsi.
 - Mtoa huduma huyo lazima akupatie nakala ya makubaliano yaliyotiwa sahihi. Mtoa huduma huyo hawezi kuwasilisha dai kwa Trillium Community Health Plan kwa huduma inayolipiwa na bima ambayo imeorodheshwa katika makubaliano hayo.

Bili za huduma za matibabu ya dharura mbali na nyumbani au nje ya jimbo

Kwa sababu baadhi ya watoa huduma wa dharura wa nje ya mtandao hawajui kanuni za OHP (Medicaid) ya Oregon, wanaweza kukutoza bili. Wasiliana na Kitengo cha Huduma kwa Wateja cha Trillium Community Health Plan ikiwa utapata bili. Tunaweza kuwa na nyenzo za kusaidia ikiwa umetozwa bili kimakosa.

Tupigie simu mara moja ikiwa utapata bili zozote kutoka kwa watoa huduma wa nje ya jimbo. Watoa huduma wengine hutuma bili ambazo hazijalipwa kwa mashirika ya kukusanya madeni na hata wanaweza kufungua mashtaka mahakamani ili kulipwa. Ni vigumu zaidi kutatua tatizo hilo pindi hilo linapofanyika. Punde tu unapopokea bili:

- Usipuuze bili za matibabu.
- Wasiliana na Kitengo cha Huduma kwa Wateja cha Trillium Community Health Plan haraka iwezekanavyo kwa 877-600-5472 (TTY: 877-600-5473).
Saa: Jumatatu hadi Ijumaa, saa 8:00 asubuhi hadi saa 5:00 jioni.
- Ikiwa utapata hati za mahakama, tupigie simu mara moja. Pia unaweza kupigia wakili simu au Simu ya Usaidizi ya Mafao ya Umma kwa 800-520-5292 kwa ushauri wa kisheria wa bila malipo. Kuna sheria za mtumiaji ambazo zinaweza kukusaidia unapotozwa bili kimakosa huku ukitumia OHP.
- Ikiwa ulipata bili kwa sababu dai lako lilikataliwa na Trillium Community Health Plan, wasiliana na Kitengo cha Huduma kwa Wateja. Pata habari zaidi kuhusu kukataliwa, haki zako, na unachopaswa kufanya ikiwa hukubaliani nasi katika ukurasa wa 92.

Vidokezo muhimu kuhusu kulipia huduma na bili.

- Tunakuhimiza kwa dhati upigie Kitengo cha Huduma kwa Wateja simu kabla ya kukubali kumlipa mtoa huduma.
- Ikiwa mtoa huduma wako atakuomba ulipe malipo ya mshiriki, usiyalipe! Waombe wafanyakazi wa ofisi hiyo kupigia Trillium Community Health Plan simu.
- Trillium Community Health Plan hulipia huduma zote zinazolipiwa na bima kwa mujibu wa Orodha Yenye Vipaumbele ya Huduma za Afya, tazama ukurasa wa 26.
- Kwa orodha fupi ya mafao na huduma ambazo hulipiwa na bima chini ya mafao yako ya OHP katika Trillium Community Health Plan, ambayo pia hulipia usimamizi wa kesi na uratibu wa huduma, tazama ukurasa wa 45. Ikiwa una maswali yoyote kuhusu kinacholipiwa na bima, unaweza kumuuliza PCP wako au upigie kitengo cha huduma kwa wateja cha Trillium Community Health Plan.
- Hakuna mtoa huduma wa ndani ya mtandao wa Trillium Community Health Plan au mtu anayemfanyia kazi anaweza kumtoza mshirika bili, kutuma bili ya mshirika kwa shirika la kukusanya madeni, au kufungua dai la kiraia dhidi ya mshirika ili kupata pesa zozote ambazo Trillium Community Health Plan inadaiwa kwa huduma usizowajibikia.

- Washirika hawatozwi kamwe kwa usafiri kwenda kwenye miadi inayolipiwa na bima. Tazama ukurasa wa 57. Washirika wanaweza kuomba kurejeshewa gharama zilizotumika kuendesha gari kuelekea kwa ziara zinazolipiwa na bima au kupata pasi za basi ili kutumia basi kuelekea kwa ziara zinazolipiwa na bima.
- Ulinzi dhidi ya kutozwa bili kwa kawaida hutumika tu ikiwa mtoa huduma wa matibabu alijua au alipaswa kujua kuwa ulikuwa na OHP. Pia, unatumika tu kwa watoa huduma wanaoshirikiana na OHP (lakini watoa huduma wengi hufanya hivyo).
- Wakati mwingine, mtoa huduma wako anakosa kujaza hati inavyofaa. Hili linapofanyika, huenda asilipwe. Hilo halimaanishi kwamba unapaswa kulipa. Ikiwa tayari umepata huduma hiyo na tukatae kumlipa mtoa huduma wako, mtoa huduma wako bado hawezi kukutoza bili.
- Unaweza kupata notisi kutoka kwetu inayosema kwamba hatutalipia huduma hiyo. Notisi hiyo haimaanishi kwamba unapaswa kulipa. Mtoa huduma atapuza malipo hayo.
- Ikiwa Trillium Community Health Plan au mtoa huduma wako atakwambia kwamba huduma hiyo hailipiwi na OHP, bado una haki ya kupinga uamuzi huo kwa kuwasilisha rufaa na kuomba usikilizaji wa kesi. Tazama ukurasa wa 92.
- Endapo Trillium Community Health Plan itafungwa, huwajibiki kulipia huduma tunazolipia au tunazotoa.

Wanachama walio na OHP na Medicare.

Watu wengine wana OHP (Medicaid) na Medicare kwa wakati mmoja. OHP hulipia baadhi ya vitu ambavyo Medicare hailipii. Ikiwa una zote mbili, Medicare ndiyo bima yako kuu ya afya. OHP inaweza kulipia vitu kama dawa ambazo Medicare hailipii.

Ikiwa una zote mbili, huwajibikii:

- Ada za malipo ya mshiriki
- Makato au
- Bima ya ushirikiano kwa huduma za Medicare, ada hizo hulipwa na OHP.

Unaweza kuhitajika kulipa malipo ya mshiriki kwa baadhi ya gharama za dawa zinazoagizwa na daktari.

Kuna nyakati ambapo unaweza kulazimika kulipa makato, bima ya ushirikiano au malipo ya mshiriki ukichagua kutembelea mtoa huduma nje ya mtandao. Wasiliana na ofisi ya eneo lako ya Aging and People with Disabilities (APD) au Area Agency on Aging (AAA). Watakusaidia kupata habari zaidi kuhusu jinsi ya kutumia mafao yako. Pigia Aging and Disability Resource Connection (ADRC) simu kwa 855-673-2372 ili kupata nambari ya simu ya ofisi ya eneo lako ya APD au AAA.

Pigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja simu ili kupata habari zaidi kuhusu ni mafao yapi hulipiwa na Medicare na OHP (Medicaid), au ili kupata usaidizi wa kutafuta mtoa huduma na jinsi ya kupata huduma.

Watoa huduma watatoza Medicare yako na Trillium Community Health Plan bili.

Trillium Community Health Plan hushirikiana na Medicare na ina makubaliano kwamba madai yote yatatumwa ili tuweze kulipa.

- Mpatie mtoa huduma nambari yako ya kitambulisho cha OHP na umwambie kwamba unapata bima kutoka kwa Trillium Community Health Plan. Ikiwa bado anasema unadaiwa pesa, pigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja simu kwa 877-600-5472, (TTY 877-600-5473). Tunaweza kukusaidia.
- Pata habari kuhusu nyakati chache ambapo mtoa huduma anaweza kukutumia bili katika ukurasa wa 76.

Washirika walio na Medicare wanaweza kubadilisha au kuondoka kwenye shirika la CCO wanalotumia kwa huduma za matibabu ya mwili wakati wowote. Hata hivyo, wanachama walio na Medicare lazima watumie CCO kwa huduma za meno na afya ya mwenendo.

Kubadilisha CCOs na kuhamisha huduma

Una haki ya kubadilisha CCOs au kuondoka kwenye CCO ikiwa una sababu iliyoidhinishwa.

Ikiwa huna CCO, OHP yako inaitwa Fee-For-Service au kadi huru. Hii huitwa “ada kwa huduma” kwa sababu jimbo huwalipa watoa huduma ada kwa kila huduma wanayotoa. Washirika wa Fee-for-service hupata aina sawa za mafao ya huduma za afya ya mwili, meno, na mwenendo kama washirika wa CCO.

Wakati ambapo unapoweza kubadilisha au kuondoka kwenye CCO.

Shirika la CCO ulilo nalo linategemea unakoishi. Baadhi ya maeneo ya zaidi ya CCO moja. Katika maeneo hayo, kuna kanuni kuhusu wakati ambapo unaweza kubadilisha shirika lako la CCO. Unaweza kuchagua kubadilisha au kukatisha uandikishaji (kuondoka) katika nyakati hizi:

- Ndani ya siku 30 ikiwa:
 - Hutaki mpango ulikoandikishwa, au
 - Uliomba mpango fulani na jimbo likakuweka katika mpango tofauti.
- Ndani ya siku 90 za kwanza baada ya kujiunga na CCO, au
 - Ikiwa jimbo litakutumia barua ya “bima” inayosema kwamba wewe ni sehemu ya CCO baada ya tarehe yako ya kuanza, basi una siku 90 baada ya tarehe ya barua hiyo.
- Baada ya kuwa katika CCO sawa kwa miezi 6.
- Unapowezesha upya OHP yako.
- Ikiwa utapoteza OHP kwa chini ya miezi 2, ukiandikishwa upya katika CCO, na ulikosa nafasi yako ya kuchagua CCO wakati ambapo ungewezesha upya OHP yako.
- Wakati ambapo shirika la CCO limesimamishwa kwa muda kuongeza washirika wapya.
- Angalau mara moja kwa kila miezi 12 ikiwa machaguo yaliyo hapo juu hayatumiki.

Ikiwa lolote kati ya yafuatayo litafanyika, unaweza kubadilisha au kuondoka wakati wowote:

- Shirika hilo la CCO lina makatazo ya kimaadili au kidini kuhusu huduma unayotaka.
- Una sababu ya kimatibabu. Wakati huduma zinazohusiana hazipatikani ndani ya mtandao na mtoa huduma wako anasema kupata huduma hizo kando kutamaanisha hatari isiyohitajika. Mfano: Upasuaji wa kujifungua na utaratibu wa kufunga mirija ya uzazi kwa wakati mmoja.
- Sababu nyingine ikiwa ni pamoja na, lakini si tu, huduma duni, ukosefu wa ufikiaji kwa huduma zinazolipiwa na bima, au ukosefu wa ufikiaji kwa watoa huduma wa mtandao ambao wana uzoefu katika mahitaji yako mahususi ya huduma za afya.

- Ukihama kutoka kwa eneo la huduma.
 - Ikiwa utahamia eneo ambalo shirika lako la CCO halihudumii, unaweza kubadilisha mipango punde tu ukiambia OHP kuhusu kuhama huko. Tafadhali pigia OHP simu kwa 800-699-9075 au utumie akaunti yako ya mtandaoni katika ONE.Oregon.gov.
- Ikiwa utapoteza OHP kwa chini ya miezi 2, ukiandikishwa upya katika CCO, na ulikosa nafasi yako ya kuchagua CCO wakati ambapo ungewezesha upya OHP yako.
- Huduma hazitolewi kwa lugha unayopendelea.
- Huduma hazitolewi kwa njia inayofaa kitamaduni; au
- Uko katika hatari ya kukosa huduma endelevu.

Watu wengine wanaweza kuomba kubadilisha au kuondoka kwenye CCO wakati wowote. Washirika hawa ni:

- Washirika walio na Medicare na OHP (Medicaid) wanaweza kubadilisha au kuondoka kwenye shirika la CCO wanalotumia kwa huduma za matibabu ya mwili wakati wowote. Hata hivyo, wanachama walio na Medicare lazima watumie CCO kwa huduma za meno na afya ya mwenendo.
- Mmarekani wa Kihindi na Mzaliwa wa Alaska aliye na ithibati ya Urithi wa Kihindi anayetaka kupata huduma kwingineko. Anaweza kupata huduma kutoka kwa kituo cha Huduma za Afya za Kihindi, kliniki/mpango wa afya wa kikabila, au kliniki ya mjini na OHP fee-for-service.

Unaweza kuuliza kuhusu machaguo haya kwa simu au maandishi. Tafadhali pigia Kitengo cha OHP cha Huduma za Wateja simu kwa 800-273-0557 au utume barua pepe kwa Oregon.Benefits@odhsoha.oregon.gov.

Jinsi ya kubadilisha au kuondoka kwenye shirika lako la CCO

Mambo ya kuzingatia: Trillium Community Health Plan inataka kuhakikisha unapokea huduma bora zaidi zinazoweza. Trillium Community Health Plan inaweza kukupatia huduma fulani ambazo FFS au kadi huru haiwezi. Wakati ambapo una tatizo la kupata huduma zinazofaa, tafadhali turuhusu tujaribu kukusaidia kabla ya kuondoka kwenye Trillium Community Health Plan.

Ikiwa bado ungependa kuondoka, lazima kuna shirika jingine la CCO linalopatikana katika eneo lako la huduma la kubadilisha mpango wako.

Ambia OHP ikiwa unataka kubadilisha au kuondoka kwenye shirika lako la CCO. Wewe na/au mwakilishi wako anaweza kupigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja cha OHP simu kwa 800-699-9075 au 800-273-0557 (TTY 711) kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa, saa 8 asubuhi hadi saa 5 jioni, majira ya PT. Tumia akaunti yako ya mtandaoni katika ONE.Oregon.gov au utume barua pepe kwa Oregon.Benefits@odhsoha.oregon.gov.

Unaweza kupata huduma huku ukibadilisha shirika lako la CCO. Tazama ukurasa wa 82 ili kupata habari zaidi.

Trillium Community Health Plan inaweza kukuomba uondoke kwa sababu fulani.

Trillium Community Health Plan inaweza kuomba OHA ikuondoe kwenye mpango wetu ikiwa:

- Unadhulumu watu, huna ushirikiano, au unawasumbua wafanyakazi au watoa huduma wetu. Isipokuwa wakati ambapo tabia hiyo inatokana na hitaji lako la huduma maalum za afya au ulemavu.
- Ukifanya ulaghai au vitendo vingine haramu, kama vile kumruhusu mtu mwingine kutumia mafao yako ya huduma za afya, kubadilisha agizo la dawa la daktari, wizi, au vitendo vingine vya uhalifu.
- Unazua vurugu au kutoa vitisho vya vurugu. Hii inaweza kuelekezwa kwa mtoa huduma wa afya, wafanyakazi wake, wagonjwa wengine, au wafanyakazi wa Trillium Community Health Plan. Wakati kitendo au tishio la vurugu linakwaza sana uwezo wa Trillium Community Health Plan wa kutoa huduma ama kwako au washirika wengine.

Lazima tuombe jimbo (Oregon Health Authority) kukagua na kuidhinisha kukuondoa kwenye mpango wetu. Utapata barua ikiwa ombi la CCO la kukatisha kuandikishwa kwako (kukuondoa) limeidhinishwa. Unaweza kutoa lalamiko ikiwa hujaridhishwa na mchakato huo au ikiwa hukubaliani na uamuzi huo. Tazama ukurasa wa 92 kwa jinsi ya kutoa lalamiko au kuomba rufaa.

Trillium Community Health Plan haiwezi kuomba kukuondoa kwenye mpango wetu kwa sababu ya sababu zinazohusiana na (lakini si tu):

- Hali yako ya afya inazidi kuwa mbaya.
- Hutumii huduma.
- Unatumia huduma nyingi.
- Unakaribia kutumia huduma au kuwekwa katika kituo cha huduma (kama vile kituo cha huduma za muda mrefu au Kituo cha Makazi cha Matibabu ya Magonjwa ya Akili)
- Tabia ya mahitaji maalum ambayo inaweza kuwa sumbufu au ya kutoshirikiana.
- Jamii yako inayolindwa, maradhi au historia inamaanisha kuwa yamkini utahitaji huduma nyingi katika siku zijazo au huduma ghali katika siku zijazo.
- Ulemavu wako wa kimwili, uwezo wa kufikiri, ukuaji au wa akili.
- Uko chini ya malezi ya ODHS Child Welfare.
- Ukitoa lalamiko, kutokubali uamuzi, kuomba rufaa au usikilizaji wa kesi.
- Ukifanya uamuzi kuhusu huduma zako ambao Trillium Community Health Plan haikubaliani nao.

Kwa maelezo zaidi au maswali kuhusu sababu nyingine zinazoweza kufanya kuandikishwa kwako kukatishwe, vighairi vya kuandikishwa vya muda au maondoleo ya kuandikishwa, pigia Trillium Community Health Plan simu kwa 877-600-5472 au Kitengo cha Huduma za Wateja cha OHP kwa 800-273-0557.

Utapata barua iliyo na haki zako za kukatishwa kwa uandikishaji angalau siku 60 kabla ya kuhitaji kuwezesha upya OHP yako.

Huduma huku ukibadilisha au kuondoka kwenye CCO

Washirika wengine wanaobadilisha mipango bado wanaweza kupata huduma sawa, bima ya dawa zinazoagizwa na daktari na kuhudumiwa na watoa huduma sawa hata kama si ndani ya mtandao. Hilo linamaanisha huduma hazitabadilika unapobadilisha CCOs au kuhama kutoka kwa OHP fee-for-service hadi kwa CCO. Hili wakati mwingine huitwa “Mabadiliko ya Huduma.”

Ikiwa una matatizo makubwa ya afya, mpango wako mpya na mpango wako wa zamani lazima ishirikiane ili kuhakikisha unapata matibabu na huduma unazohitaji.

Je, nani anaweza kupata huduma sawa huku akibadilisha mipango?

Usaidizi huu ni wa washirika ambao wana matatizo makubwa ya afya, wanaohitaji huduma za hospitali, au huduma za afya za kulazwa hospitalini kwa matatizo ya kiakili. Hapa ni orodha ya baadhi ya mifano ya wale wanaoweza kupata usaidizi huu:

- Washirika ambao wanahitaji huduma za hatua ya mwisho ya ugonjwa wa figo.
- Watoto dhaifu kiafya.
- Washirika wa mpango wa matibabu ya saratani ya matiti na mlango wa kizazi.
- Wanachama wanaopata usaidizi wa Care Assist kutokana na VVU/UKIMWI.
- Washirika waliopandikiziwa sehemu ya mwili.
- Washirika ambao ni wajaawazito au wamejifungua mtoto tu.
- Washirika wanaopata matibabu ya saratani.
- Mshirika yeyote ambaye asipopata huduma endelevu anaweza kupata madhara makubwa kwa afya yake au kuwa katika hatari ya kuhitaji huduma za hospitali au taasisi.

Kipindi cha wakati ambacho huduma hii hudumu ni:

- Siku 90 kwa washirika ambao wana Medicare na OHP (Medicaid).
- Kwa washirika wengine, kipindi chochote cha wakati ambacho ni kifupi zaidi:
 - Siku 30 kwa afya ya mwili na kinywa na siku 60 kwa afya ya mwenendo, au
 - Hadi PCP mpya wa mshirika akipitia mpango wake wa huduma.

Trillium Community Health Plan itahakikisha kwamba washirika wanaohitaji huduma sawa huku wakibadilisha mipango wanapata:

- Ufikiaji endelevu kwa huduma na usafiri kwenda kupata huduma.
- Kuruhusu huduma kutoka kwa mtoa huduma wao hata kama hayupo katika mtandao wa Trillium Community Health Plan hadi moja kati ya yafuatayo yafanyike:
 - o Mpangilio wa chini zaidi au ulioidhinishwa wa matibabu yaliyoagizwa na daktari unakamilika, au
 - o Mtoa huduma anayefanya ukaguzi akiamua kwamba huduma hiyo haihitajiki tena kimatibabu. Ikiwa huduma inatolewa na mtaalamu, mpango wa matibabu utakaguliwa na mtoa huduma aliye na sifa zinazostahili.
- Aina fulani za huduma zitaendelea hadi zikamilike na mtoa huduma wa sasa. Aina hizi za huduma ni:
 - o Huduma kabla na baada ya kupata ujauzito/kujifungua mtoto (za kabla na baada ya kujifungua).
 - o Huduma za kupandikiziwa sehemu ya mwili hadi mwaka wa kwanza baada ya kupandikizwa huko.
 - o Tibamiali au tibakemikali (matibabu ya saratani) kwa mpangilio wake wa matibabu.
 - o Dawa zilizo na mpangilio wa chini zaidi wa matibabu uliofafanuliwa ambao unazidi vipindi vya wakati vya mabadiliko ya huduma vilivyo hapo juu.

Unaweza kupata nakala ya Sera ya Uratibu wa Huduma ya Trillium Community Health Plan, pigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja simu kwa 877-600-5472. Pia inapatikana katika tovuti yetu: www.trilliumohp.com/members/oregon-health-plan/Benefits-and-Services/care-coordination-and-case-management.html. Tafadhali pigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja simu ikiwa una maswali.

Maamuzi ya mwisho wa maisha.

Maagizo ya mapema.

Watu wazima wote wana haki ya kufanya maamuzi kuhusu huduma zao. Hii ni pamoja na haki ya kukubali na kukataa matibabu. Ugonjwa au jeraha linaweza kukuzuia kumwambia daktari wako, wanafamilia au mwakilishi wako kuhusu huduma unazotaka kupokea. Sheria ya Oregon inakuruhusu kutaja matakwa, imani, na melengo yako mapema, kabla ya kuhitaji aina hiyo ya huduma. Fomu unayotumia inaitwa **agizo la mapema**.

Agizo la mapema hukuruhusu:

- Kushiriki maadili, imani, malengo na matakwa yako ya huduma za afya ikiwa huwezi kuyaeleza mwenyewe.
- Kutaja mtu wa kufanya maamuzi yako ya huduma za afya ikiwa huwezi kuyafanya mwenyewe. Mtu huyu anaitwa mwakilishi wako wa huduma za afya na lazima akubali kufanya jukumu hili.

- Hukupatia haki ya kukataa au kukubali matibabu au upasuaji na haki ya kufanya maamuzi kuhusu huduma zako za tiba.

Jinsi ya kupata maelezo zaidi kuhusu Maagizo ya Mapema.

Tunaweza kukupatia kijitabu cha bila malipo kuhusu maagizo ya mapema. Kinaitwa “Kufanya Maamuzi ya Huduma za Afya”. Tupigie simu tu ili kupata habari zaidi, kupata nakala ya kijitabu hicho na fomu ya Agizo la Mapema. Pigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja cha Trillium Community Health Plan simu kwa 877-600-5472. Trillium Community Health Plan pia hutoa. Ili kupakua fomu ya Agizo la Mapema, tafadhali tembelea:

www.oregon.gov/oha/ph/about/pages/adac-forms.aspx

Pia unaweza kupata habari kuhusu maagizo ya mapema kwa kupigia Oregon Health Decisions simu kwa: **503-692-0894** au **800-422-4805** (Watumiaji wa TTY, tafadhali piga simu kwa 711). Saa: Jumatatu hadi Alhamisi, saa 9 asubuhi hadi saa 3 jioni, majira ya PT.

Kwa maelezo zaidi kuhusu sera na utaratibu wa Trillium Community Health Plan kuhusu Maagizo ya Mapema, tafadhali tembelea [www.trilliumohp.com/members/oregon-health-plan/formembers/Advance Directive.html](http://www.trilliumohp.com/members/oregon-health-plan/formembers/Advance_Directive.html)

Maelezo mengine muhimu kuhusu Maagizo ya Mapema

- Kujaza agizo la mapema ni uchaguzi wako. Ikiwa utachagua kutojaza na kutia sahihi agizo la mapema, bima yako au ufikiaji kwa huduma utasalia kuwa sawa tu.
- Hutahudumiwa kwa njia tofauti na Trillium Community Health Plan ukiamua kutojaza na kutia sahihi agizo la mapema.
- Ikiwa utajaza agizo la mapema, hakikisha unazungumza na watoa huduma wako na familia yako kulihusu na uwapatie nakala.
- Trillium Community Health Plan itaheshimu uchaguzi wowote ambao umeorodhesha katika Agizo lako la Mapema lililojazwa na kutiwa sahihi.

Jinsi ya kulalamika ikiwa Trillium Community Health Plan haikufuata masharti ya agizo la mapema.

Unaweza kutoa lalamiko kwa Health Licensing Office ikiwa mtoa huduma wako atakosa kufanya unachoomba katika agizo lako la mapema.

Health Licensing Office

503-370-9216 (Watumiaji wa TTY, tafadhali piga simu kwa 711)

Saa: Jumatatu hadi Ijumaa, saa 8 asubuhi hadi saa 5 jioni, majira ya PT.

Tuma lalamiko kwa barua kwa:

1430 Tandem Ave NE, Suite 180

Salem, OR 97301

Barua pepe: hlo.info@odhsoha.oregon.gov

Pigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja cha Trillium Community Health Plan simu kwa 877-600-5472 (TTY 711) ili kupata nakala ya karatasi ya fomu ya lalamiko.

Unaweza kupata fomu za malalamiko na kupata habari zaidi katika:

www.oregon.gov/oha/PH/HLO/Pages/File-Complaint.aspx.

Jinsi ya Kubatilisha Agizo la Mapema.

Ili kubatilisha, omba urudishiwe nakala za agizo lako la mapema na uzirarue. Pia unaweza kuandika LIMEBATILISHWA kwa maandishi makubwa, utie sahihi na kuzitia tarehe. Kwa maswali au maelezo zaidi, wasiliana na Oregon Health Decisions kwa 800-422-4805 au 503-692-0894 (TTY 711).

Je, kuna tofauti gani kati ya POLST na agizo la mapema?

Maagizo Yanayobebeka ya Matibabu ya Kuendeleza Maisha (POLST)

POLST ni fomu ya tiba unayoweza kutumia kuhakikisha kwamba matakwa yako ya matibabu karibu na mwisho wa maisha yanafuatwa na watoa huduma wa tiba. Huhitajiki kamwe kujaza POLST, lakini ikiwa una ugonjwa mbaya au sababu nyingine kwa nini hungetaka aina zote za matibabu, unaweza kupata habari zaidi kuhusu fomu hii.

POLST ni tofauti na Agizo la Mapema:

	Agizo la Mapema	POLST
Je, ni nini?	Hati ya kisheria	Agizo la tiba
Je, nani anaweza kuipata?	Kwa watu wazima wote walio na umri wa zaidi ya miaka 18	Mtu yeyote wa umri wowote aliye na ugonjwa mbaya
Je, mtoa huduma wangu anahitaji kuidhinisha/kutia sahihi?	Haihitaji idhini ya mtoa huduma	Inahitaji kutiwa sahihi na kuidhinishwa na mtoa huduma wa afya
Je, hutumiwa wakati upi?	Huduma au maradhi ya siku zijazo	Huduma na maradhi ya sasa

Ili kupata habari zaidi, tembelea: <https://oregonpolst.org/>

Barua pepe: polst@ohsu.edu au pigia Oregon POLST simu kwa 503-494-3965.

Tamko la Matibabu ya Afya ya Akili.

Oregon ina fomu ya kuandika matakwa yako ya huduma za afya ya akili. Fomu hiyo inaitwa Tamko la Matibabu ya Afya ya Akili. Fomu hiyo ni ya wakati ambapo una mgogoro wa afya ya akili, au huwezi kufanya maamuzi kuhusu matibabu yako ya afya ya akili. Una chaguo la kujaza fomu hii, wakati ambapo huna mgogoro, na unaweza kuelewa na kufanya maamuzi kuhusu huduma zako.

Je, fomu hii hunifanyia nini?

Fomu hiyo hueleza aina ya huduma unayotaka endapo utawahi kukosa uwezo wa kufanya maamuzi mwenyewe. Ni mahakama au madaktari wawili tu wanaweza kuamua ikiwa huwezi kufanya maamuzi kuhusu afya yako ya akili.

Fomu hii hukuruhusu kufanya uchaguzi kuhusu aina za huduma unazotaka na usizotaka. Inaweza kutumiwa kuchagua mtu mzima wa kufanya maamuzi kuhusu huduma zako. Mtu utakayemchagua sharti akubali kuzungumza kwa niaba yako na kufuata matakwa yako. Ikiwa matakwa yako hayajaandikwa, mtu huyu ataamua unachotaka.

Fomu ya tamko ni halali kwa miaka 3 pekee. Ikiwa utakosa uwezo wa kufanya maamuzi dani ya miaka hiyo 3, fomu yako itaanza kutumika. Itaendelea kutumika hadi ukiweza kufanya maamuzi tena. Unaweza kubatilisha tamko lako wakati ambapo unaweza kufanya uchaguzi kuhusu huduma zako. Lazima upeane fomu yako kwa PCP wako na mtu unayemchagua akufanyie maamuzi.

Ili kupata habari zaidi kuhusu Tamko la Matibabu ya Afya ya Akili, tembelea tovuti ya Jimbo la Oregon katika https://aix-xweb1p.state.or.us/es_xweb/DHSforms/Served/le9550.pdf

Ikiwa mtoa huduma wako atakosa kufuata matakwa yako yaliyo katika fomu yako, unaweza kulalamika. Fomu ya hili inapatikana katika www.healthoregon.org/hcrqi. Tuma lalamiko lako kwa:

Health Facility Licensing and Certification Program

800 NE Oregon Street, Suite 465

Portland, OR 97232

Barua pepe: mailbox.hclc@odhsosha.oregon.gov

FAKSI: (971) 673-0556

Kuripoti Ulaghai, Ufujaji, na Matumizi Mabaya.

Sisi ni mpango wa afya ya jamii, na tungependa kuhakikisha kuwa dola za huduma za afya zinatumiwa kuwasaidia washirika wetu kuwa na afya njema na vyema. Tunahitaji usaidizi wako ili kufanya hivyo.

Ikiwa unafikiri ulaghai, ufujaji, au matumizi mabaya yamefanyika ripoti hilo haraka uwezavyo. Unaweza kuripoti hilo bila kujulikana. Sheria za mfichua maovu huwalinda watu ambao huripoti ulaghai, ufujaji, na matumizi mabaya. Hutapoteza bima yako ukitoa ripoti. Ni kinyume cha sheria kunyanyasa, kutishia, au kubagua mtu anayeripoti ulaghai, ufujaji, au matumizi mabaya.

Ulaghai wa Medicaid ni kinyume cha sheria na Trillium Community Health Plan huchukulia hili kwa uzito.

Baadhi ya mifano ya ulaghai, ufujaji na matumizi mabaya ya mtoa huduma ni:

- Mtoa huduma kukutoza ada kwa huduma inayolipiwa na Trillium Community Health Plan
- Mtoa huduma kutoza bili kwa huduma ambazo hukupokea
- Mtoa huduma kukupatia huduma ambayo huhitaji kulingana na hali yako ya afya

Baadhi ya mifano ya ulaghai, ufujaji na matumizi mabaya ya mshirika ni:

- Kwenda kwa madaktari wengi kwa maagizo ya dawa kwa dawa ambayo tayari umeagiziwa na daktari
- Mtu kutumia kitambulisho cha mtu mwingine kupata mafao

Jinsi ya kutoa ripoti ya ulaghai, ufujaji na matumizi mabaya.

Unaweza kutoa ripoti ya ulaghai, ufujaji na matumizi mabaya kwa njia chache:

Piga simu, tuma faksi, au uwasilishe mtandaoni au uandikie Trillium Community Health Plan moja kwa moja. **Tunaripoti ulaghai, ufujaji na matumizi mabaya yote yanayoshukiwa yanayofanywa na watoa huduma au washirika kwa mashirika ya jimbo ambayo yameorodheshwa hapa chini.**

Pigia simu yetu ya usaidizi: 877-600-5472

Faksi: 844-805-3991

Wasilisha Ujumbe Salama: www.trilliumohp.com/login.html

Andikia: Trillium Community Health Plan

PO Box 11740

Eugene, OR 97440-3940

AU

Ripoti ulaghai, ufujaji na matumizi mabaya ya Mshirika kwa kupiga simu, kutuma faksi au kuandikia:

DHS Fraud Investigation Unit

P.O. Box 14150

Salem, OR 97309

Simu ya Usaidizi: 1-888-FRAUD01 (888-372-8301)

Faksi: 503-373-1525 Kumbuka: Simu ya Usaidizi

Tovuti: www.oregon.gov/oha/FOD/PIAU/Pages/Report-Fraud.aspx.

AU (mahususi kwa watoa huduma)

OHA Office of Program Integrity

3406 Cherry Avenue NE

Salem, OR 97303-4924

Simu ya Usaidizi: 1-888-FRAUD01 (888-372-8301)

Faksi: 503-378-2577

Tovuti: www.oregon.gov/oha/FOD/PIAU/Pages/Report-Fraud.aspx.

AU

Medicaid Fraud Control Unit (MFCU)

Oregon Department of Justice

100 SW Market Street

Portland, OR 97201

Simu: 971-673-1880

Faksi: 971-673-1890

Ili kuripoti ulaghai wa mteja na mtoa huduma mtandaoni:

www.oregon.gov/dhs/abuse/Pages/fraud-reporting.aspx

Trillium Community Health Plan imejitolea kwa dhati kuzuia ulaghai, ufujaji na matumizi mabaya. Tutafuata sheria zote zinazohusiana, ikiwa ni pamoja na Sheria ya Jimbo ya Madai ya Uongo na Sheria ya Shirikisho ya Madai ya Uongo.

Malalamiko, Manung'uniko, Rufaa na Usikilizaji wa Haki wa Kesi

Trillium Community Health Plan huhakikisha kwamba washirika wote wana ufikiaji kwa mfumo wa manung'uniko (malalamiko, manung'uniko, rufaa na usikilizaji wa kesi). Huwa tunajaribu kufanya iwe rahisi kwa washirika kuwasilisha lalamiko, nung'uniko, au rufaa na kupata taarifa kuhusu jinsi ya kuwasilisha usikilizaji wa kesi kwa Oregon Health Authority.

Tujulishe ikiwa unahitaji usaidizi katika sehemu yoyote ya mchakato wa lalamiko, nung'uniko, rufaa, na/au usikilizaji wa kesi. Pia tunaweza kukupatia taarifa zaidi kuhusu jinsi tunavyoshughulikia malalamiko/manung'uniko na rufaa. Nakala za kiolezo chetu cha notisi zinapatikana pia. Ikiwa unahitaji usaidizi au ungependa kupata taarifa zaidi ya kilicho katika mwongozo huu, wasiliana nasi kwa:

- Simu: 541-214-3948
- Pigia Mratibu wetu wa Manung'uniko simu kwa 877-600-5472
TTY: 877-600-5473
- Faksi: 844-805-3991
- Barua: Trillium Community Health Plan
PO Box 11740
Eugene, OR 97440-3940
- Barua pepe: Grievances@TrilliumCHP.com
- Wavuti: www.trilliumohp.com/members/oregon-health-plan/for-members/member-satisfaction.html

Unaweza kutoa lalamiko

- **Lalamiko** ni kutujulisha kwamba hujaridhika.
- **Pingamizi** ni wakati ambapo hukubaliani na Trillium Community Health Plan au mtoa huduma.
- **Nung'uniko** ni lalamiko unaloweza kutoa ikiwa hufurahishwi na Trillium Community Health Plan, huduma zako za afya, au mtoa huduma wako. Pingamizi pia inaweza kuwa nung'uniko.

Ili kufanya iwe rahisi, OHP hutumia neno **lalamiko** kwa manung'uniko na pingamizi, pia.

Una haki ya kutoa lalamiko ikiwa hujaridhishwa na sehemu yoyote ya huduma zako. Tutajaribu kuboresha mambo. Piga tu simu kwa Kitengo cha Huduma kwa Wateja kwa 877-600-5472, TTY: 877-600-5473. Pia unaweza kutoa lalamiko kwa OHA au Mchunguzi wa Malalamiko ya Umma. Unaweza kuwasiliana na OHA kwa 1-800-273-0557 au Mchunguzi wa Malalamiko ya Umma kwa 1-877-642-0450.

au

Andika:

Trillium Community Health Plan
PO Box 11756
Eugene, OR, 97440
Barua pepe: grievances@Trilliumchp.com

Faksi: 844-850-4861

Pia unaweza kupata fomu ya malalamiko katika www.trilliumohp.com/members/oregon-health-plan/for-members/member-satisfaction.html

Unaweza kuwasilisha lalamiko kuhusu suala lolote kando na kukataliwa kwa huduma au mafao na wakati wowote kwa kutamka au kwa maandishi. Ukiwasilisha lalamiko kwa OHA, litatumwa kwa Trillium Community Health Plan.

Mifano ya sababu unaweza kuwasilisha lalamiko ni:

- Matatizo ya kupanga miadi au kupata usafiri
- Matatizo ya kupata mtoa huduma karibu na unakoishi
- Kutohisi unaheshimiwa au kueleweka kwa watoa huduma, wafanyakazi wa mtoa huduma, madereva au Trillium Community Health Plan
- Huduma ambayo hukuwa na uhakika kuihusu, lakini ukaipokea hata hivyo
- Bili za huduma ambazo hukukubali kulipa
- Pingamizi kuhusu mapendekezo ya kurefusha muda wa kufanya maamuzi ya idhini ya Trillium Community Health Plan
- Usalama wa dereva au gari
- Ubora wa huduma uliyopokea

Mwakilishi au mtoa huduma wako anaweza kutoa (kuwasilisha) lalamiko kwa niaba yako, kwa ruhusa yako iliyoandikwa ya kufanya hivyo.

Tutapitia lalamiko lako na kukujulisha kinachoweza kufanywa haraka kadiri afya yako inavyohitaji. Hili litafanywa ndani ya siku 5 za kazi kuanzia siku ambayo tulipata lalamiko lako.

Ikiwa tunahitaji muda zaidi, tutakutumia barua ndani ya siku 5 za kazi. Tutakwambia sababu ya kuhitaji muda zaidi. Tutaomba tu muda zaidi ikiwa hilo linafaa kwa maslahi yako zaidi. Barua zote zitaandikwa kwa lugha unayopendelea. Tutakutumia barua ndani ya siku 30 baada ya wakati ambao tulipata lalamiko hilo inayoeleza jinsi tutakavyolishughulikia.

Ikiwa hujafurahishwa na jinsi tulivyoshughulikia lalamiko lako, unaweza kutoa habari kuhusu hilo kwa Kitengo cha Huduma za Wateja cha OHP kwa 1-800-273-0557 au tafadhali wasiliana na Mpango wa Wachunguzi wa Malalamiko ya Umma wa OHA. Wachunguzi wa Malalamiko ya Umma ni watetezi wa washirika wa OHP na watafanya kadiri wawezavyo ili kukusaidia. Tafadhali tumia OHA barua pepe. OHA.OmbudsOffice@odhsosha.oregon.gov au uache ujumbe katika 877-642-0450.

Nyenzo nyingine ya usaidizi na huduma katika jamii yako ni 211 Info. Piga simu kwa 2-1-1 au nenda katika tovuti ya www.211info.org kwa usaidizi.

Trillium Community Health Plan, makandarasi wake, makandarasi wadogo, na watoa huduma wanaoshiriki hawawezi:

- Kumzuia mshirika kutumia sehemu yoyote ya mchakato wa mfumo wa malalamiko na rufaa au kuchukua hatua ya kuadhibu dhidi ya mtoa huduma anayeomba matokeo yaliyoharakishwa au kuunga mkono rufaa ya mshirika.
- Kuhimiza uondoaji wa lalamiko, rufaa, au usikilizaji wa kesi ambao umewasilishwa tayari; au
- Kutumia uwasilishaji au matokeo ya lalamiko, rufaa, au usikilizaji wa kesi kama sababu ya kuchukua hatua dhidi ya mshirika au kuomba kukatisha kuandikishwa kwa mshirika.

Unaweza kutuomba tubadilishe uamuzi tuli ofanya.

Hili linaitwa rufaa.

Ikiwa tutakataa, kukomesha, au kupunguza huduma ya matibabu, meno au afya ya mwenendo, tutakutumia barua ya kukataliwa ambayo inakwambia kuhusu uamuzi wetu. Barua hii ya kukataliwa inaitwa Notisi ya Uamuzi Hasi wa Mafao (NOABD). Pia tutamjulisha mtoa huduma wako kuhusu uamuzi wetu.

Ikiwa hukubaliani na uamuzi wetu, una haki ya kutuomba tu badilishe. Hili linaitwa rufaa kwa sababu unakata rufaa dhidi ya uamuzi wetu.

Fuata hatua hizi ikiwa hukubaliani na uamuzi wetu	
Hatua ya 1	<p>Omba rufaa. Lazima uombe ndani ya siku 60 baada ya tarehe ya barua ya kukataliwa (NOABD).</p> <p>Tupigie simu kwa 877-600-5472 (TTY 877-600-5473) au utumie fomu ya Ombi la Kukagua Uamuzi wa Huduma za Afya. Fomu hiyo hutumwa pamoja na barua ya kukataliwa. Pia unaweza kuipata katika www.trilliumohp.com/members/oregon-health-plan/for-members/handbooks-forms.html.</p>

	<p>Unaweza kutuma fomu hiyo kwa barua kwa:</p> <p>Trillium Community Health Plan PO Box 11756 Eugene, OR, 97440</p> <p>Barua pepe: Appeals@TrilliumCHP.com</p> <p>Pia unaweza kutuma fomu hiyo kwa faksi kwa 844-850-4861.</p> <p>Je, nani anaweza kuomba rufaa? Wewe au mtu aliye na ruhusa iliyoandikwa ya kuzungumza kwa niaba yako. Huyo anaweza kuwa daktari wako au mwakilishi aliyeidhinishwa.</p>
<p>Hatua ya 2</p>	<p>Subiri jibu letu. Baada ya kupata ombi lako, tutapitia uamuzi wa asili. Daktari mpya atapitia rekodi zako za matibabu na ombi la huduma ili kuona ikiwa tulifuata kanuni inavyofaa. Unaweza kutupatia maelezo yoyote ya ziada unayofikiri yataweza kutusaidia kukagua uamuzi huo.</p> <p>Je, mnatumia muda gani kukagua rufaa yangu? Tuna siku 16 kukagua ombi lako na kujibu. Ikiwa tunahitaji muda zaidi, tutakutumia barua. Tuna hadi siku 14 zaidi ili kujibu.</p> <p>Je, itakuwaje ikiwa ninahitaji jibu la haraka? Unaweza kuomba rufaa ya haraka. Hii pia inaitwa rufaa iliyoharakishwa. Tupigie simu au utume fomu ya ombi kwa faksi. Fomu hiyo hutumwa pamoja na barua ya kukataliwa. Pia unaweza kuipata katika www.trilliumohp.com/members/oregon-health-plan/for-members/handbooks-forms.html. Omba rufaa ya haraka ikiwa kusubiri rufaa ya kawaida kunaweza kuweka maisha yako, afya na uwezo wako wa kufanya shughuli hatarini. Tutakupigia simu na kukutumia barua, ndani ya siku 1 ya kazi, ili kukujulisha kwamba tumepokea ombi lako la rufaa ya haraka.</p> <p>Je, rufaa ya haraka huchukua muda gani? Ukipata rufaa ya haraka, tutafanya uamuzi wetu haraka kadiri afya yako inavyohitaji, si zaidi ya saa 72 kuanzia wakati ambapo ombi la rufaa ya haraka lilipokewa. Tutafanya kadiri tuwezavyo kuwasiliana nawe na mtoa huduma wako kwa simu ili kukujulisha uamuzi wetu. Pia utapata barua.</p> <p>Kwa ombi lako au ikiwa tunahitaji muda zaidi, tunaweza kurefusha kipindi cha wakati kwa hadi siku 14.</p> <p>Ikiwa rufaa ya haraka itakataliwa au muda zaidi unahitajika, tutakupigia simu na utapokea notisi iliyoandikwa ndani ya siku mbili. Ombi lililokataliwa la rufaa ya haraka litakuwa rufaa ya kawaida na linahitaji kutatuliwa ndani ya siku 16 au linaweza kurefushwa kwa siku 14 zaidi.</p> <p>Ikiwa hukubaliani na uamuzi wa kurefusha kipindi cha wakati cha rufaa au ikiwa rufaa ya haraka itakataliwa, una haki ya kuwasilisha lalamiko.</p>

Hatua ya 3

Soma uamuzi wetu.

Tutakutumia barua iliyo na uamuzi wetu wa rufaa. Barua hii ya uamuzi wa rufaa pia huitwa Notisi ya Uamuzi wa Rufaa (NOAR). Ikiwa unakubali uamuzi huo, huhitaji kufanya chochote.

Je, bado hukubaliani? Omba usikilizaji wa kesi.

Unaweza kuomba jimbo likague uamuzi wa rufaa. Hili linaitwa kuomba usikilizaji wa kesi. Lazima uombe usikilizaji wa kesi ndani ya siku 120 baada ya tarehe ya barua ya uamuzi wa rufaa (NOAR).

Je, itakuwaje ikiwa ninahitaji usikilizaji wa haraka wa kesi?

Unaweza kuomba usikilizaji wa haraka wa kesi. Huu pia unaitwa usikilizaji ulioharakishwa wa kesi.

Tumia fomu ya mtandaoni ya usikilizaji wa kesi katika www.trilliumohp.com/members/oregon-health-plan/formembers/handbooks-forms.html. Ili kuomba usikilizaji wa kawaida wa kesi au usikilizaji wa haraka wa kesi.

Pia unaweza kupigia jimbo simu kwa 800-273-0557 (TTY 711) au utumie fomu ya ombi iliyotumwa pamoja na barua. Pata fomu hiyo katika www.trilliumohp.com/members/oregon-health-plan/formembers/handbooks-forms.html. Unaweza kutuma fomu hiyo kwa:

OHA Medical Hearings
500 Summer St NE E49
Salem, OR 97301
Faksi: 503-945-6035

Jimbo litaamua ikiwa unaweza kupata usikilizaji wa haraka wa kesi siku 2 za kazi baada ya kupata ombi lako.

Je, nani anaweza kuomba usikilizaji wa kesi?

Wewe au mtu aliye na ruhusa ya kuzungumza kwa niaba yako. Huyo anaweza kuwa daktari wako au mwakilishi aliyeidhinishwa.

Je, nini hufanyika katika usikilizaji wa kesi?

Katika usikilizaji wa kesi, unaweza kumwambia hakimu wa Sheria ya Utawala ya Oregon sababu ya kutokubali uamuzi wetu kuhusu rufaa yako. Hakimu huyo atafanya uamuzi wa mwisho.

Maswali na majibu kuhusu rufaa na usikilizaji wa kesi

Je, itakuwaje ikiwa sitapata barua ya kukataliwa? Je, bado naweza kuomba rufaa?

Lazima upate barua ya kukataliwa kabla ya kuomba rufaa.

Ikiwa mtoa huduma wako anasema kwamba huwezi kupata huduma au kwamba utalazimika kulipia huduma, unaweza kutuomba barua ya kukataliwa (NOABD). Baada ya kupokea barua hiyo ya kukataliwa, unaweza kuomba rufaa.

Je, itakuwaje ikiwa Trillium Community Health Plan itakosa kutimiza muda uliowekwa wa rufaa?

Ikiwa tutachukua zaidi ya siku 30 kujibu, unaweza kuomba jimbo kufanya ukaguzi. Huu unaitwa usikilizaji wa kesi. Ili kuomba usikilizaji wa kesi, pigia jimbo simu kwa 800-273-0557 (TTY 711) au utumie fomu ya ombi iliyotumwa pamoja na barua ya kukataliwa (NOABD). Pata fomu hiyo katika www.trilliumohp.com/members/oregon-health-plan/for-members/handbooks-forms.html.

Je, mtu mwingine anaweza kuniwakilisha au kunisaidia katika usikilizaji wa kesi?

Una haki ya kuwakilishwa na mtu mwingine unayemchagua katika usikilizaji wa kesi. Huyu anaweza kuwa mtu yeyote, kama rafiki, mwanafamilia, wakili, au mtoa huduma wako. Pia una haki ya kujiwakilisha ukichagua. Ikiwa utaajiri wakili, sharti ulipe ada zake.

Kwa ushauri na uwakilishaji unaowezekana wa bila malipo, pigia Simu ya Usaidizi ya Mafao ya Umma kwa 1-800-520-5292; TTY 711. Simu hiyo ya usaidizi ni ushirikiano kati ya Legal Aid of Oregon na Oregon Law Center. Maelezo kuhusu usaidizi wa kisheria wa bila malipo yanaweza kupatikana katika OregonLawHelp.com

Je, bado naweza kupata mafao au huduma huku nikisubiri uamuzi?

Ikiwa umekuwa ukipata mafao au huduma iliyokataliwa na tuliacha kuitoa, unaweza kutuomba tuiendelee wakati wa mchakato wa rufaa na usikilizaji wa kesi. Unaweza kuomba kuendelezwa kwa mafao kwa simu, barua au faksi.

Unahitaji:

- Kuomba hili ndani ya siku 10 baada ya tarehe ya notisi au kufikia tarehe ambayo uamuzi huu utatekelezwa, yoyote itakayokuwa ya baadaye.
- Kutumia fomu ya Ombi la Kukagua Uamuzi wa Huduma za afya. Fomu hiyo hutumwa pamoja na barua. Pia unaweza kuipata katika www.trilliumohp.com/members/oregon-health-plan/for-members/handbooks-forms.html.
- Jibu “ndiyo” kwa swali kuhusu kuendeleza huduma kwenye sanduku la 8 kwenye ukurasa wa 4 kwenye fomu ya *Ombi la Kukagua Uamuzi wa Huduma za Afya*.

Je, lazima nilipie huduma iliyoendelezwa?

Ikiwa utachagua kupata mafao au huduma iliyokataliwa bado, huenda ukalazimika kuilipia. Ikiwa tutabadilisha uamuzi wetu wakati wa rufaa, au ikiwa hakimu atakubaliana nawe wakati wa usikilizaji wa kesi, hutahitaji kulipa.

Ikiwa tutabadilisha uamuzi wetu na hukuwa unapokea huduma au mafao hayo, tutaidhinisha au kutoa huduma au mafao hayo haraka kadiri afya yako inavyohitaji. Hatutachukua zaidi ya saa 72 kuanzia siku tutakayopata notisi kwamba uamuzi wetu ulitanguliwa.

Je, itakuwaje ikiwa nina Medicare pia? Je, nina haki zaidi za rufaa?

Ikiwa una Trillium Community Health Plan na Medicare, unaweza kuwa na haki zaidi za rufaa kuliko zilizo rodheshwa hapo juu. Pigia Kitengo cha Huduma kwa Wateja simu kwa 877-600-5472 (TTY: 877-600-5473) kwa maelezo zaidi. Pia unaweza kupigia Medicare simu kwa 800-633-4227 ili kupata habari zaidi kuhusu haki zako za rufaa.

Maneno ya Kujua

Rufaa – Wakati ambapo unaomba mpango wako kubadilisha uamuzi usiokubali kuhusu huduma ambayo daktari wako aliagiza. Unaweza kupiga simu, kuandika barua au ujaze fomu inayoeleza sababu ya mpango huo kubadilisha uamuzi wake. Hili linaitwa kuwasilisha rufaa.

Agizo la Mapema – Fomu ya kisheria ambayo hukuruhusu kueleza matakwa yako ya huduma za mwisho wa maisha. Unaweza kuchagua mtu wa kukufanyia maamuzi ya huduma za afya ikiwa huwezi kuyafanya mwenyewe.

Tathmini – Ukaguzi wa maelezo kuhusu huduma, matatizo ya huduma za afya, na mahitaji ya mgonjwa. Hii hutumiwa kujua ikiwa huduma zinahitaji kubadilika na kupanga huduma za siku zijazo.

Bili ya salio (kutozwa bili isiyotarajiwa) - Kutozwa bili ya salio ni wakati ambapo unapata bili kutoka kwa mtoa huduma wako ya kiasi kinachosalia. Hili hufanyika wakati ambapo mpango unakosa kulipa gharama kamili ya huduma. Hii pia inaitwa bili isiyotarajiwa. Watoa huduma wa OHP hawapaswi kuwatoza washirika bili ya salio.

Afya ya mwenendo – Hii ni afya ya akili, ugonjwa wa akili, uraibu na magonjwa ya matumizi ya dawa za kulevya. Inaweza kubadilisha hali yako ya hisia, kufikiri, au jinsi unavyotenda mambo.

Malipo ya Mshiriki au Malipo ya Pamoja – Kiasi cha pesa ambacho lazima mtu alipe kwa huduma kama dawa zilizoagizwa na daktari au ziara. Washirika wa OHP hawana malipo ya mshiriki. Bima ya binafsi ya afya na Medicare wakati mwingine huwa na malipo ya mshiriki.

Uratibu wa Huduma – Huduma ambayo hukupatia elimu, usaidizi na nyenzo za jamii. Hukusaidia kushughulikia afya yako na kuelewa jinsi ya kutumia mfumo wa huduma za afya.

Dai la Kiraia – Kesi inayowasilishwa ili kupata malipo. Hii si kesi ya uhalifu. Baadhi ya mifano ni jeraha la binafsi, kupata malipo ya bili, uzembe wa kikazi wa tiba, na ulaghai.

Bima ya kushirikiana – Kiasi ambacho lazima mtu alipe kwa mpango wa afya kwa huduma. Mara nyingi ni asilimia ya gharama, kama 20%. Bima hulipia iliyosalia.

Sheria za Mtumiaji – Kanuni na sheria zinazokusudiwa kuwalinda watu na kukomesha mazoea ya udanganyifu katika biashara.

Shirika la huduma zinazoratibiwa (CCO) – CCO ni mpango wa eneo husika wa OHP ambao hukusaidia kutumia mafao yako. CCOs hujumuisha aina zote za watoa huduma wa afya katika jamii. Hushirikiana ili kuwahudumia washirika wa OHP katika eneo au sehemu ya jimbo.

Mgogoro – Wakati wa shinda, tatizo au hatari. Unaweza kusababisha hali ya dharura ukikosa kushughulikiwa.

Tamko la Matibabu ya Afya ya Akili – Fomu unayoweza kujaza wakati ambapo una mgogoro wa afya ya akili na huwezi kufanya maamuzi kuhusu huduma zako. Hueleza uchaguzi kuhusu huduma unayotaka na usiyotaka. Pia hukuruhusu kuchagua mtu mzima anayeweza kufanya maamuzi kuhusu huduma zako.

Makato – Kiasi unacholipa kwa huduma za afya zinazolipiwa na bima kabla ya bima yako kulipa kilichosalia. Hii ni ya Medicare na bima ya afya ya binafsi tu.

Vifaa vya kuwezesha kupata ujuzi wa kuishi maisha ya kawaida na kuwezesha upya kuishi maisha ya kawaida – Vifaa vya kukusaidia kwa huduma za tiba au kazi nyingine za kila siku.

Mifano ni pamoja na:

- Vifaa saidizi vya kutembea
- Fimbo
- Magongo ya kutembelea
- Vifaa vya kufuatilia glukosi
- Pampu za kutilia dawa mwilini
- Viungo bandia na vifaa vya orthotiki
- Vifaa vya kuwezesha kuona kwa walio na uwezo duni wa kuona
- Vifaa vya mawasiliano
- Viti vya magurudumu vya umeme
- Mashine saidizi ya kupumua

Utambuzi wa Tatizo – Mtoa huduma anapogundua tatizo, hali au ugonjwa.

Vifaa vya kudumu vya tiba (DME) – Vitu kama viti vya magurudumu, vifaa saidizi vya kutembea na vitanda vya hospitali ambavyo hudumu kwa muda mrefu. Huwa haviishi kama bidhaa za dawa.

Hali ya dharura ya meno – Tatizo la afya ya meno linalolingana na dalili zako. Mifano ni maumivu makali au kuvimba kwa meno.

Hali ya dharura ya kimatibabu – Ugonjwa au jeraha linalohitaji matibabu mara moja. Hii inaweza kuwa kutokwa na damu kusikokoma, maumivu makali au mifupa iliyovunjika. Inaweza kuwa kitu ambacho kitafanya sehemu fulani ya mwili wako kuacha kufanya kazi. Hali ya dharura ya afya ya akili ni hisia ya kutokuwa na udhibiti au kuhisi kana kwamba unaweza kujiumiza au kumuumiza mtu mwingine

Usafirishaji wa matibabu ya dharura – Kutumia gari la wagonjwa au Life Flight kupata huduma za matibabu. Wahudumu wa matibabu ya dharura hutoa matibabu wakati unasafiri kwa gari au ndege.

ER au ED – Inamaanisha chumba cha dharura au idara ya dharura. Hili ndilo eneo katika hospitali ambako unaweza kupata huduma kwa dharura ya matibabu au afya ya akili.

Huduma za chumba cha dharura – Huduma unazopata wakati una tatizo baya la afya na si salama kusubiri. Hii inaweza kufanyika katika ER.

Huduma za dharura – Huduma ambazo huimarisha au kutuliza maradhi mabaya ya ghafla au ya afya ya akili.

Huduma zisizojumuishwa – Kile ambacho mpango wa afya haulipii. Mfano: OHP hailipii huduma za kuimarisha sura yako, kama upasuaji wa kuboresha sura au vitu ambavyo huona vyenyewe, kama mafua.

Sheria ya Madai ya Uongo ya Shirikisho na Jimbo – Sheria zinazofanya iwe hatia kwa mtu kutoa rekodi ya uongo huku akijua au kuwasilisha dai la uongo la huduma za afya.

Nung'uniko – Lalamiko rasmi unaloweza kutoa ikiwa hujafurahishwa na shirika lako la CCO, huduma zako za afya, au mtoa huduma wako. OHP huita hili lalamiko. Sheria inasema kwamba mashirika ya CCO lazima yajibu kila lalamiko.

Huduma na vifaa vya kuwezesha kupata ujuzi wa kuishi maisha ya kawaida – Huduma na vifaa ambavyo hufundisha ujuzi wa maisha ya kila siku. Mfano ni tiba ya matatizo ya kunena kwa mtoto ambaye hajaanza kuzungumza.

Bima ya afya – Mpango ambao hulipia huduma za afya. Baada ya kujisajili, kampuni au shirika la serikali hulipia huduma za afya zinazolipiwa na bima. Baadhi ya mipango ya bima huhitaji malipo ya kila mwezi, yanayoitwa *ada za kujisajili*.

Uchunguzi wa Hatari ya Afya – Utafiti kuhusu afya ya mshirika. Utafiti huo huuliza kuhusu afya ya kihisia na mwili, mienendo, hali za maisha na historia ya familia. CCOs huutumia ili kuwaunganisha washirika kwa msaada na usaidizi unaofaa.

Huduma za Afya za Nyumbani – Huduma unazopata ukiwa nyumbani ili kukusaidia kuishi vyema zaidi baada ya upasuaji, ugonjwa au jeraha. Usaidizi wa dawa, vyakula na kuoga ni baadhi ya huduma hizi.

Huduma za Wagonjwa Mahututi – Huduma za kumfariji mtu anayekufa na kusaidia familia yake. Huduma za wagonjwa mahututi zinaweza kubadilika kulingana na hali na zinaweza kuwa matibabu ya kutuliza maumivu, ushauri na utunzaji wa muda ili mtunzaji wa kawaida apumzike.

Huduma za kulazwa na kutolazwa hospitalini – Huduma za kulazwa hospitalini: Unapolazwa hospitalini na kukaa huko kwa angalau usiku tatu (3). Huduma za kutolazwa za hospitalini: Wakati ambapo upasuaji au matibabu yanatolewa hospitalini na kisha unaondoka baadaye.

Kupelekw hospitalini – Wakati ambapo mtu anafikishwa hospitalini kwa matibabu.

Uratibu wa uangalizi makini – Baadhi ya washirika walio na mahitaji maalum ya huduma za afya watapata usaidizi na nyenzo zaidi ili kupata matokeo mema. Mfano wa mtu aliye na mahitaji maalum ya huduma za afya anaweza kuwa:

- Watu wazima walio na umri mkubwa
- Watu walio na ulemavu
- Watu walio na maradhi mengi au sugu
- Watoto walio na matatizo ya mwenendo
- Watu wanaotumia dawa za kulevya za kudungwa kwa IV
- Wanawake walio na ujauzito ulio na hatari ya juu
- Wanajeshi wa zamani na familia zao
- Watu walio na VVU/UKIMWI au kifua kikuu

Medicaid – Mpango wa kitaifa unaosaidia kwa gharama za huduma za afya kwa watu wenye mapato wa chini. Ndani ya Oregon, unaitwa Oregon Health Plan.

Inayohitajika kimatibabu – Huduma na vifaa ambavyo vinahitajika ili kuzuia, kutambua au kutibu maradhi au dalili zake. Pia inaweza kumaanisha huduma ambazo ni matibabu ya kawaida.

Medicare – Mpango wa huduma za afya kwa watu wenye umri wa miaka 65 au zaidi. Pia huwasaidia watu walio na ulemavu fulani wenye umri wowote.

Mtandao – Watoa huduma wa matibabu, afya ya akili, meno, famasia na vifaa ambao wana kandarasi na CCO.

Mtoa Huduma wa Ndani ya Mtandao au Anayeshiriki – Mtoa huduma yeyote anayeshirikiana na shirika lako la CCO. Unaweza kuhudumiwa na watoa huduma wa ndani ya mtandao bila malipo. Baadhi ya wataalamu wa mtandao wanahitaji rufaa.

Mtoa Huduma wa Nje ya Mtandao – Mtoa huduma ambaye hajatia sahihi kandarasi na CCO. Shirika la CCO halilipii washirika ili wahudumiwe nao. Lazima upate idhini ili kuhudumiwa na mtoa huduma wa nje ya mtandao.

Ondoleo la OHP la Makubaliano ya Kulipa (OHP 3165 au 3166) - Fomu unayotia sahihi ikiwa unakubali kulipia huduma ambayo OHP hailipii. Ni halali tu kwa huduma na tarehe mahususi zilizoandikwa kwenye fomu hiyo. Unaweza kutazama fomu tupu ya ondoleo katika <https://bit.ly/OHPwaiver>. Je, huna uhakika ikiwa ulitia sahihi fomu ya ondoleo? Unaweza kuuliza ofisi ya mtoa huduma wako. Kwa lugha za ziada, tafadhali tembelea: www.oregon.gov/oha/hsd/ohp/pages/forms.aspx

Huduma za tabibu – Huduma unazopokea kutoka kwa daktari.

Mpango – Shirika la afya au CCO ambalo hulipia huduma za afya za washirika wake.

POLST – Maagizo Yanayobebeka ya Matibabu ya Kuendeleza Maisha (POLST). Fomu unayoweza kutumia kuhakikisha matakwa yako ya huduma karibu na mwisho wa maisha yanafuatwa na watoa huduma wa tiba.

Huduma za Baada ya Kuimarika – Huduma baada ya dharura za kukufanya uendelee kuwa na hali thabiti, au ili kuimarisha au kuponya tatizo lako

Idhini ya mapema (idhini ya awali, au PA) – Hati inayosema kwamba mpango wako utalipia huduma. Baadhi ya mipango na huduma huhitaji PA kabla ya kupata huduma. Madaktari hushughulikia hili kwa kawaida.

Ada – Gharama ya bima.

Bima ya dawa zinazoagizwa na daktari – Bima ya afya au mpango ambao husaidia kulipia dawa.

Dawa zinazoagizwa na daktari – Dawa ambazo daktari wako hukwambia utumie.

Huduma za kuzuia magonjwa au kinga – Huduma za afya ambazo husaidia kukufanya uwe na afya njema. Mifano ni kupata chanjo ya mafua au uchunguzi kila mwaka.

Mtoa huduma wa msingi (PCP) – Mtaalamu wa tiba ambaye hutunza afya yako. Kwa kawaida ndiye mtu wa kwanza unayempigia simu unapokuwa na matatizo ya afya au unapohitaji huduma. PCP wako anaweza kuwa daktari, muuguzi mtaalamu, msaidizi wa tabibu, tabibu wa mifupa au wakati mwingine daktari wa tiba asili.

Daktari wa meno wa msingi (PCD) – Daktari wa meno unayemwendea kwa kawaida ambaye hutunza meno na fizi zako.

Mtoa huduma – Mtu au shirika lolote ambalo hutoa huduma za afya.

Huduma za kuwezesha upya kuishi maisha ya kawaida – Huduma ambazo hokusaidia kupata tena afya kamili. Hizi husaidia kwa kawaida baada ya upasuaji, jeraha, au matumizi ya dawa za kulevya.

Mwakilishi – Mtu aliyechaguliwa kuchukua hatua au kuzungumza kwa niaba yako.

Uchunguzi – Utafiti au tathmini ya kuangalia matatizo ya afya na mahitaji ya huduma.

Huduma za uuguzi stadi – Usaidizi kutoka kwa muuguzi wa kutunza kidonda, tiba au kutumia dawa yako. Unaweza kupata huduma za uuguzi stadi hospitalini, katika kituo cha uuguzi au nyumbani kwako kwa huduma za afya za nyumbani.

Mtaalamu – Mtoa huduma wa tiba aliye na mafunzo maalum ya kutibu sehemu fulani ya mwili au aina ya ugonjwa.

Kujitua uhai – Kitendo cha kujitua.

Huduma ya afya kwa vifaa vya mawasiliano – Huduma kwa video au huduma kupitia kwa simu badala ya katika ofisi ya mtoa huduma.

Mabadiliko ya huduma – Baadhi ya washirika wanaobadilisha mipango ya OHP bado wanaweza kupata huduma sawa na kuhudumiwa na watoa huduma sawa. Hilo linamaanisha kwamba huduma hazitabadilika unapobadilisha kati ya mipango ya CCO au kuhamia kwa/kuhama kutoka kwa OHP fee-for-service. Hili linaitwa mabadiliko ya huduma. Ikiwa una matatizo makubwa ya afya, mpango wako mpya na mpango wako wa zamani lazima ishirikiane ili kuhakikisha unapata matibabu na huduma unazohitaji.

Mfanyakazi wa afya wa kawaida (THW) – Mfanyakazi wa afya ya jamii ambaye hushirikiana na watoa huduma wa afya ili kuhudumia jamii au kliniki. THW huhakikisha washirika wanatendewa kwa haki. Si THWs wote wamethibitishwa na jimbo la Oregon. Kuna aina sita (6) tofauti za THWs, ikiwa ni pamoja na:

- Mfanyakazi wa afya ya jamii
- Mtaalamu wa ustawi wa wenza
- Mwelekezi wa binafsi wa afya
- Mtaalamu wa usaidizi wa wenza
- Doula wa uzazi
- Wafanyakazi wa Afya wa Kawaida wa Kikabila

Huduma za matibabu ya haraka – Huduma unazohitaji ndani ya siku sawa kwa maumivu makali. Pia inajumuisha huduma za kuzuia jeraha au ugonjwa kuwa mbaya zaidi, au ili kuepuka kupoteza utendakazi katika sehemu ya mwili wako.

Mfichua maovu – Mtu ambaye huripoti ufujaji, ulaghai, matumizi mabaya, ufisadi, au hatari za afya na usalama wa umma.

